

MADA

**UHAKIKI WA FANI KATIKA *TENZI ZA HOWANI MWANA
HOWANI* NA *MWANAKUKUWA ZA ZAYNAB HIMID
MOHAMMED***

NA

LINA AKAKA MBAYI

**UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA CHUO KIKUU CHA
NAIROBI.**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA
JULAI, 2009**


University of NAIROBI Library




0472484 5


IKIRARI


Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.



LINA AKAKA MBAYI
(MWANAFUNZI)



TAREHE

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi.


DR.KINEENE WA MUTISO
(MSIMAMIZI)


TAREHE


DR. RAYYA TIMAMMY
(MSIMAMIZI)


TAREHE

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa:

Lydia O. Mbayi

Na

Habil O. Mbayi

SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwenu nyote mlionishika mkono mkanihimiza na kunitia moyo kila hatua. Siwezi kujidai kuwa jitihada zangu pekee zingeniwezesha kufua dafu bila mchango wa wengine wengi.

Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na siha. Kama si Yeye, kusoma kwangu na changamoto zilizonikabili wakati huo wote nikiwa chuoni zingenizidia na kupelekea kuacha kwangu masomo. Kwa uwezo na neema zake, nimefika nilipofika.

Pili natoa shukrani kwa wazazi wangu ambao kila mara walikuwa wakinitia moyo na kunitaka nisome kwa bidii na hata kuendelea zaidi baada ya kuhitimu katika shahada hii. Dua ambazo mamangu mpendwa Lydia alikuwa akiniombea zimezaa matunda. Asante babangu mpendwa Habil kwa kuwa na imani nami. Nitasoma hadi nifike utakapo wewe.

Wahadhiri katika Idara ya Isimu na Lugha - Chuo Kikuu cha Nairobi wanastahili shukrani. Mchango wao wa moja kwa moja umeacha athari kubwa katika maisha na masomo yangu. Miongoni mwao ni: Profesa M.H. Abdulaziz, Dkt. Mbatiah. Dkt. Alfred Buregeya, Dkt. Tom Olali, Profesa Kithaka Wa Mberia, Dkt. John Habwe, Dkt. Zaja Omboga, Bw. Mungania na Dkt. A. Mukhwana.

Shukrani zangu maalum ni kwa wasimamizi wangu wawili: Dkt. Kineene wa Mutiso na Dkt. Rayya Timammy. Mbali na kuwa walimu wangu, wasomi hawa walihusiana nami kama ndugu na sahibu. Daima nitawakumbuka kwa wema wao.

Wenzangu tuliong'oa nanga pamoja nawashukuru kwanza kabisa kwa kuwajua na kufanya urafiki nanyi. Zaidi ni kwa usaidizi wenu na njia yenu maalum ya kumwondolea mtu wasiwasi hasa mambo yalipopamba moto: Geoffrey Mukabane, Peter Nyaga, John Gitonga, Mary Njeri, Josephine Mulila na Margaret Mwachanya kwa ucheshi wake mwingi; alilichangamsha darasa.

Shukrani zaidi ni kwa Mume wangu mpendwa Nathan Wambua Mutuku aliyenifaa kwa hali na mali. Bw. na Bi. Makhapila kwa kunifaa katika mambo yaliyohusu kusoma kwangu. Asanteni sana kwa vitabu mliyokuwa mnaniazima kila nilipovihitaji, kwa dua na wema wenu pia. Rafiki yangu wa dhati Doris Odongipou, wewe ni zaidi ya rafiki. Dada ulinifaa. Mambo yaliponizidia ulikuwa kando yangu kila wakati ukinitia moyo, ukiniombea na kufadhili kifedha. Asante sana Mola akubariki. Dadangu mpendwa Agnes Imali asante kwa kunisaidia kazi nyumbani wakati nilipokuwa ninasoma. Sijui ingekuwaje bila wewe. Asante sana, Mungu akubariki. Ndugu yangu Alex Nyangule kwa changamoto ulizokuwa ukinipa za kusoma zaidi. Bw. Newton Maungu kwa kunifaa wakati nilipokuwa narudi masomoni, isingekuwa wewe, nisingepata fursa ya kuendeleza masomo yangu. Asante. Mwisho ni kwa wanangu Brian Abucheri na Harrison Mutuku kwa kuwa wanangu, kwa uvumilivu wenu, mapenzi yenu na ari mnipayo kila ninapowaona na kuwafikiria.

YALIYOMO

Mada	i
Ikirari	ii
Tabaruku	iii
Shukrani	iv
Muhtasari	vi
Yaliyomo	vii
Sura Ya Kwanza	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo La Utafiti	9
1.2 Madhumuni Ya Utafiti.....	9
1.4 Sababu Za Kuchagua Mada Hii	10
1.5 Upeo Na Mipaka.....	11
1.6 Msingi Wa Nadharia Ya Utafiti.....	12
1.6.1 Sifa / Kaida Za Nadharia Ya Umuundo.....	16
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii	19
1.8 Mbinu Za Utafiti	24
1.9 Uchanganuzi Wa Data	25
Sura Ya Pili	26
2.0 Utangulizi	26
2.1.0 Dhana Ya Fani	26
2.1.1 Wahusika	28
2.1.2 Mandhari.....	34
2.1.3 Toni.....	37
2.1.4 Wakati.....	40
2.1.5 Usimulizi.....	43

2.1.6 Msuko	48
2.1.7 Umbo	53
2.1.8.0 Lugha	58
2.1.8.1.0 Uhuru Wa Kishairi.....	64
2.1.8.1.1 Msamiati Wa Kilahaja	64
2.1.8.1.2 Kingozi	64
2.1.8.1.3 Msamiati Wa Kiarabu.....	65
2.1.8.1.4 Msamiati Wa Kiingereza	65
2.1.8.2 Mbinu Za Utunzi.....	66
2.1.8.2.1 Mpinduo Sarufi.....	66
2.1.8.2.2 Tabdila	66
2.1.8.2.3 Mazida	66
2.1.8.2.4 Inkisari	66
2.1.8.3 Tamathali Za Usemi	67
2.1.8.3.1 Tashbihi	67
2.1.8.3.2 Sitiari.....	67
2.1.8.3.3 Jazanda.....	68
2.1.8.3.4 Methali.....	68
2.1.8.3.5 Chuku.....	68
2.1.8.3.6 Maswali Ya Balagha.....	69
2.1.8.3.7 Tasfida	69
2.1.8.3.8 Kejeli.....	69
2.1.8.3.9 Tabaini	69
2.1.8.3.10 Sadfa	70
2.1.8.3.11 Misemo	70
2.1.8.3.12 Visawe	70
2.1.8.3.13 Tanakali Sauti	70
2.1.8.3.14 Nidaa.....	71
2.1.8.3.15 Usambamba	71
2.1.8.3.16 Takriri	71
2.1.8.3.17 Taashira / Ishara.....	71

2.1.8.3.18 Utohozi	72
2.1.8.3.19 Mbinu Rejeshi.....	72
2.1.8.3.20 Kinaya.....	72
2.1.8.3.21 Taabini	72
2.1.8.3.22 Ubashiri / Utabiri	73
2.1.8.3.23 Taswira	73
2.1.8.3.24 Nyimbo / Ngomezi	73
2.1.8.3.25 Tashihisi / Uhuishaji.....	74
2.1.8.3.26 Taharuki.....	74
2.1.8.3.27 Visaasili	74
2.1.8.4 Hitimisho	75
Sura Ya Tatu.....	76
3.0 Utangulizi	76
3.1 Umbo	76
3.2 Lugha	80
3.2.1 Uhuru Wa Kishairi.....	80
3.2.1.1 Lahaja Ya Kiamu.....	80
3.2.1.2 Msamiati Wa Kiarabu.....	80
3.2.1.3 Msamiati Wa Kiingereza	81
3.2.2 Mbinu Za Utunzi.....	82
3.2.2.1 Mpinduo Wa Sarufi	82
3.2.2.2 Tabdila	82
3.2.2.3 Mazida	82
3.2.2.4 Inkisari	83
3.2.3 Tamathali Za Usemi	83
3.2.3.1 Tashbihi	83
3.2.3.2 Sitiari.....	84
3.2.3.3 Jazanda.....	84
3.2.3.4 Methali.....	84
3.2.3.5 Maswali Ya Balagha.....	85

3.2.3.6 Tasfida	85
3.2.3.7 Misemo	85
3.2.3.8 Visawe	86
3.2.3.9 Tanakali Sauti	86
3.2.3.10 Nidaa	86
3.2.3.11 Usambamba	86
3.2.3.12 Takriri	87
3.2.3.13 Mbinu Rejeshi	88
3.2.3.14 Taswira	88
3.2.3.15 Taabini	89
3.2.3.16 Nyimbo / Ngoma	89
3.2.3.17 Visaasili	89
3.3 Wahusika	90
3.3.1 Wazazi Wa Mamake Sihadaike	90
3.3.2 Mamake Sihadaike	90
3.3.3 Bibi	92
3.3.4 Wanajamii	92
3.4 Toni	93
3.5 Msuko	95
3.6 Wakati	98
3.7 Usimulizi	99
3.8 Mandhari	100
3.9 Hitimisho	103
Sura Ya Nne	104
4.0 Utangulizi	104
4.1 Umbo	104
4.2 Lugha	106
4.2.1 Uhuru Wa Kishairi	106
4.2.1.1 Lahaja Ya Kingozi	106
4.2.1.2 Lahaja Ya Kiamu	106

4.2.1.3 Msamiati Wa Kiarabu.....	107
4.2.1.4 Msamiati Wa Kiingereza	108
4.2.2 Mbinu Za Utunzi.....	108
4.2.2.1 Mpinduo Wa Sarufi	108
4.2.2.2 Tabdila	109
4.2.2.3 Mazida	109
4.2.2.4 Inkisari	109
4.2.3 Tamathali Za Usemi	110
4.2.3.1 Tashbihi	110
4.2.3.2 Sitiari.....	111
4.2.3.3 Jazanda.....	111
4.2.3.4 Methali.....	113
4.2.3.5 Maswali Ya Balagha.....	113
4.2.3.6 Tasfida	114
4.2.3.7 Tabaini	114
4.2.3.8 Misemo	114
4.2.3.9 Visawe	115
4.2.3.10 Tanakali Sauti	116
4.2.3.11 Nidaa.....	116
4.2.3.12 Taharuki.....	117
4.2.3.13 Usambamba	118
4.2.3.14 Takriri	118
4.2.3.15 Ishara / Taashira.....	119
4.2.3.16 Tauria / Kitanza Ndimi	119
4.2.3.17 Mbinu Rejeshi.....	120
4.2.3.18 Kinaya.....	120
4.2.3.19 Ubashiri.....	121
4.2.3.20 Taswira	121
4.2.3.21 Chuku.....	121
4.2.3.22 Tashihisi / Uhuishaji.....	122
4.2.3.23 Kejeli.....	122

4.2.3.24 Sadfa	123
4.2.3.25 Taabini	123
4.2.3.26 Nyimbo / Ngoma	124
4.2.3.26.1 Wimbo Wa Chenda Naye	124
4.2.3.26.2 Wimbo Wa Chereko	124
4.2.3.26.3 Nyimbo Za Bataani.....	124
4.2.3.26.4 Wimbo Wa Sasambura	124
4.2.3.26.5 Tumbuizo	125
4.2.3.26.6 Ngoma Ya Lelemama.....	125
4.2.3.26.7 Ngoma Ya Bomu.....	125
4.2.3.26.8 Ngoma Za Uromboni.....	125
4.3 Wahusika	125
4.3.1 Mamake Kukuwa.....	125
4.3.2 Babake Mwanakukuwa.....	127
4.3.3 Mwanakukuwa.....	129
4.3.4 Babu Yake Mwanakukuwa.....	130
4.3.5 Somo / Manyakanga / Makungwi.....	130
4.3.6 Wahusika Wa Kike	132
4.3.7 Wanajamii.....	133
4.3.8 Wahusika Wadogo.....	134
4.4 Toni.....	135
4.5 Msuko	141
4.6 Mandhari.....	145
4.7 Wakati.....	147
4.8 Usimulizi.....	150
4.9 Hitimisho	151
Sura Ya Tano	152
5.0 Hitimisho	152
5.1 Mapendekezo.....	157
Marejeleo	158

ALAMA ZILIZOTUMIKA

1. k.h.j – Kama hapo juu
2. T.U.K.I – Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
3. ub. - Ubeti
4. uk. - Ukurasa

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Fasihi ni aina ya sanaa inayotumia lugha kueleza tajriba za binadamu. Kuna mstari mwembamba kati ya historia na fasihi. Zote ni taaluma zinazohifadhi matukio na tajriba za maisha ya binadamu, tofauti inatokana na njia ya mawasilisho. Fasihi hutumia lugha kisanaa. Fasihi ni pana na ina mitazamo mbalimbali: ya kiwasifu, kihistoria, kifalsafa, kiujumi na mtazamo wa ndani. Tutashughulikia mitazamo miwili ya mwisho katika utafiti wetu. Mitazamo hiyo inajihusisha na miundo, maumbo, matumizi ya lugha, arudhi na tanzu kama vipengele vya kuiunda. Mitazamo hiyo inahusika pia na jinsi kazi fulani inavyoundwa kilugha katika viwango vyake mbalimbali bila kuihusisha na mambo au taathira zilizoko nje.

Fasihi imegawika katika matawi mawili: andishi na simulizi. Matawi haya yana tanzu zake. Tutashughulikia utanzu wa ushairi wa tawi la fasihi andishi. Uchunguzi uliokwishafanywa na washairi wa Kiswahili umethibitisha kwamba chanzo na asili ya ushairi wa Kiswahili ni nyimbo. Utafiti wetu unahusu utanzu wa tenzi. Tutashughulikia fani katika tenzi za Zaynab Himid Mohammed za *Howani Mwana Howani na Mwanakukuwa*.

Itakuwa muhimu kuangazia kwa kifupi kumhusu Bi. Zaynab kabla hatujaingilia uhakiki wa kazi zake. Alikuwa mkaazi wa kisiwa cha Zanzibar. Alizaliwa Unguja, tarehe 12/2/1918 na akafariki tarehe 31/12/2002. Alitunga tenzi mbili: *Howani Mwana Howani*,

Kitunguu na Ubani na Utenzi wa Mwanakukuwa ambamo ameendeleza *Howani Mwana Howani*.

Utenzi wa Howani Mwana Howani ulichapishwa kwa mara ya kwanza katika jarida la TUKI kwa anwani *Howani Mwana Howani, Kitunguu na Ubani*. Ulihaririwa na Mulokozi pamoja na Massamba katika mwaka wa (1983). Hatimaye utenzi huo ulichapishwa na TUKI katika mwaka wa (2004) pamoja na *Utenzi wa Mwanakukuwa* kama kazi moja. Anwani *Kitunguu na Ubani* ilidondoshwa katika chapa ya pili. Hakuna uhakiki wowote uliofanyiwa *Utenzi wa Howani Mwana Howani* katika jarida hilo isipokuwa uandishi wa mtiririko wa utenzi wenyewe. Wa Mutiso (2002), aliutarjumi kwa kifupi katika *Kiingereza* na akaangazia kumhusu Zaynabu.

Anwani ya *Howani Mwana Howani* ina maana ya ‘nyamaza mtoto nyamaza.’ Zaynab alimtungia bintiye Sihadaike, akimweleza taabu alizopata tokea ashike mimba yake, alivyoilea hadi alipofikia kujifungua na hapo kazi ya ulezi ikaanza. *Utenzi wa Mwanakukuwa* unaendeleza *Howani Mwana Howani*. Ulichapishwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili katika mwaka wa (2004), miaka miwili baada ya kifo chake.

Utenzi wa Mwanakukuwa unaeleza shida wanazopitia akina mama katika kumkuza mtoto wa kike tokea anapobaleghe hadi anapoozwa kwa mumewe. Kwa maoni yetu, anwani ya utenzi huu ina maana ya, ‘kukua kwa mtoto...’ : yaani kwa maneno mengine ni kazi. Mawazo haya yanamulikwa na mwandishi Said Ahmed Mohammed katika tamthilia yake: *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Mhusika Bi. Haja anamfumbia mwanawe Mambo

na mkewe Sikitu fumbo la kazi ngumu ya ulezi wa mwana kwa kuwapikia vitumbua alivyovitia mchanga. Bi. Haja ana kinyongo na wanawe (Mambo na Sikitu) kwa kumwachilia mjukuu wake Fikirini kufanya urafiki na Hidaya.

Hidaya ni msichana wa kimasikini na anayedhaniwa kuwa kiruka njia na jamii. Bi. Haja alipika vitumbua akavitia mchanga makusudi akijaribu kuwasilisha ujumbe wake. Upishi wa vitumbua ni kazi ngumu sana inayohitaji muda mrefu wa matayarisho na mapishi. Bi. Zaynab anaeleza kazi ngumu na shida wanazopitia akina mama. Kulea mimba, kuzaa na kumkuza mtoto hadi abaleghe na afikie kuolewa ni kazi. Kazi hiyo huwakosesha akina mama usingizi. Bi Haja aliilinganisha kazi ngumu ya upishi wa vitumbua na kazi ngumu ya ulezi wa mwana.

Kwa mujibu wa ushairi wa utanzu wa tenzi, tumeona kwamba itakuwa muhimu kuifafanua dhana hii. Tenzi hujipambanua kwa sifa zake maalum tofauti na aina nyingine za mashairi. Tutaangalia fasiri za wataalamu mbalimbali kuhusu dhana ya tenzi.

Massamba (1983) asema kwamba tenzi ni mojawapo ya tanzu za ushairi. Ni utungo ambao kimaudhui unaeleza tukio fulani linalotokea katika jamii au lililowahi kutokea. Pengine huweza kuwa ni maelezo juu ya wasifu wa mtu, historia au jambo lolote zito linaloelezwa kwa maelezo marefu. Tenzi huwa na beti nyingi hususan kati ya mia moja na elfu moja mia tano.

Fasiri ya Massamba (khj) ina walakini. Kwanza kabisa, si urefu wa shairi unalolipa hadhi ya tenzi, kuna tenzi fupi ambazo hubeba mawazo mazito. Mbali na maudhui, sifa zingine

zinazopambanua tenzi ni mizani. Tenzi huwa na mikondo mitatu ya mizani, 6, 8, na 11 katika kila mshororo. Utenzi huwa na kina kimoja na kina cha kibwagizo huwa ni cha aina ya bahari. Madai kuwa tenzi huwa na beti kati ya mia moja na elfu moja si kweli kwa sababu idadi ya beti huwa ishirini na zaidi, (beti 20-5000).

Mbatiah (2001) asema kwamba utenzi ni aina ya ushairi unaojipambanua kwa urefu wake na uzito wa masuala unayoyashughulikia. Utendi huwa ni mseto wa masimulizi na maelezo yenye urefu wa mamia au maelfu ya beti, juu ya wahusika, tukio au jambo zito....., naye Wamitila (2002) anasema kuwa.....hapana idadi maalum ya mizani katika kila mshororo.....

Kama tulivyokwishataja hapo juu, idadi ya beti za tenzi huwa ishirini kwenda juu na madai ya Wamitila (khj) kuwa tenzi hazina idadi maalum ya mizani katika kila mshororo ni ya kutiliwa shaka kwa sababu idadi maalum ya mizani yake ndiyo sifa mojawapo inayozipambanua kama tenzi.

Kusema kweli, hakuna mtaalamu anayeweza kudai kuwa anaweza kutoa fasiri mwafaka ya dhana hii, zilizopo ni za kuchangiana mawazo. Upungufu huu umetupelekea kuibuka na fasiri yetu ambapo tunafafanua tenzi kama kijitanzu cha ushairi kinachoeleza matukio mazito ya kihistoria, ya kidini na maelezo juu ya wasifu wa mtu kwa mapana; huwa na kina kimoja katika kila mshororo na idadi maalum ya mizani.

Ni muhimu pia kueleza usuli wa tenzi kwani ndio uti wa mgongo wa utanzu wa ushairi. Knappert (1983) anasema kuwa imekuwa vigumu kuandika usuli na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili kwa sababu miswada mingi ilipatikana katika hali mbaya zilizotatiza usomaji. Mingine ikapatikana katika vipande vilivyoonyesha kuwa kuna habari iliyopotea, lakini hata hivyo, walitumia miswada michache waliopata kutia historia ya fasihi ya Kiswahili katika kumbukumbu licha ya mengi waliokuwa wakiambiwa na wenyeji. Baadhi ya miswada iliyopatikana inaonyesha kuwa tenzi zilianza kutungwa mapema katika karne ya kumi na tatu.

Madai ya Knappert yana walakini kwa sababu asilimia themanini na tano ya fasihi ya Kiswahili haiwezi kupatikana katika tenzi pekee. Isitoshe, wingi wa miswada anayoizungumzia Knappert ni ile ya tenzi zilizo na maudhui ya dini ya Kiislamu. Maendeleo ya fasihi ya Kiswahili yameelezwa na wenyeji wenyewe, kupitia nyimbo na mashairi yaliyotungwa na wenyeji. Kwani ina maana kuwa fasihi ya Kiswahili ilianza tu wakati ilipoanza kuandikwa? Je, na wakati ilikuwa inasimuliwa kwa njia ya mdomo, haikuwa fasihi?

Wataalamu wengi katika kazi zao wakiwemo Msokile (1993), Njogu na Chimerah (1999) na wengineo wanasema kuwa ushairi ulitokana na nyimbo zilizoimbwa jandoni na unyagoni, harusini, wakati wa kupanda, kuvuna na kadhalika. Kuna wale wanaosema kuwa mashairi yana usuli wake katika tenzi, kama vile Wamitila (2002).

Msimamo wetu kuhusu madai haya ni kuwa kabla ya tenzi, Waswahili walikuwa na fasihi yao waliyoihifadhi kwa kupokezana kutoka kizazi hadi kingine kwa njia ya mdomo kwa simulizi na nyimbo. Baada ya uvamizi wa wageni kutoka pande mbalimbali za ulimwengu, wenyeji walishuhudia mwingiliano wa tamaduni zao na tamaduni za kigeni kama vile za Kiarabu na Kiajemi.

Wageni Waingereza, Wajerumani na Waturuki walifika Pwani pia kwa shughuli za kimishenari, kibiashara na mengineyo. Kipindi hiki kilishuhudia maandishi ya tenzi za Kiswahili katika hati za Kiarabu na Kirumi. Mfano mzuri ni *Utenzi wa Fumo Liyongo*, uliotungwa na Mohammed Kijumwa katika mwaka wa 1913, zipo sababu nyingi za kutuwezesha kuamini kuwa kulikuwako na utendi simulizi kumhusu Fumo Liyongo kabla ya wakati huu.

Kwa maoni yetu, tenzi za zamani zilijikita katika maudhui ya kidini ingawa suala la tarehe za utunzi wa baadhi ya tenzi ni la mjadala. Baadhi ya tungo pia si kazi asilia za wenyeji bali walizitarjumi tu kutoka lugha ya Kiarabu hadi Kiswahili kwa hati za Kiarabu na Kirumi. Tunavyofikiria sisi ni kwamba matumizi ya msamiati mwingi wa Kiarabu katika tenzi hizi za zamani ni mojawapo ya ithibati kuwa baadhi yazo ni tafsiri tu. Mwingiliano wa tamaduni za Waswahili na Waarabu pia uliathiri pakubwa utunzi wa tenzi za Kiswahili. Kwa hivyo, tutakuwa tukitoa uamuzi mbaya tukisema kuwa tenzi zote zilikuwa tarjumi. Hadi hapo, tumefikia kauli kuwa usuli wa ushairi ni nyimbo.

Kama tulivyotaja awali, maudhui ya dini yalitawala tenzi nyingi zilizotungwa katika kipindi cha utawala wa Kiarabu. Watunzi waliotunga waliisifia dini ya Kiislamu na Mtume Mohammed (S.A.W.) lakini kufikia karne ya kumi na sita, Muyaka bin Haji aliyaondoa mashairi misikitini. Alianza kuibua tungo za upinzani kufuatia kipindi cha utawala wa Omani (1730) katika upwa wa Afrika Mashariki. Kipindi hiki kiliambatana na migogoro ya kisiasa na ustawi wa tabaka la juu la watawala wenyeji na Waarabu. Tabaka hilo liliiga mambo mengi ya utamaduni wa Kiarabu na kusisitiza uzingativu wa mafundisho ya Kiislamu katika masuala ya kimaisha.

Tabaka hili lililokuwa na wasomi wengi wa elimu ya dini lilianza kutunga tungo nyingi za kidini zilizohusu historia ya kuasisiwa kwa uislamu huko Uarabuni. Baadhi ya tenzi hizo ni: *Utenzi wa Ras al-Ghuli*, *Utenzi wa Herekali*, *Utenzi wa Siri li Asirali*, *Mwana Fatuma*, *Utenzi wa Seyyidina Ali* na nyinginezo.

Ustawi wa miji ya Waswahili ulipoanza kuanguka kwa sababu ya uvamizi wa nchi za kigeni kama vile Ureno na Oman, watunzi walibuni tungo za falsafa, mawaidha na utamaduni. Baadhi ya tenzi hizo ni *Al-Inkishafi*, *Dural Mandhuma*, *Wajiwaji* na baadaye *Mwana Kupona*. Baada ya zaidi ya miaka mia moja, watunzi kama vile Shabaan Robert, Zaynab Himid na wengineo, waliendelea kutunga tungo za utamaduni na mawaidha. Ni maoni yetu kuwa, aina hii ya maudhui ilinawiri sana katika enzi za watunzi hawa kwa sababu ya kufifia kwa mifumo ya kitamaduni ya jando na unyago. Tenzi zikabaki kama njia ya pekee ya kufundisha jamii maadili.

Mbali na Zaynab Himid Mohammed, watunzi wengine wa kike waliotunga tenzi ni:

Binti Bwana Lemba, Mwana Mwarabu (1663) aliyetunga *Utenzi wa Siri li Asirali*, *Utenzi wa Mwana Kupona* ulitungwa na Mwana Kupona binti Mshamu (1858), Mwana Bukhalasi aliyetunga *Utenzi wa Masahibu* na Binti wa Said Amini bin Said Uthman (Mwana Sayyid Amini) alitunga *Utenzi wa Mwana Fatuma*. Haijulikani iwapo Mwana Sayyid ndiye mtunzi au aliuandika upya tu utenzi huu lakini kuondoa shaka hilo mwenyewe katika beti za (438 na 446) anasema:

Nami ni mwane Amini, nimezoandika, yuwani

Ni mwakwe shingoni, atatuhifazi Jalia.

Mezoandika, yuwani, mwane Saidi Amini.

Wa Saidi Usmani, kabila Mahadalia.

Baadhi ya tenzi zilizotungwa na wasanii wa kike zinaingia katika fungu la tungo za mawaidha na utamaduni. Utunzi wa tenzi za ‘wosia’ uliigwa na baadhi ya wasanii kama vile: Shaaban Robert katika tungo zake, *Tenzi za Hati na Adili*, Semghanga akatunga *Kidani cha Huba na Ewe Mwana* katika diwani yake ya *Teuzi za Nafsi* (1971) na Said Karama akatunga *Wasia wa Baba*.

Tutahakiki fani katika tenzi mbili za Zaynab kwa misingi ya nadharia ya umuundo. Nadharia hii ndiyo huipa fasihi mwelekeo wa uhakiki wa kimuundo ambao pia ndio msingi wa nadharia hiyo. Nadharia hii inasisitiza uhakiki wa kimatini wa kazi za fasihi pasipo urejelezi wa nje, kinyume na uhakiki unaorejelea jamii. Hata hivyo uhakiki wa kifani unaweza kuiakisi jamii lengwa kwa sababu fani zinazotumiwa huchotwa katika jamii yenyewe. Baadhi ya fani ambayo huiakisi jamii ni kama vile wahusika, mandhari

na matumizi ya lugha. Vijenzi hivyo vya fani ni vielekezi vinavyotumiwa na msanii kuhakiki jamii inayorejelewa katika kazi ya fasihi.

1.1 TATIZO LA UTAFITI

Katika tafiti zetu za tenzi, pamoja na uhakiki ambao tayari umefanyiwa baadhi ya tenzi, hakuna uhakiki unaojulikana nasi ambao umepata kufanyiwa tenzi za Bi. Zaynabu Himid za *Howani Mwana Howani na Mwanakukuwa*.

Tunakusudia kuhakiki wahusika, umbo, usimulizi, lugha, toni, wakati, msuko na mandhari kama vipengele vya fani katika tenzi hizi. Tutaongozwa na nadharia ya umuundo katika uhakiki wetu kwa sababu itatusaidia kujibana katika uhakiki wa vipengele hivi kimatini bila kuwa na urejelezi wowote wa nje.

Tatizo la uchunguzi lililotupelekea kufanya uhakiki wa kifani wa tenzi hizi ni kutokuwepo kwa kazi za kihakiki za tenzi nyingi za Kiswahili. Kazi zilizofanywa na wageni wa kizungu za kuzikusanya, kuziandika katika hati za Kirumi na kuzihariri tenzi hazitoshi kukidhi haja ya kiusomi katika lugha ya Kiswahili. Ukweli huu ulitulia changamoto ya kuendeleza kazi hizo alipoiachia mzungu kwa kutoa mchango wetu katika kuzihakiki. Tenzi hizi mbili hazijapata kuhakikiwa kifani wala hata kushughulikiwa zaidi kwa namna yoyote ile. Utafiti wetu unapania kujaza pengo lililopo kwa sasa la kukosa uhakiki hususan wa kifani ambao hujawahi kufanyiwa tenzi hizi.

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti wetu umeshughulikia maswala yafuatayo:

- i) Uchunguzi wa muundo wa ndani na wa nje wa *Tenzi za Howani Mwana Howani na Mwanakukuwa*.
- ii) Kubainisha mandhari mbalimbali yanayojitokeza katika tenzi za Zaynab Himid Mohammed.
- iii) Kuchunguza lugha kama ilivyotumiwa na Zaynab Himid Mohammed.
- iv) Kuchunguza usawiri wa wahusika.
- v) Kubainisha usahili au uchangamani wa msuko.

1.3 NADHARIA TETE.

Utafiti huu umefanywa kwa misingi ya nadharia tete zifuatazo:

- i) Tenzi zina muundo wa ndani na wa nje
- ii) Sifa za wahusika zinajitokeza katika maelezo ya msanii kuwahusu, matendo yao pamoja na mazungumzo yao wenyewe kwa wenyewe.
- iii) Msanii ametumia mandhari mbali mbali kutegemea matukio na wahusika.
- iv) Msuko katika tenzi zote ni sahili.
- v) Msanii ametumia lugha kisanaa na kishairi.

1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Tenzi zote mbili zilitungwa na Bi. Zaynab Himid Mohammed: *Howani Mwana Howani* ulichapishwa mwaka wa (1983) na *Mwanakukuwa* ukachapishwa mwaka wa (2004), miaka miwili baada ya kifo chake.

Tumechagua mada hii kwa lengo la kutoa mchango wetu katika taaluma ya kiusomi. Tunatarajia kwamba uhakiki huu utakuwa wa manufaa kwa wasomi wa Kiswahili. Watakapopata nafasi ya kusoma kazi yetu watagundua kuwa tenzi, ambazo watu wengi

huchelea kuzisoma kwa sababu ya urefu wazo pamoja na sifa zake za matumizi ya msamiati wa Kiswahili cha kale na msamiati wa Kiarabu, zitaweza kueleweka kwa urahisi.

Tulipopitia kazi za uhakiki wa kimuundo wa tenzi uliofanywa na wahakiki waliotangulia, tuligundua kuwa wengi wamefanya uhakiki wao kwa misingi ya nadharia za ufani au urasimu. Tunaazimia kujaribu nadharia ya umuundo katika uhakiki wa fani katika tenzi mbili za Zaynab tulizochagua kushughulikia.

1.5 UPEO NA MIPAKA

Tutashughulikia uhakiki wa fani katika *Tenzi za Howani Mwana Howani na Mwanakukuwa*. Tutazidurusu tenzi hizo, hatimaye tuvatambue na kuvielezea vipengele vya fani. Uhakiki wetu utafanywa kwa misingi ya nadharia ya umuundo ambayo husisitiza uhakiki wa kifasihi kimuundo bila ya urejelezi wa nje.

Utafiti wetu utajikita katika ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya fani kama vile wahusika, lugha (tamathali za usemi, msamiati wa lahaja, Kiingereza na Kiarabu), msuko, mandhari, usimulizi, umbo, toni na wakati. Fani na maudhui ni mambo mawili yasiyoweza kutenganishwa. Fani ndiyo malighafi yanayojenga kazi yoyote ile ya kifasihi, kwa sababu hiyo, tutayapitia maudhui kijuujuu. Lengo la utafiti wetu ni kuhakiki fani na iwapo tutaliingilia swala la maudhui kwa kina tutakuwa tunakiuka upeo na mipaka ya utafiti wetu.

Tutaangalia wanayosema wanafasihi mbalimbali kuhusu fani. Tutayatathmini mawazo yao na kutoa maoni yetu itakapobidi. Tutazisoma tenzi tunazoshughulikia na tubainishe iwapo kazi hizi zimejengeka kwa fani zote tunazoazimia kuzihakiki. Licha ya kutoa maelezo kuhusu vipengele mbalimbali vya fani, tutanukuu pia mifano kutoka katika *Tenzi za Howani Mwana Howani na Mwanakukuwa* kama ithibati kuwa mtunzi wa tenzi hizi amezitumia katika kazi yake.

1.6 MSINGI WA NADHARIA YA UTAFITI

Utafiti huu utafanywa kwa misingi ya nadharia ya umuundo. Tumeichagua nadharia hii kwa sababu itatufaa sana katika uhakiki wa fani. Ufaafu wake unatokana na sifa ya nadharia hii ya kuangalia uhakiki wa kazi ya kifasihi kwa misingi ya fani zilizotumika katika matini bila kwenda nje yake. Hii nadharia itatuelekeza katika kuchanganua vipengele mbalimbali vya fani katika tenzi mbili tulizochagua kuhakiki

Hawthorn (1994) anasema kuwa mradi wa umuundo ulikuwa ukikuza ushairi ambao utakuwa kwa fasihi kama isimu ilivyo kwa lugha. Kwa hivyo, ushairi hautapania kueleza maana ya kazi husika. Utajaribu kuweka wazi mfumo wa maumbo na kaida zinazoweza kazi za kifasihi kuwa na maumbo na maana zilizo nazo.

Haya maoni ya Hawthorn (khj) yanamulikwa na wanaumuundo pamoja na wahakiki wa fasihi kimuundo. Tunakubaliana naye kwa sababu kazi za fasihi hubainishwa na kazi za matawi mengine ya isimu kwa sababu ya fani. Fani huchukua asilimia tisaini ya ujenzi wa kazi ya kifasihi. Maudhui hayatoshi kufanya kazi iitwe ya kifasihi kwa sababu hata

uandishi wa magazeti unaweza kumulika moja kwa moja yaliyomo katika kazi za kifasihi kwani yanahusu jamii.

Oxford Advanced Learners Dictionary (2005) yasema kuwa nadharia ya umuundo inaangalia matini kama umbo lililo na sehemu kadha wa kadha ambazo huwa tu na maana zinapohusishwa na zingine katika matini husika. Madai kama haya yanaelekea kupuuza nafasi ya msomaji katika ufasiri wa maana ya matini.

Mbatiah (2001) anasema kwamba umuundo ni nadharia ya uhakiki iliyoibuka katika kipindi cha miaka ya hamsini hadi sitini, na ambayo inashughulikia fasihi katika misingi ya mawazo ya mwanaisimu anayejulikana kama Ferdinand de Saussure. Katika mwelekeo wa umuundo, fasihi inaangaliwa kama mfumo wa ngazi ya pili unaotegemea mfumo wa ngazi ya kwanza ambao ni lugha. Uhakiki wa kimuundo unatumia dhana za kiisimu katika uchambuzi wa matini za kifasihi. Umuundo unaangaliwa na wahakiki wengi kama nadharia iliyotokana na ufani.

Madai ya Mbatiah (khj) yamemulika kipengele cha fani cha lugha na kupuuza vipengele vingine kwa hivyo yana upungufu. Hata hivyo kipengele cha lugha ndicho kitovu cha fani kwani ndicho hutumiwa kujenga vipengele vingine vya fani.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), umuundo ni istilahi inayotumiwa kuelezea aina ya uhakiki ambao unachunguza kaida zilizopo katika uundaji wa kazi fulani. Ukuaji wa nadharia ya umuundo unahusiana na isimu kwa kiasi kikubwa. Mawazo ya isimu kama

mfumo au muundo unaathiri wahakiki wa ki-umuundo wanaoiona kazi ya kifasihi kama muundo. Umuundo unatilia mkazo kwenye muundo wa kazi. Wana-umuundo wanashikilia kuwa fasihi imepangwa kama lugha. Kutokana na ujuzi wetu wa isimu tunajua kuwa lugha ina viwango mbalimbali ambavyo kwa jumla huzaa mfumo wa lugha hiyo.

Mawazo ya Wamitila (khj), kuwa fasihi imepangwa kama lugha yana maana kwamba kwa vile lugha ni mfumo, fasihi nayo ni mfumo. Tunakubaliana na kauli hii kwa sababu mfumo wa fasihi umejengwa na vipengele mbalimbali vya fani. Mfumo wa lugha nao unajumlisha sauti na ishara.

Nadharia ya umuundo iliasisiwa na wanaisimu wa Shule ya Prague kati ya miaka 1928 na 1946 wakiwemo Roman Jakobson, Trubetzkoy, Claude Levi Strauss na wengineo ambao walihusika na urasimu wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Wasomi hawa waliathiriwa na mawazo ya wahakiki wa kirasimu wa nchi za Zeshi, pamoja na mawazo ya Ferdinand de Saussure kuhusu dhana za ujumla lugha (*langue*) na matumizi lugha (*parole*). Dhana hizi zilishughulikia uhusiano wa ishara inayotumiwa katika lugha na kiashiriwa chake au ishara (*signifier*) na kitajwa (*signified*). Waliendeleza mawazo ya De Saussure kuwa maneno yalikusiana kimlalo (*syntagmatic*) na kimuimo (*paradigmatic*). Katika uhusiano wa kimlalo, maneno huungana, kukubaliana na kuingiliana katika matini hivyo basi kuibua maana. Katika uhusiano wa kimuimo, fahiwa mbalimbali za maneno zaweza kutumiwa kurejelea neno moja katika matini na bado maneno hayo tofauti yabebe maana moja.

Saussure alichanganua lugha kisinkronia tofauti na wanafilolojia waliokuwa wakichanganua lugha kimaendeleo. Saussure aligundua kuwa lugha ina sifa ya urejelezi katika njia ambayo maneno hufafanuliwa kwa kuhusiana. Alisisitiza kuwa maneno hayana uhusiano wowote na kile kinachoashiriwa. Kati ya maneno yafuatayo, kuna uhusiano wa kimaana:

mchele

pilau

wali

biriani

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Iwapo maneno pilau, wali na biriani hayangekuwepo, neno mchele lingepanuliwa maana kujumlisha maana za yale maneno matatu ya mwisho.

Jambo lingine muhimu ambalo Saussure alizungumzia ni wazo kuwa uelewa wetu wa vitu unaathiriwa na lugha inayotumiwa kuvieleza. Wamagharibi wanachukulia kuwa, Waarabu wazalendo wa mrenge wa kushoto ni magaidi lakini katika nchi zao wanachukuliwa kama wazalendo wanaopigania ukombozi wa wazalendo.

Saussure alibaini kuwa *parole* ni lugha ya kimatumizi ilhali *langue* ni mfumo lugha ulio na jumla ya taratibu za lugha ambazo kila msemaji wa lugha hizo anazifahamu. Fasihi inaweza kuangaliwa kama mfumo ulio na kanuni, taratibu na sheria zake. Kila msanii wa fasihi lazima auelewe mfumo wa fasihi, aelewe jinsi fasihi inavyoweza kutumiwa kama njia ya mawasiliano kijamii na hata kimuundo.

Kazi ya mhakiki ni kuweza kubainisha vipengele mbalimbali vya fani za kifasihi anavyofafanua lugha na sheria zake. De Saussure ana mtazamo wa kisinkronia wa lugha, jambo ambalo linapelekea kuwepo kwa isimu-miundo.

1.6.1 SIFA / KAIDA ZA NADHARIA YA UMUUNDO

Nadharia ya umuundo ina baadhi ya kaida au sifa zifuatazo:

1. Maana hutokea kupitia tofauti. Maana haitokani na kutambulisha kiashirii na kifaa katika ulimwengu halisia; dhana iliyoishi kabla ya ukweli au uhalisia fulani muhimu. Inatokana na tofauti kati ya viashirii katika mfumo wa kuashiria maana za maneno: Mwanamke na bibi yanahusiana katika viko vya maana na yote yanamrejelea binadamu wa kike lakini tofauti hizo zinatokana na virejelewa bali si uhalisia au hali yoyote.
2. Uhusiano baina ya ishara ni wa ujirani na ubadilishanaji, uunganishaji na uteuzi. Mambo haya husababisha kuwepo kwa 'sarufi' zote, ubadilishanaji, uwezo wa kujua kitu kupitia kingine na zaidi ya yote istiari na metonimia. Wazo la uunganishaji na uteuzi hutoa msingi wa uchanganuzi wa kifasihi au kishairi katika matumizi ya uradidi na kubadilika kwa mikondo ya sauti na miungano. Hutoa pia nafasi muhimu kwa vipengele vya kimsingi vya utamaduni.
3. Umuundo unatambua kuwa ulimwengu wetu dhahania umeundwa kutokana na vinyume, ulinganuzi, ukinzani na uwiliuwili ambamo maana hupatikana. Dhana hizi zinaweza kutumiwa katika uhakiki wa kimuundo kuhakiki wahusika, lugha na mandhari.
4. Umuundo hujenga msingi wa semiotiki: mtalaa wa ishara. Ishara ni muungano wa kiashiria na kiashiriwa na pia ni kitu kinachowakilisha kingine (au

alivyosema Umberto Eco 1976: ishara ni kitu chochote kinachoweza kutumiwa kudanganya). Wazo ambalo hatukubaliani nalo kwa sababu kila ishara inawakilisha dhana katika ulimwengu halisi wala haiwezi kutumiwa kudanganya.

5. Kilicho cha muhimu katika semiotiki ni misimbo ambayo huzipa ishara muktadha: Misimbo ya kitamaduni, kifasihi na mingineyo. Usomi wa semiotiki na misimbo hufungua usomi wa kifasihi kwa usomi wa kitamaduni. Hupanua pia malighafi ya mhakiki katika kujadili maana za matini kwa kujenga au kutambua maana kutegemea uhusiano wa ishara zinazojumlisha vikoa vya maana katika utamaduni. (Mtandao).

Kaida hizi zinaelekea kuisisitiza uhakiki wa kimuundo wa kazi za kifasihi huku zikijikita sana katika matumizi ya lugha; hususan maneno katika lugha yanavyohusiana kujenga maana (kimlalo na kimuimo) na usambamba unaotokea katika matumizi ya maneno na uumbaji wa wahusika.

Wafuasi wa umuundo wanaamini kuwa kazi ya kifasihi haina urejelezi wa nje. Kwa kutokuwa na urejelezi huu, kazi hiyo inaishia kutufanya tuiwazie hali yake ya lugha. Maoni yao ni kuwa neno halihitaji urejelezi ili lipate maana. Mkabala huu huiangalia lugha kama mfumo unaojitosheleza. Mfumo huo hautegemei kusudi la msemaji au wasemaji (mwandishi au waandishi). Ulimwengu wa nje au wa kiurejelezi au hata mfasiri hana mchango mkubwa katika kuizaa maana ya kazi.

Umuundo humpuuza mwandishi katika uhakiki wake ili kufichua au kuweka wazi mifumo au harakati za kiuashiriaji ambazo zinatokea katika kazi hiyo. Kwa wahakiki wa ki-umuundo, viashirii vina maana na uzito mkubwa kuliko viashiriwa. Hii ina maana gani? Mhakiki wa ki-umuundo anaelekea kuvutiwa zaidi na jinsi maana inavyozushwa au kukuzwa kuliko maana yenyewe. Hii ni sifa ambayo kwa kiasi kikubwa inauhusisha mtazamo huu na uhakiki mpya na urasimu wa Kirusi. Hata hivyo wana-umuundo hawaimiliki maana ya kazi kama wanavyofanya wana uhakiki mpya. Wana urasimu kwa upande wao wanauona uhusiano uliopo kati ya fasihi na mbinu za kiukanushi na kiupinzani. Wana umuundo kwa upande wao huuona kama wa ki-usambamba au ki-homolojia (mfanano).

Umuundo unatilia mkazo miundo ya kiuashiriaji katika kazi ya kifasihi. Mkabala huu hupuuza masuala yanayohusiana na yaliyomo au maudhui ya kazi fulani. Kwao kazi ya kifasihi huwa ni udhihirishaji wa muundo wa kijumla. Udhihirishaji huu huwa ni aina moja tu ya uwezekano mbalimbali. Maana ya kazi ya kifasihi, kwa maoni yao, inatokana na sheria na kaida mbalimbali za mifumo tofauti ya kuashiria. Maana haitokani na mtu (mwandishi au msomaji). Huu ndio msingi wa dhana inayojulikana kama ugatuzi wa nafsi katika nadharia ya umuundo.

Nadharia ya umuundo huweka mkazo mkubwa kwenye unasibishi wa maana. Maana nasibishi ya neno ni maana inayohusishwa na neno hilo wala siyo kile kinachorejelewa. Neno 'jogoo' kwa mfano lina maana husishi, kuku ambaye ni wa kiume na anayewika. Maana yake nasibishi ni mwanamume awapendaye wanawake sana. Labda katika

mazingira ya nchi ya Kenya neno hili litakuwa na maana nyingine nasibishi, ya chama cha kisiasa chenye wasifu fulani .

Wamitila (2003) anasema kuwa, mawazo ya umuundo yanaendelezwa na baadhi ya mengine kupingwa na uhakiki wa ki-umuundoleo. Mtazamo huu unahusishwa kimsingi kwa kiasi kikubwa na mhakiki wa kifaransa anayeitwa Jacques Derrida.

Baada ya kupitia mawazo ya wataalamu mbalimbali kuhusu nadharia ya umuundo, kuna mambo yanayojitokeza ambayo yanamulikwa na kila mwanaisimu. Nadharia ya umuundo ina misingi yake katika mawazo ya Ferdinand de Saussure. Inasisitiza uhakiki wa kazi pasipo kuihusisha na jamii wala mwandishi, inapuuza ufasiri wa msomaji na inaangalia jinsi maneno yalivyopangwa na kuhusiana ili kutoa maana lakini isiyo na urejelezi wa nje. Wana-umuundo wanaangalia maana ya kila neno katika sentensi na linavyohusiana na maneno jirani. Isitoshe, wanaangalia umbo la kazi kimofolojia (mizani), kifonolojia (sauti au kiimbo), kisintaksia (mpangilio wa sentensi) na kisemantiki (maana ya maneno).

Wanaisimu wengi waliotoa michango yao kuitetea nadharia hii walisisitiza uhakiki wa matini bila kuihusisha na lolote kutoka nje. Tunadhamiria kuzihakiki kazi zetu na kutathmini ufanisi wa mtunzi katika kutumia vipengele mbalimbali vya fani kwa mujibu wa shule ya mawazo ya wanaisimu wa *Prague*.

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Historia ya tenzi inarudi nyuma katika karne ya kumi na tatu pwani mwa Afrika Mashariki. Itatarajiwa kuwa uhakiki wa tenzi umeshughulikiwa sana na wahakiki wa

kifasihi. Ajabu ni kwamba habari za kiusomi kuhusu tenzi zimebaki kuwa adimu. Kazi nyingi kuhusu tenzi zilizofanywa na wageni wa kizungu zilihusu ukusanyaji wa miswada kutoka kwa wenyeji, uandishi katika hati za kirumi, tarjumi na uhariri wa tenzi zilizopatikana. Wageni walizihakiki kimuundo kwa kiasi kidogo sana.

Uhakiki wa tenzi mbalimbali umeshughulikiwa kwa kiwango kidogo sana kwa sababu ya matumizi ya lahaja mbalimbali za Kiswahili na msamiati wa Kiarabu ambao huwatatiza wasomaji kuelewa. Hata hivyo baadhi ya tenzi zimehakikiwa isipokuwa tunazozishughulikia.

Kazi ambazo zimeshughulikia uhakiki wa tenzi za Kiswahili na zitakazotunufaisha ni:

Tasnifu ya M.A. ya Mungai (2005) ambamo amehakiki ulinganishi wa kifani wa *Tenzi za Swifa ya Nguvumali na Mikidadi na Mayasa* kwa misingi ya nadharia ya ufani au urasimu. Tumefaidika sana kutokana na ufafanuzi wake wa vipengele vya fani. Mifano aliyorejelea kutoka katika tenzi alizoshughulikia imetupa mwanga zaidi katika kazi yetu.

Wesah (2005) katika tasnifu yake ya M.A. ameshughulikia uhakiki wa kifani katika *Utenzi wa Siri li Asirali na Utenzi wa Fatuma* kwa misingi ya nadharia ya urasimu wa Kirusi. Kazi hii imetupa mwanga hasa katika ufafanuzi wa vipengele mbalimbali vya lugha.

Maina (2005) katika tasnifu yake ya M.A. ameshughulikia nafasi ya mwanamke katika tenzi mbili za Shaaban Robert : *Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili*. Amezihakiki kwa

msingi ya nadharia ya ufeministi. Kazi hii ina manufaa sana kwetu kwani imetufaidi katika kutathmini sifa za wahusika wa kike katika kazi yetu.

Wa Mutiso (1985) ameshughulikia maudhui ya Hurafa na Uyakiniifu katika *Utenzi wa Hamziyya*. Katika tasnifu yake ya M.A amelinganisha sifa apewazo Mtume Muhammadi S.A.W. na zile za mashujaa wengine duniani. Aliitafsiri *Kasida ya Hamziyya* kwa Kiingereza na kuihakiki pia katika *The Hamziyya Epic: Translation and Commentary*. Amehakiki *Kasida ya Burudai* (1996) katika tasnifu yake ya PhD na kuitafsiri katika Kiingereza. Ameshughulikia swala la fasihi zilizo na msingi ya kiislamu na ambazo zimeandikwa au kutarjumiwa kwa Kiswahili. Alitafsiri utenzi wa Fatuma katika *the Epic of Princess Fatuma* (2002), *Utenzi wa Siri li Asirali* katika *Epic of Secret of all Secrets* (2003). Katika mwaka wa 2005 alishughulikia *Kasida ya Hamziyya* ambayo ameifasiri kwa undani zaidi. Alihakiki fani yake katika tarjumi 'Maelezo na Uhakiki', kazi ambayo imechapishwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) Tanzania.

Kazi zote za Wa Mutiso zimetunufaisha haswa katika kipengele cha fani cha matumizi ya lugha kwa sababu tumeweza kutathmini jinsi alivyohakiki lugha iliyotumiwa na watunzi katika baadhi ya kazi alizohakiki na kwa hivyo zimetupa mwelekeo wa jinsi tumekishughulikia kipengele hicho.

Wa Mberia (1989) alihakiki *Utenzi wa Fumo Liyongo* ambamo alitathmini sifa za Fumo Liyongo kama shujaa wa masimulizi. Kazi hii imetupa mwanga katika uhakiki wa wahusika katika kazi yetu. Muhammed Seif Khatib (1985) alihakiki nafasi ya mwanamke

katika *Utenzi wa Mwana Kupona*. Kazi yake imetusaidia katika uhakiki wa wahusika wa kike katika kazi yetu. Abdulaziz (1968) alichambua matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* naye Kadenge (1982) alishughulikia ukiushi wa lugha iliyotumiwa katika utenzi huo. Kazi hizi zimetupa mwanga katika kuainisha na kutathmini vipengele mbalimbali vya lugha katika kazi yetu.

Olali (2004) alishughulikia Kasida ya Hamziyya katika tasnifu yake ya PhD, katika kazi yake : *The Veneration of The Prophet: The Role of Kasida ya Hamziyya during the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya*. Kazi hii imekuwa ya manufaa sana katika utafiti wetu kwa sababu imetupa mwanga kuhusu utamaduni wa Waswahili. Imetusaidia katika kuhakiki kipengele cha wahusika, mandhari, lugha na toni.

Mbali na wasomi wenyeji wa kiafrika kuzihakiki tenzi za kale ingawa kwa kiwango kidogo, wageni wa kizungu wanastahili hongera kwa kujibidiisha katika kuzikusanya, kuziandika katika hati za Kirumi na kuzihariri. Baadhi ya wageni waliotoa mchango wao katika kuzishughulikia na kuzihifadhi tenzi hizo ni:

Lyndon (1962) ameshughulikia tenzi mbalimbali kwa kuzitafsiri na kuzihariri kwa Kiingereza. Ameshughulikia *Tenzi za Mwana Kupona, Ras-al-Ghuli, Inkishafi na Utenzi wa Hati, Adili na Liyongo*.

Allen (1971) ametarjumi *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* kwa Kiingereza .

Knappert (1979) alikusanya tenzi mbalimbali akazitafsiri kwa Kiswahili, katika kazi yake alihakiki muundo wa mizani na vina kwa jumla. Knappert (1964) alihariri *Utenzi wa Yaaqubu na Yusufu, Utenzi wa Maisha ya Nabii Adamu, Utenzi wa Seyidini Ali na Mudhari bin Darimi* na *Utenzi wa Mwana Hasina na Rashidi Walii*. Knappert (1967) alitafsiri *Utenzi wa Miiraji na Utenzi wa Tambuka* katika Kiingereza. Lienhardt (1968) amehariri *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na kuutafsiri kwa Kiingereza Werner (1932) alitafsiri beti mia moja sitini na moja za *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*.

Dammann (1940) amegusia kidogo *Utenzi wa Mwana Fatuma* kwa lugha ya Kijerumani, kazi ambayo si ya maana sana kwetu kutokana na kutoimudu kwetu lugha ya Kijerumani. Hata hivyo, tunampongeza kwa juhudi zake za kutarjumi utenzi huu kwa lugha ya Kijerumani. Kazi yake bila shaka imewafaa wengine wengi wanaoelewa lugha hiyo. Jan Knappert (1979:120-127) pia anautaja *Utenzi wa Fatuma* kwa mpito tu, hasa mtiririko wa hadithi. Anaeleza tu jinsi mambo yanavyotokea katika utenzi huu pasipo kuhakiki chochote.

Miswada ya tenzi ilikuwa mali ya mtu binafsi na ilipatikana katika nyumba za watu. Tenzi nyingi ziliandikwa kwa hati za Kiarabu lakini wageni wa Kijerumani waliokuja pwani mwa Kenya wakaziandika katika hati za Kirumi. Baadhi ya tenzi hizo ni: *Kutawafu kwa Nabii Muhammad, Shufaka* ulioandikwa katika hati hizo na Carl G. Buettner, *Ayubu MwanaKupona, Mikidadi na Mayasa* na Dkt. Alice Werner, *Miiraji, Esha, Fatuma, Abdur Rahamani, Andharuni, Ngamia na Paa*, Prof. Ernst Dammann,

Wadachi, Kiyama, Abdur Rahmani, na Bwana J.W.T Allen, Vita vya Uhudi na Bwana H.E. Lambert.

Kazi zote tulizozinukuu, zilishughulikiwa na wageni wa kizungu. Kazi hizi ndizo zilizowatia wasomi wenyeji changamoto ya kuanza kutarjumi na kuhakiki tenzi za kale za Kiswahili ambazo kwa muda mrefu zilikuwa zimepuuzwa. Kazi hizi zimetufaa sana katika utafiti wetu kwa sababu tumekuwa tukizirejelea mara kwa mara kama mifano ambamo baadhi ya vipengele vya fani vimetumiwa. Ingawa utafiti wetu haukuhusu mojawapo ya tenzi hizi, zimetufaa kwa kiasi kidogo kwa sababu ya sifabia za tenzi zilizo nazo.

1.8 MBINU ZA UTAFITI

Tumefanya utafiti kwa kudurusu matini mbalimbali zilizokuwa za manufaa kwetu: vitabu, tasnifu na majarida yanayojadili fani. Tumepitia pia kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusiana na nadharia tutakayoitumia katika utafiti wetu. Ili kuboresha utafiti wetu imetubidi tusome yaliyoandikwa kwenye mtandao kuhusu fani na maendeleo ya nadharia ya umuundo. Mbali na kusoma tenzi tunazoshughulikia, tumerejelea kazi za wahakiki waliotutangulia na kutathmini jinsi walivyoshughulikia uhakiki wa tenzi mbalimbali kimaudhui na kifani. Katika kufanya hivyo, kazi zao zimetunufaisha pakubwa.

1.9 UCHANGANUZI WA DATA

Baada ya kusoma kwa makini tenzi tulizoshughulikia na kuzitathmini, tumeichanganua data (mifano mbalimbali katika tenzi) tuliyoikusanya. Uchanganuzi wetu utakuwa wa kielezi pasipo matumizi ya takwimu.

SURA YA PILI

MISINGI YA UHAKIKI WA KIFANI: UFAFANUZI WA DHANA

MBALIMBALI

2.0 UTANGULIZI

Kabla ya kuingilia uhakiki wa fani ni muhimu kufahamu vipengele vya fani ambavyo pia ni sehemu ya malighafi yanayojenga fasihi kiujumi. Katika sura hii tumefafanua dhana ya fani na kueleza kila kipengele kinachojenga. Ufafanuzi huu umetupa mwanga zaidi katika kuelewa muundo wa ndani na wa nje wa tenzi tulizoshughulikia. Tumetathmini muundo wa ndani kwa kueleza dhana za wahusika, mandhari, msuko, toni, wakati, usimulizi na matumizi ya lugha. Tumeshughulikia muundo wa nje kwa kufafanua umbo la tenzi. Tumeeleza mizani, mishororo, beti, vina na vipande. Isitoshe tumeangalia jinsi msanii alivyotumia uhuru alio nao wa utunzi katika kazi hizi kwa kufafanua tabdila, inkisari, mazida na kutazama jinsi sarufi ilivyobadilishwa.

2.1.0 DHANA YA FANI

Fani ni jumla ya vijengo vya kazi ya fasihi avitumiavyo mtunzi kuwasilisha ujumbe wake. Vijengo hivi vinajumlisha muundo wa ndani na wa nje wa kazi ya kifasihi. Utafiti wetu unahusu tenzi kwa hivyo tumechunguza muundo yote miwili ya tenzi tunazoshughulikia. Vipengele vya muundo wa ndani wa tenzi vinajumlisha: Wahusika, msuko, usimulizi, mandhari, wakati, toni na lugha. Muundo wa nje unahusu umbo la tenzi ambalo lina vijenzi vyake kama vile mizani, mishororo, beti, bahari, vipande na vina.

Swala la fani limezua hisia mbalimbali miongoni mwa wanazuoni wakiwemo wananadharia katika uhakiki wa kazi za kifasihi. Kuna wale wanaoipa fani kipaumbele na kusisitiza kuwa kazi za kifasihi zihakikiwe kwa misingi yake na kuna wengine wanaosisitiza kwamba uhakiki ufanywe kwa misingi ya kijamii.

Waasisi wa nadharia ya umuundo wanaamini kuwa lugha ya kishairi ni tofauti na lugha ya kawaida kwa namna inavyotumia mbinu mbalimbali mathalani wizani na mizani. Wao wanatilia mkazo uhakiki wa kunga zinazotumiwa kuwasilisha mawazo ya msanii kuliko mawazo yenyewe. Kwa hivyo, uhakiki wa kifani hupuuza maana ya matini ya kifasihi inayohakikiwa. Wana nadharia hii wanashikilia kwamba iwapo fani zitatumwa vyema zitaeleweka na hivyo kuzifanya tungo za kisanaa zifasiriwe kwa njia iliyokusudiwa na msanii. Wanayahusudu sana mambo halisi yanayoweza kusomwa katika tungo, kwamba ndiyo miongozo inayofanikisha matini kuwa kazi ya kisanaa

Dorsch (1965) anasema kuwa wanafilosofia wa Kirasimi kutoka Ugiriki, Aristotle na Plato walitofautiana kuhusu nafasi ya fasihi katika jamii. Plato aliangalia fasihi kwa misingi ya maadili katika jamii kinyume na Aristotle aliyesisitiza kuwa vipengele vinavyojenga shairi vijumlisha ploti, wahusika, lugha na matukio. Alijaribu kuutenga ushairi na jamii. Alipendekeza kuwa ushairi utofautishwe kutokana na kazi zingine za fasihi kwa fani yake, ikiwemo ploti, umbo, lugha ilivyotumiwa na wahusika.

Jitihada za Aristotle za kuutenga ushairi na jamii na kusisitiza uzingativu wa fani yake yumkini ndio ulioweka msingi wa uhakiki wa fani. Fani ndiyo inayohifadhi muundo wa mashairi na kuyatenga na kazi zingine za kifasihi kwa hivyo kuna umuhimu wa kuhifadhi

vijenzi vyake katika utunzi. Isitoshe, kama tutakavyodhirisha katika sura za tatu na nne, baadhi ya vipengele vya fani huiakisi jamii inamotungiwa kazi husika. Tunakubaliana na Plato pia kwa sababu mambo yanayozungumziwa katika ushairi huiakisi jamii. Wote hawakukosea, waliweka misingi ya uhakiki wa mashairi kimaudhui na kifani ambao wasomi wametumia kujenga mawazo zaidi kwa miaka mingi.

Massamba (1983) ameyanukuu mawazo ya watunzi wa mashairi ya Kiswahili wakiwemo Shaaban Robert, Abdilatif Abdalla, Abed Kaluta, Mnyampala na wengineo ambao wanaendeleza mawazo ya Aristotle. Wanasistiza kuwa katika ushairi, fani na maudhui ni vitu muhimu kabisa na kwamba kila kimoja kati ya vitu hivyo kina wajibu wake maalum. Baadhi yao wanaelekea kutia mkazo kwenye fani na wengine kwenye maudhui.

2.1.1 WAHUSIKA

Wamitila (2002) anasema kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni 'binadamu' wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda. Wahusika hutambulishwa kwa maelezo ya mhusika mwenzao au msimulizi. Wamitila anawainisha wahusika katika kategoria zifutazo: Wahusika akisi, bapa, bapa sugu, bapa kielelezo, batili, duara, ghibu, jumui, kipokeo, kani, mchomozi, msaidizi, foili, msimulizi, shinda, na wahusika wakuu.

Uainishaji wa wahusika katika vikundi vidogo alivyovigawa Wamitila (khj) unaweza kumkanganya mhakiki. Sifa za wahusika katika vikundi vingi tofauti alivyoainisha

zinaingiliana, hazina tofauti dhahiri. Kwa maoni yetu, ili kuzuia utata, ni bora kuwainisha wahusika katika vikundi vinne: Wahusika wakuu, wahusika bapa, duara na wahusika wajenzi, wasaidizi au wadogo.

Aristotle (1987) aliangazia kanuni nne ambazo ndizo misingi ya kuwachunguza na kuwatathmini wahusika. Alisema kuwa lazima mhusika aonyeshe hali ya juu ya kimaadili. Kanuni hii inatokana na mtazamo wa jadi wa fasihi. Fasihi ilitazamwa kwenye misingi yake ya kimaadili; kuwa inapaswa kuchangia katika ukuzaji wa maadili ya wasomaji.

Mtazamo wa Aristotle (khj) ni wa kiutopia au kinjozi kwa sababu wahusika hawaonyeshi kuathiriwa na mazingira yao. Zaynab Himid amewasawiri wahusika katika hali zao halisia. Wahusika wake ni wa kuaminika kwa sababu kazi yake inasimulia ukweli kamili kuhusu ada, mila, na mafunzo ya dini na dunia yanayoambatana na vipindi mbalimbali vya maisha ya mwanamke wa kizanzibari; kuanzia kuzaliwa kwake, utoto wake, avunjapo ungo na kuwa mwari, anapoposwa, kufungishwa ndoa na kuolewa, maisha ya ndoa na ulezi wa mimba.

Kanuni zingine alizoibua Aristotle ni kuwa lazima mhusika apewe sifa au vitambulishi vinavyohusiana vizuri na matendo yake, lazima awe na sifa zinazomtambulisha kama mhusika na awe kama binadamu na lazima awe na uthabiti unaotokeza waziwazi.

Kanuni hizi ni muhimu sana katika uhakiki wa wahusika. Mtunzi anaweza kumpa mhusika wasifu fulani wa kimaumbile, lugha ya kipekee, mazingira maalum, mtazamo na itikadi ambazo zinamtambulisha kama mhusika binafsi. Wahusika katika tenzi za Zaynab wanaakisi sifa na tabia za jamii ya kizanzibari wakati huo aliokuwa akitunga kazi zake. Isitoshe maelezo mengi kuhusu wahusika yametolewa na mtunzi mwenyewe.

Forster (1927) aliwagawa wahusika katika makundi mawili makuu; bapa na duara. Wahusika bapa husimamia wazo fulani, hawabadiliki tangu mwanzo hadi mwisho. Kuna aina mbili za aina hii ya wahusika; bapa sugu na bapa vielelezo. Bapa sugu ni wale ambao wanajulikana kutokana na maelezo ya msanii. Sifa zao au jinsi wanavyoelezwa na mwandishi ni ile ile katika utokeaji wao wote. Wahusika bapa-vielelezo hawabadiliki pia, na hupewa majina ambayo yanaafikiana na matendo yao na tabia zao. Majina ya wahusika hawa huwa kama kielekezi na kifupisho cha wasifu wao. Kwa mujibu wa Forster, hawa ni wahusika ambao wanakaribiana kwa kiasi kikubwa na binadamu wa kawaida. Uduara wa wahusika hawa umo kwenye mabadiliko yanayowajia. Yanaweza kuwa ya kisaikolojia, kijamii na kiukuaji. Katika uhakiki wetu tutajishughulisha na aina zote mbili za wahusika wa aina hii kwa sababu wamejitokeza katika tenzi za Zaynab.

Wasanii wengi wa kazi za kifasihi huwaumba wahusika bapa sugu alivyowataja Forster (khj) Wahusika wa aina hii hawawezi kamwe kupatikana katika ulimwengu halisia lakini hutokea katika kazi za kifasihi tu kwa lengo la kusisitiza ujumbe fulani. Aghalabu mwishoni mwa kazi matendo yao hutajwa tu kuwa yalibadilika bila msanii kuingia katika maelezo ya kina ya mabadiliko hayo. Mhusika duara ndiye mwakilishi halisia wa

binadamu wa kawaida ingawa wakati mwingine sifa anazopewa huenda zisiakisi binadamu wa kawaida. Tukirejelea tenzi zilizotungwa zamani kumsifia Mtume, tunatambua kuwa, ingawa alikuwa na sifa za mhusika duara, kuna mambo ya kiajabuajabu ambayo alikuwa anatenda ambayo yasingetendwa na binadamu wa kawaida.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa, wahusika ni sehemu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Msanii huwaweka wahusika wake katika mandhari yatakayomsaidia kuwasilisha hoja zake kutokana na vitendo, maingiliano na fikra zao. Wamewagawa wahusika katika vikundi kumi na viwili: Wahusika wakwezi, wa kisaikolojia, wa kimapinduzi, jumui, wakuu, wasaidizi, wajenzi, wa miraba minne, wa mraba mmoja, duara, bapa na wahusika shinda.

Migao mingi ya wahusika waliofanya Njogu na mwenziwe (khj) ina mwingiliano kwa sababu mhusika mmoja anaweza kuwa wa kimapinduzi, wa kisaikolojia na mhusika mkuu kwa wakati mmoja. Tunapendekeza kuwa kategoria za wahusika zisivunjwe zaidi kwa sababu zinaweza kuleta utatanishi katika uhakiki. Madai ya kuwa wahusika hubuniwa kutokana na mazingira ya msanii ni kweli kabisa lakini wasomi hawa wanafaa kukumbuka kuwa kuna wahusika wanaobuniwa kwa misingi ya itikadi na imani za dini (watu ambao hawakupata kuonekana, wanasikika tu katika hadithi). Je, katika hali kama hizo, tutasema kuwa wamebuniwa kutokana na mazingira ya msanii?

Mbatiah (2001) anasema kuwa wahusika ni watu tunaokutana nao katika kazi za kifasihi na ambao kutokana na matendo na mazungumzo yao wanatudokezea kuhusu ujumbe wa

kazi inayohusika. Wahusika ni vijenzi muhimu vya tanzu za drama, riwaya, novela na hadithi fupi. Katika fasihi simulizi na fasihi andishi isiyo ya kiuhalisia, wahusika wanaweza kuwa wanyama. Mbatiah amewagawa wahusika katika kategoria zifuatazo: bapa, duara, dufu, wahusika wasaidizi na wakuu.

Tunakubaliana na mawazo ya Mbatiah (khj) ingawa hatujaridhika na maelezo yake. Mbatiah anapuuza ukweli kuwa wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi wanaakisi watu katika ulimwengu wa kiuhalisia. Madai yake pia kuwa katika fasihi simulizi na fasihi andishi isiyo kiuhalisia, wahusika wanaweza kuwa wanyama yanaelekea kudokeza kuwa wahusika wanyama hawawezi kuakisi binadamu katika ulimwengu wa kiuhalisia. Hatukubaliani naye katika wazo hilo kwa sababu kuna baadhi ya kazi za kifasihi ambazo wahusika ni wanyama walio na sifa za kibinadamu: Kama vile riwaya ya George Orwell (1967) ya *Shamba La Wanyama*. Sifa ya wahusika wanyama ilitawala katika fasihi simulizi na sifa za wanyama hao ziliwakilisha binadamu wa kawaida. Sifa hii ilikuwa ikitokea pia katika fasihi andishi za zamani yumkini kabla ya maendeleo ya fasihi.

Mohammed (1995) asema kuwa mshairi huwa ni mtungaji shairi na mhusika wakati mmoja, ingawa mhusika huyu haonekani kusimama waziwazi juu ya kurasa za shairi, anajificha nyuma ya mwandishi. Wahusika ni viumbe vya mawazoni vinavyoumbwa na mwandishi na kuibuka katika kazi yake ya fasihi. Wahusika huhusika na matendo na matukio kadha katika kazi hiyo, hupatikana katika tamthilia, riwaya na hadithi fupi,

lakini wakati mwingine hata katika ushairi simulizi kama vile utenzi. Mohammed amewagawa wahusika wake katika vikundi vitatu: Wahusika mviringo, bapa na vinyago.

Madai ya Mohammed (khj) kuwa wahusika ni viumbe vya mawazoni vinavyoumbwa na mwandishi si kweli. Mwandishi huchota wahusika katika mazingira yake na jambo hili ndilo limeipa fasihi hadhi katika jamii. Mwandishi hawezi kuumba wahusika katika ombwe tupu kwa sababu azma yake ya kuandika huwa ni kuyamulika maovu na mema anayoyaona katika jamii. Sifa za wahusika wake huakisi sifa za watu katika jamii inayomzunguka.

Gill (1985) anasema kwamba wahusika ni viumbe waliobuniwa, si watu halisi katika maisha. Wasanii wanapobuni wahusika, huchagua sifa za watu wa kawaida, wanazijenga huku wakipuuzza zingine na kuziunga pamoja walizoteua wanavyopenda. Matokeo ya ufinyanzi huu ni viumbe wa kubuni tu walio na uhai katika kurasa za kazi kisanii bali si viumbe wa kawaida.

Gill (khj) anatofautisha aina mbili za wahusika: funge na wazi. Aliye wazi, hukua na kuendelea. Msanii humruhusu msomaji kuingia katika akili za wahusika wa namna hii na hivyo basi hueleweka. Msomaji huweza kufuatilia tajriba nyingi tofauti za mhusika aina hii wakati mwingine yakiwemo mauti. Wahusika funge hawabadiliki, na msanii hawaruhusu wasomaji kuingia akilini mwao. Uhakiki wa sampuli hii ya wahusika huwezekana tu kupitia yale ambayo wahusika wengine wanasema juu yao, maelezo ya mwandishi kuwahusu, wanaoshirikiana nao na tabaka lao katika jamii.

Wanazuoni mbalimbali wametoa fasiri tofauti za dhana ya wahusika na zote zinaelekea kubeba mawazo yanayowiana kwamba: wahusika ni viumbe vya kisanii vinavyoumbwa na wasanii wenyewe lakini vinavyoakisi sifa na tabia za watu fulani katika maisha ya uhalisia. Kazi ya kifasihi huwa na aina tofauti za wahusika wanaowakilisha watu mbalimbali wanaopatikana katika jumuiya anayoizungumzia na kazi ya kifasihi haiwezi kukamilika bila wahusika kwa sababu wahusika ndio wamojawapo wa vijenzi vya kazi hiyo.

2.1.2 MANDHARI

Mbatiah (2001) anasema kuwa istilahi hii inahusiana hasa na utanzu wa drama. Inarejelea sura mahsusi inayotokana na mapambo na vifaa vilivyopangwa kwenye jukwaa. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yaliyoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mazingira kama hayo yanaweza kuwa nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita. Istilahi ya mandhari pia hutumiwa kwa maana ya sura ya mahali, hasa ikiwa ya kuvutia.

Mawazo ya Mbatiah (khj) yana udhaifu kwa kuwa amefafanua dhana hii kwa muktadha wa tamthilia pekee. Ameeleza pia mandhari finyu ya kimazingira bila kueleza dhana hii kwa upana wake. Mandhari hupatikana katika kazi zote za kifasihi (ushairi, riwaya na hadithi fupi), ni kipengele cha fani kisichoweza kuepukika. Dhana hii ni pana kwa sababu inajumlisha mambo yote yanayohusu itikadi na mila za jamii inayozungumziwa kwa hivyo hatuwezi kupuuza maana zingine katika ufafanuzi wetu.

Wamitila (2002) anasema kuwa mandhari ni dhana inayorejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia. Yaani mazingira ya utendaji wake au usimulizi wake. Katika maana pana, dhana hii huelezea mazingira ya kijamii na kielimu wanakojikuta wahusika wa kifasihi. Aghalabu wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia.

Katika fasiri ya Wamitila (khj), anaonekana kusema kuwa mandhari hupatikana katika tamthilia, riwaya na hadithi fupi peke yake. Mawazo haya yanaonekana kumulikwa na baadhi ya wasomi. Wanaonekana kuwa na mawazo kuwa kipengele cha fani cha mandhari hakimo katika ushairi. Wana mawazo haya pengine kwa kuwa mandhari katika ushairi huvumbuliwa pamoja na matukio bila kutoa maelezo ya kina. Sababu nyingine ni kuwa huenda wasomi wengi wanahusisha mandhari na mazingira peke yake pasipo kuyahusisha na mila na itikadi za wanajamii. Katika ushairi wa tenzi, mandhari ambayo hutokea sana ni ya mambo yanayohusu utamaduni na imani za jamii husika.

Gill (1985) anasema kwamba mandhari ni neno pana linalojumlisha mahali ambapo wahusika wamewasilishwa, muktadha wa kijamii wa wahusika kama vile familia, marafiki, matabaka, tamaduni, imani na kaida za jamii kitabia. Gill anasema kuwa mandhari huchangia katika kueleza mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali waliyomo na hata husaidia katika kutambua maudhui yaliyo katika kazi ya kifasihi.

Kama alivyosema Gill, neno mandhari, ni pana. Msanii huchora mandhari mbalimbali kwa ujuzi wa kutumia maneno kitaswira. Mandhari huhamishwa kutoka mahali pamoja

hadi pengine; katika nyumba, mikahawani, vijijini, mashambani na kwingineko. Taswira ya mandhari inaonekana katika *Tenzi za Miiraji na Fatuma* (mandhari ya mbinguni), *Herekali*, *Siri Li Asirali* na *Vita vya Uhudi* (mandhari ya kivita), *Adamu na Hawaa* (mandhari ya paradiso). Tunakubaliana na Gill (khj) kuwa neno mandhari ni pana. Halimaanishi tu mandhari finyu ya kimazingira bali linajumlisha pia itikadi, mila na desturi za jamii husika katika ulimwengu halisia. Mandhari huakisi hali ya maisha ya jamii au watu halisia wanaoakilishwa na wahusika katika kazi ya kifasihi

Mandhari hutumiwa na wasanii kwa njia ya ukinzani au usambamba, mojawapo ya mbinu za wanaumuundo. Katika kazi ya kifasihi, msanii hutumia mandhari kinzani kuwasilisha ujumbe wake. Hutuchorea hali duni ya mhusika kwa kueleza kinagaubaga jinsi nyumba yake ilivyo na kueleza utajiri wa mwingine kwa kutupa picha ya nyumba yake pia. Mandhari ni kipengele muhimu sana katika kazi za kifasihi kwa sababu huchukua majukumu mbalimbali ya kuwa kama kielekezi, kihimili, kihisishi, kisitari, kitaashira, kidhibiti halihamasa (*mood*) kiishara, mandhari kama kipengele cha kiutanzu, kidhibiti cha wahusika na mandhari kama majaaliwa yaani maelezo ya msanii kuhusu mahali fulani katika kazi yake yanaweza kutupa mwelekeo maalum wa hadithi au kututolea mwangaza kuhusu matukio yanayojiri hivyo basi yakawa kama kielekezi cha hadithi yenyewe.

Mandhari kutumika kama sitari ya hali fulani inayomhusu mhusika au inayohusu tukio fulani. Yanaweza pia kutumika kama kihisishi ambapo huelezwa kwa namna inayoleta hisia fulani kwa msomaji, hisia imwelekezayo apende au achukie jambo na kitu fulani.

Mandhari huweza kudhihirika kwa namna mbili: hali ilivyo kijiografia (kimazingira) na kihistoria (kiwakati). Udhihirikaji huu huelekezwa katika uteuzi wa vipengele vingine vinavyojenga fani kama vile msamiati, wahusika, toni na vinginevyo.

Baada ya kupitia maoni ya waandishi mbalimbali kuhusu dhana ya mandhari, tumefikia kubaini kuwa mandhari ni wakati na mahali ambapo hadithi au mchezo wa kuigiza hufanyika.

Yanaweza kuwasilishwa punde tu kazi ya kifasihi inapoanza kupitia kwa maelezo ya kina au yakavumbuliwa kwa hatua baada ya nyingine kupitia maelezo na matukio. Huchangia sana katika kuibua athari za kihisia za hadithi na huchukua sehemu muhimu katika migogoro inayotokea katika kazi. Uamilifu wake mwingine muhimu ni kusaidia katika uhakiki wa sifa za wahusika. Mandhari hutuelekeza kuviamini vipengele vingine vilivyoteuliwa ambapo mbali na kutupa taswira ya hali husika, hisia zetu huguswa na aina ya toni inayosawiriwa kwayo.

2.1.3 TONI

Wamitila (2002) asema kwamba toni ni dhana inayotumiwa kuelezea mkabala alio nao msimulizi wa hadithi kwenye wahusika waliomo katika hadithi yake na yaliyomo pia, matukio na hali iliyopo. Aghalabu toni huhusiana na masafa ujumi katika fasihi.

Tunakubaliana na mawazo ya Wamitila (khj). Toni ni kama hitimisho la msanii la kazi yake. Ni katika toni ambamo tunapata dhamira ya msanii ya kutunga kazi yake. Kupitia kwa toni, tunafasiri yanayomchukiza, anayoyapenda na maoni yake kuhusu jamii adilifu.

Murray (1978) anasema kuwa, ushairi una aina saba ya wasemaji. Kati ya hawa wasemaji kuna angalau mmoja ambaye huwa na mtazamo fulani kuhusu anayemzungumzia au anachokizungumzia. Ni lazima pia ajione kuwa ana uhusiano fulani na anayemzungumzia. Toni ya matamshi yake itategemea uhusiano na mtazamo alionao na anayemzungumzia. Kwa hivyo, toni ni jinsi mzungumzaji wa kifasihi anavyoeleza mtazamo wake kuhusu msikilizaji na uhusiano wake naye.

Madai ya Murray (khj) yanafaa tu wakati ambao mashairi yanawasilishwa jukwaani. Msanii hukabiliana na wasikilizaji wake ana kwa ana, na kwa kuwa ana uhusiano nao, yeye huwa katika hali nzuri ya kutumia sauti na toni ya matamshi yake kuibua hisia mbalimbali kama vile za uchungu, masikitiko, furaha, mshangao na huzuni.

Richards (1964) asema kwamba, lugha katika ushairi ina majukumu kadha wa kadha. Anabainisha maana nne za uamilifu wa lugha kwa misingi kuwa matamshi ya binadamu yanaweza kuwa na mitazamo minne: Fasili ya dhana akilini (*sense*), hisia, toni na nia. Tukirejelea anavyosema kuhusu toni, anadai kuwa toni ni mtazamo fulani alionao msemaji kumhusu msikilizaji. Kwa hivyo, anateua na kuyapanga maneno yake kimakusudi kutegemea hadhira inayomsikiliza huku akitambua uhusiano wake nayo. Toni ya matamshi yake huakisi ufahamu wa uhusiano huo na hisia zake juu ya anaowazungumzia.

Mawazo ya Richards (khj) yanaelekea kukubaliana na yetu kuwa toni ya msanii huakisi mtazamo alio nao kuhusu msikilizaji wake. Ni jumla ya mambo anayoyafikiria kumhusu

msikilizaji wake. Kwa hivyo msanii huhitajika kufanya uteuzi wa maneno na kuyapanga kimakusudi ili afikie lengo la kugusa hisia za msikilizaji wake kwa vyovyote vile hata iwe kwa njia hasi au chanya.

Leech na Short (1981) wanasema kuwa toni ni mtazamo au msimamo unaochukuliwa na msanii kuhusu wasomaji wake na pia kuhusu ujumbe anaowasilisha. Wanasema kuwa mhakiki huweza kutambua toni kwa kulinganisha hali ya msomaji na ile ya msanii. Hali ya msomaji huwa kama kioo kinachoonyesha hali ya mwandishi. Leech wanadai kuwa masafa ndiyo kiini cha ulinganishi huu wa toni. Masafa haya yanaweza kuwa rasmi au yasiyo rasmi, ya mazungumzo ya kawaida na ya uhusiano wa karibu mno. Msanii anaweza kuchagua kuzungumza kwa masafa ya mbali na kumweka mbali msomaji au ya karibu kwa uteuzi wa maneno ambayo yanaonyesha uhusiano wa karibu. Kadri masafa yanavyokuwa mafupi, ndivyo toni hujitokeza wazi. Leech wanadai pia kuwa msanii ndiye hudhibiti mwitiko wa msomaji anapobadilisha mtindo na toni yake katika kazi ya kifasihi.

Mawazo ya Leech na mwenziwe (khj) yana ufafanuzi mpana wa dhana ya toni. Ni kweli kuwa licha ya mhakiki kuwa na uwezo wa kufasiri hali ya msomaji kupitia kwa toni ya msanii, ni rahisi kufasiri hali ya msanii pia kupitia kwa toni yake. Msomaji ana uwezo wa kuingia katika akili ya msanii na kutambua hali ya maisha yake, tabia na mienendo yake kupitia kwa toni ya kazi yake. Toni mara nyingi, kama wanavyodai Leech, yaweza kuwa ya masafa ya mbali au karibu kutegemea hisia za msanii kuhusu analoliandikwa. Aghalabu

wasanii wengi huchagua kuzungumza kwa masafa ya mbali kwa sababu ujumbe wao huilenga jamii pana.

Kwa hivyo toni ni mtazamo ambao mwandishi huchukua kumhusu msomaji, mhusika au anayezungumziwa. Toni hujitokeza kupitia kwa uteuzi wa msamiati na maelezo ya kina ya wahusika na mandhari. Toni ni mojawapo ya vipengele vya fani ambavyo hujenga kazi ya kifasihi na kuipa maana na inaweza kuwa ya majonzi, maaso, huruma, mabezo au masikitiko. Holman (1960) anatilia mkazo kwa kusema kuwa yaweza kutumiwa kuonyesha hali ya kazi yenyewe ya sanaa pamoja na mbinu mbalimbali zinazotumiwa kuunda hali hiyo. Katika hali kama hii, toni ni zao la mseto, na hata kubadilikabadilika kwa vitu kama vina, takriri na ishara.

2.1.4 WAKATI

Wamitila (2002) anasema kuwa ni dhana muhimu katika uhakiki wa kifasihi. Hutumiwa kuelezea kipindi au vipindi ambapo hali na matukio yanayosimuliwa na uwasilishaji wake hutokea. Huweza kutumiwa katika upana wa kurejelea kipindi cha kihistoria ambacho ni msingi mkuu wa kazi inayohusika.

Wamitila (2003) anasema kuwa kipengele cha wakati hutazamwa sambamba na kipengele cha usimulizi kwa sababu kutokana na kipengele hiki, tunapata simulizi au hadithi zilizosimuliwa katika wakati uliopita, uliopo na wakati ujao. Tungo nyingi husimuliwa katika wakati uliopo kihistoria. Dhana hii ya wakati uliopo kihistoria inazitambulisha kazi za kifasihi hasa zilinganishwapo na zisizo za kifasihi. Matumizi ya *sasa* huchangia kuifanya kazi ya kifasihi kuyafupisha masafa ya kiwakati kati ya matukio

yake na wasomaji wa kazi hiyo. Msimulizi anajiweka kwenye nafasi sawa kiwakati na matukio anayoyasimulia.

Tunakubaliana na Wamitila (khj) kuwa kipengele cha wakati ni muhimu sana katika uhakiki wa kifasihi. Ni kutokana na dhana ya wakati ambapo wahakiki huelewa vipengele vingine vya fani katika kazi, kama vile mandhari, lugha, toni na wahusika. Jambo hili linatokea kwa sababu kila kipindi cha kihistoria huwa na mambo yake tofauti na kingine. Si hayo tu, kipengele cha wakati humsaidia msomaji kuiweka kazi katika muktadha wa wakati wa utunzi wa kazi hiyo. Jambo hili huwaruhusu wasomaji kukadiria maendeleo ya jamii kupitia kazi hizo kwa sababu kila wakati huiakisi hali ya jamii wakati huo husika.

Mohammed (1995) anasema kwamba wakati ni kipengele muhimu sana kwa sababu unashikamana na mabadiliko ya nyakati mbalimbali kwa jinsi matukio mbalimbali yanavyobadilikabadilika nayo. Hadithi ya kazi yoyote hutokea baina ya ncha mbili za wakati; mwanzo na mwisho. Kwenye nafasi ya ncha mbili hizi kunaweza kuwepo muda unaohusishwa na dakika, saa, siku, miezi, miaka na hata karne. Simulizi ya hadithi kiwakati huweza kufuata mfuatilizio wa kufululiza kutokea mwanzo hadi mwisho huku matukio yakipangwa kwa mpango wa *la mwanzo lije mwanzo na la mwisho lije mwisho* au kwa njia ya *urudio*. Aghalabu huwepo mchanganyiko wa hizi njia mbili.

Madai ya Mohammed (khj) kuhusu kipengele cha wakati yanaweka wazi ukweli kuwa kuna uhusiano kati ya vipengele vya wakati na usimulizi. Ameangalia kipengele hiki

(wakati) kwa upana na ufinyu wake. Mawazo ya Mohammed yana misingi yake katika nadharia ya umuundo. Amekifungamanisha kipengele hiki na usimulizi, kwa hivyo anatazama wakati katika matini na jinsi unavyotokea katika viwango tofauti vikiwemo saa, siku, miezi na miaka. Tumeyatahmini mawazo ya Mohammed na kugundua kuwa yanafungamana pia na kipengele cha msuko haswa tunapozungumza kuhusu usahili na uchangamano wake.

Gill (1985) asema, ni kaida kuwa kipindi kirefu cha wakati kinaweza kuchukua muda wa masaa mawili au matatu kuwasilisha kazi ya kifasihi. Hii inamaanisha kuwa muundo wa kazi ya kifasihi huonyesha mpito wa wakati. Wakati katika kazi za kifasihi huelezwa na mwandishi, wahusika na kupitia mbinu rejeshi.

Gill (khj) amekitazama kipengele cha wakati kimatini (muda unaochukuliwa kuwasilisha kazi) na vile dhana hii hutokea katika kazi ya kifasihi. Mawazo ya Gill yamepuuza mambo mengi kuhusu kipengele cha wakati katika kazi za kifasihi. Tunakubaliana naye pia kuwa kipengele hiki huelezwa na wahusika pamoja na msanii. Maoni yetu ni kuwa kipengele hiki hutokea pia katika baadhi ya tamathali za usemi kama vile mbinu rejeshi, taswira na ubashiri.

Kazi ya kifasihi ina sifa ya ukiushi wa utaratibu wa kiwakati. Mwandishi huweza kufupisha wakati kwa kutumia mbinu ya udondoshi wa matukio au maelezo ambayo si muhimu na kuacha mapengo katika kazi yake. Matumizi ya mbinu rejeshi hurejesha

wakati nyuma na mbinu elekezi au kionambali hutumiwa kuangazia matukio ambayo hayajatokea na hivyo kurefusha wakati.

Kwa kuhitimisha, wakati ni kipindi fulani ambacho ndicho msingi wa kazi ya kisanaa inayohusika. Wakati unaweza kuwa mwanzo wa kipindi maalum katika historia, msimu au majira ya mwaka au hata enzi ya mamlaka fulani. Kipengele cha wakati hujitokeza katika kazi zote za kifasihi kwa njia mbili; wakati ambao hudhihirika katika kutokea kwa matukio ndani ya kazi na wakati ambao msanii huandika kazi yake yaani kipindi cha kihistoria ambamo kazi hiyo hubuniwa.

Mawazo ya wataalamu hawa kuhusu kipengele cha wakati yanaridhisha lakini itakuwa bora iwapo mhakiki atawajibika na kutazama swala hili kwa njia mbili tulizoeleza awali anapohakiki kazi ya kifasihi. Swala la wakati limepelekea wahakiki wachanga kuyatia kapuni maandishi ya nyakati zilizopita kwa kusema kuwa yamepitwa na wakati bila kuyaweka katika muktadha na mazingira ya nyakati hizo zilizopita ili uzuri na umuhimu wake utambuliwe na kila msomaji. Ni vizuri kuangalia hali ya mambo katika mazingira ya nyakati mbalimbali na kuyalinganisha na wakati tulio nao ili tuone kama tumepiga hatua ya maendeleo au tunarudi nyuma.

2.1.5 USIMULIZI

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Ametaja na kueleza usimulizi anuwai unaojitokeza katika kazi za kifasihi. Aina hizo za usimulizi ni: Usimulizi anuwai, usimulizi ngazi, usimulizi maizi, usimulizi penyezi,

usimulizi sawia, usimulizi tangulizi, usimulizi wa ki-itimamu, usimulizi wa ki-utendi, usimulizi wa ki-utomaji, usimulizi wa nafsi ya pili na usimulizi wa nafsi ya tatu.

Wamitila (khj) anasema kwamba katika kazi yoyote ya fasihi huwa mna kisa au hadithi fulani ambayo inasimuliwa na msimulizi. Msimulizi huyu huisimulia hadithi yake kwa mtindo fulani na kwa njia maalum. Usimulizi wa hadithi huingiliana na kuathiriwa na aina mbalimbali za mitazamo. Inawezekana msimulizi akawa na mawazo au njia ya kuyaangalia maswala fulani ambayo anataka msomaji wake ayaone au hata akubaliane nayo. Usimulizi huo unaopatikana katika kazi hiyo unaweza ukawa wa moja kwa moja na ambao unafululiza au kutiririka kwa njia iliyo rahisi kufuata na pia inawezekana usimulizi huo ukawa na mikatizo ya hapa na pale.

Mawazo ya Wamitila (khj) ni ya kweli kwa sababu, ili kuchunguza suala la usimulizi katika kazi ya kifasihi, vipengele viwili vyaweza kuangaliwa ili kulielezea: Mhusika na msimulizi. Kazi yoyote huwa na sauti inayoelezea au kuyasimulia matukio yanayotokea au yanayopatikana hadithini; sauti hiyo hutokana na msimulizi. Msimulizi anaweza kuwa mtu kando na mwandishi au msimulizi-mwandishi. Msimulizi-mwandishi anaweza kuchukua mtazamo unaoafikiana na mtazamo halisi wa mwandishi wa kazi inayohusika au akachukua mtazamo ambao unapingana na mtazamo au misimamo ya mwandishi huyo kama kiumbe halisi.

Wasimulizi katika kazi ya fasihi wanaweza kuwa washiriki katika matukio au wanaoshuhudia tu bila kushiriki. Aina hii ya usimulizi imetokea katika *Utenzi wa Ras l'*

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa hadithi. Kuna aina kadha za usimulizi: Usimulizi wa mwandishi mwenyewe na usimulizi wa mmoja wa wahusika. Katika usimulizi wa mwandishi mwenyewe, msanii hutumia nafsi ya tatu, humfuata mhusika wake unyonyo. Katika kufanya hivyo, mwandishi hapa ana uhuru mkubwa, anaweza kwenda popote atakapo na kuhisi kama wahusika wake. Ni mtawala wa hadithini. Msimulizi anapokuwa mmoja wa wahusika, msomaji humfuata mhusika-msimulizi, usimulizi unakuwa wa ana kwa ana.

Tunakubaliana na mawazo ya Njogu na Chimera (khj). Hata hivyo katika aina zote za usimulizi sauti ya msanii hudhihirika. Msanii ndiye huwa muumbaji wa wahusika wake kwa hivyo yeye mwenyewe huwa na uhuru wa kuchagua mhusika atakayesema nini na vipi kutegemea nafasi aliyompa katika kazi yake.

Gill (1985) anasema usimulizi ni jambo pana kwa sababu uhusiano kati ya matukio, mwandishi na msomaji hutofautiana pakubwa. Anadai kuwa mwandishi ana njia kadha wa kadha za kuwasilisha ujumbe wake. Anaweza kuandika katika nafsi ya mtu wa kwanza ambapo mwandishi huwa kama mhusika anayesimulia kisa. Mhusika huyu msimulizi huumbwa na mwandishi kusimulia kisa kwa misingi ya mtazamo wa mwandishi.

Gill (khj) anasema kuwa, usimulizi wa nafsi ya mtu wa kwanza humpa mwandishi nafasi ya kumwalika msomaji kumhukumu mhusika-msimulizi. Hufanya hivyo kwa kumfanya msimulizi aseme mambo ambayo anamtarajia msomaji kukubaliana nayo au kukosa

kukubaliana nayo au kwa kumfanya msimulizi kutambua makosa yake. Mwandishi anaweza akakubaliana na msimulizi huyu au akakosa kukubaliana naye. Usimulizi wa nafsi ya mtu wa kwanza humruhusu msomaji kuhisi uchungu na furaha za tajriba ya msimulizi, kumwelewa zaidi na kushuhudia ukuaji wake.

Wasimulizi wa nafsi ya tatu si wahusika katika kazi ya kifasihi. Anasema kwamba katika karne ya kumi na nane msimulizi alikuwa akijitangaza eti yeye ndiye msimulizi lakini nyakati hizi, msimulizi huyu haonekani, hajitangazi. Wasimulizi aina hii wana uwezo na nguvu (wanalinganishwa na Mungu) kwa sababu ndio wanaoelekeza matukio wanavyopenda. Katika usimulizi wa aina hii, mwandishi huchagua kuingia katika akili ya mhusika mmoja hususan yule mkuu na kujua fikra zake.

Vipengele vya toni na usimulizi vinafungamana kutegemea aina ya usimulizi ambao mwandishi amechagua kuutumia. Mhakiki huweza kufasiri toni ya mwandishi kupitia usimulizi. Mwandishi anayechagua kutoa msimamo wake kuhusu anayoandikia hukubali kuwa yeye ndiye mwandishi wa kazi, huwahukumu na kutoa maoni yake kuhusu wahusika na tabia zao; huwabeza, kuwadhihaki, kuwatania na hata kuwafokea. Wakati huo wote, huwa pia anawapa wasomaji wake nafasi ya kushiriki katika kisa na kuona anayoyaona katika kazi yake.

Wellek na Warren (1949) wanasema kuwa katika tenzi, mtunzi husimulia kisa kama msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafasi wahusika wake, kuzungumza moja kwa moja. Kuna waandishi ambao huchagua kusimulia kisa pasipo

mwelekeo wa mgogoro linapotokea. Baadaye, matatizo na fumbo la msuko hufumbuliwa na suluhisho kupatikana.

Peck na Coyle (1984) wanasema msuko ni sehemu kamili ya hadithi. Inajumlisha asili ya wahusika, uhusiano baina ya matukio na athari zake za kidrama. Wanadai kuwa kazi ya kifasihi inaweza kuwa na misuko zaidi ya mmoja inayotokea sambamba katika hadithi. Msuko mkuu humlenga mhusika mkuu na misuko midogo huvilenga vikundi vingine vya wahusika na matukio.

Hadithi huwa na zaidi ya msuko mmoja kama wanavyodai Peck na mwenziwe. Msuko mkuu hudhihirika kwa njia iliyo wazi katika kazi na kumruhusu msomaji kuufuata kwa mfululizo unaoeleweka kwa urahisi. Matukio katika misuko midogo huisukuma hadithi mbele na kuufafanua zaidi msuko mkuu. Misuko midogo huzuka hadithi inapochukua mkondo mpya kupitia mbinu rejeshi au mbinu ya kiona mbali. Wakati mwingine misuko hii huzuka kutokana na migogoro inayotokea baina ya wahusika.

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa msuko ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana. Msuko unaweza kuelezwa kama mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo vinavyozuana. Matukio husababishana na kuelekezana kwenye suluhisho fulani.

Mawazo ya Njogu na Chimera (khj) yanaelekea yana udhaifu kidogo kwa sababu yanapuuza ukweli kuwa hadithi inaweza kukosa kuwa na mtiririko kwa sababu ya swala

la uchangamani wa msuko. Hata hivyo hatuwezi kuwahukumu kwa ukali sana kwa sababu zipo hadithi ambazo mtiririko wake ni sahili. Pengine msanii hutunga kazi ya msuko sahili kwa nia ya kutaka kusisitiza ujumbe wake. Yaani pasiwe na lolote la kupoteza umakini wa msomaji katika kufuatilia kiini kikuu cha hadithi.

Wamitila (2003) anasema kwamba msuko ni dhana inayorejelea mpangilio wa matukio yanayopatikana katika hadithi na huhusisha matendo ya nguli na jinsi yanavyowaathiri wahusika wengine. Msuko hueleza jinsi matukio hayo yanavyofuatana kisababishi. Msuko unatofautiana na hadithi kwa kuwa unahusisha kujiuliza swali la kwa nini tukio fulani linafuatwa na jingine na kwa nini tukio fulani limelitangulia jingine. Msuko huzua taharuki, msisimko na mshangao. Msuko unaweza kuwa sahili au changamano. Wamitila (2002) ameorodhesha na kufafanua kaida zinazotumika kuuboresha msuko kama ukubalifu, mshtukizo, taharuki, usababishi na tokeo, matarajio au matumaini, mvuto, mgogoro na mantiki.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Fasiri ya Wamitila ya dhana ya msuko ni ya kina. Tunakubaliana na mawazo yake kwa sababu yanajumlisha ufafanuzi wote kuhusu msuko. Wamitila anatofautisha baina ya msuko na hadithi kama wataalamu wenzake waliomtangulia (Forster). Msuko, tofauti na hadithi ni mpana na huhusisha tamathali za usemi na visababishi vya matukio ilhali hadithi inahusisha usimulizi wa kimitiririko pasipo kuzingatia visababishi vya matukio.

Forster (1927) anafafanua msuko kwa kueleza tofauti baina yake na hadithi. Anasema kwamba hadithi ni usimulizi wa matukio lakini msisitizo uko kwenye kisababishi. Anatoa

mfano kudhihirisha tofauti hizi: Mfalme alifariki kisha malkia akafariki ni hadithi. Mfalme alifariki kisha malkia akafa kutokana na simanzi iliyomkumba kufuatia kifo cha mfalme, ni msuko. Msuko, licha ya kuhifadhi kipengele cha wakati, hueleza zaidi kuhusu sababu ya tukio. Kwa hivyo kimsingi, katika hadithi msuko huuliza sababu ya kutokea kwa tukio ilhali hadithi hutoa msururu wa matukio kiwakati pasipo kuzingatia visababishi vya matukio.

Tunakubaliana na mawazo ya Forster (khj) kwa kuwa yanaweka wazi mpaka baina ya hadithi na msuko. Msuko hutia msisitizo kwenye visababishi nayo hadithi hutia msisitizo katika mtiririko wa hadithi kiwakati.

Mohammed (1995) anasema msuko ni msukumo wa hadithi katika mpangilio fulani. Msukumo huu hujengwa na wahusika wanaotenda na kutendana na kuathiriana kusababisha matukio, mwendo na kasi ya kwenda kiwakati na pahala. Anatofautisha baina ya hadithi na msuko kwa kusema kuwa, hadithi ni simulizi tu, tokea ncha moja hadi nyingine. Kinachotokea baina ya ncha hizo mbili ni msuko. Msuko unaingiza visababishi na matokeo yake. Kwa hivyo katika kazi ya kifasihi, msuko huhusika na maswala ya vipi, kwa nini, wapi na lini.

Gill (1985) anayamulika madai ya Forster kuhusu msuko. Anatilia mkazo dai kuwa kuna tofauti baina ya msuko na hadithi. Msuko, anasema, hueleza visababu vya msururu wa matukio. Anafafanua msuko kwa misingi ya matukio yaliyopita, malengo ya wahusika

katika matendo yao, safari ya mhusika mkuu, uvumbuzi wa kimaisha wa wahusika wakuu, utendakazi wa jamii husika na mambo yaliyofichika.

Tofauti na wataalamu wenzake, Gill (khj) amehusisha msuko na wahusika, matendo ya wahusika wakuu na uvumbuzi wa maisha yao katika hadithi pamoja na utendakazi wa jamii husika. Analosema Gill ni kuwa wahusika katika hadithi ndio kijenzi kikuu cha msuko, jambo ambalo tunaliunga mkono. Maoni yetu hapa pia ni kuwa, licha ya wahusika, mandhari huchukua sehemu kubwa pia katika kujenga mhusika. Jambo hili hutokea katika kazi ya kifasihi msanii anapoumba wahusika walio na tofauti za mila, itikadi na mitazamo tofauti ya mambo kwa sababu ya asili na malezi yao. Tofauti hizi huzua migogoro na misuko katika hadithi wahusika wanapohusiana na kuingiliana kwa njia mbalimbali.

Ngara (1982) anasema kuwa uti wa mgongo wa kazi ya kifasihi ni msuko. Msuko hushikilia vipengele vingine vya kazi ya kifasihi na kuvipa muundo. Msuko kwa hivyo, ni msururu wa matukio yaliyopangwa kiwakati. Matukio haya yana uhusiano wa kusababishana na kutegemeana katika suluhu. Msuko huenda nyuma na mbele kupitia mbinu rejeshi huku mwandishi akimpitisha msomaji katika wakati uliopita, uliopo, na ujao akieleza visababu vya matukio.

Tunakubaliana na mawazo ya Ngara (khj) kuwa msuko ni kama mhimili wa muundo wa kazi ya kifasihi. Katika msuko, tunapata vipengele vya wakati, wahusika, mandhari, usimulizi na lugha. Amehusisha kipengele cha wakati na matukio katika hadithi. Kupitia

kipengele hiki visababishi vya matukio huelezwa na suluhu kupatikana. Mara nyingi hali za wahusika katika wakati uliopo, ziwe nzuri au mbaya huelezwa kiwakati kupitia mbinu rejeshi.

Maelezo ya dhana ya msuko yaliyotolewa na wataalamu tuliowataja wote yanatosheleza.

Kutokana nayo tumepata mambo muhimu yanayofafanua msuko kama:

- i) Mpangilio: Lazima mwandishi ateue na kuyapanga matukio yake kulingana na azma ya msuko.
- ii) Mfululizo wa vitendo: Vitendo huanzia mwanzo na kuendelea kwa uhusiano wa kimantiki. Matukio mbalimbali hukua, moja baada ya jingine yakifuatana kiusababishi, kuingiliana kwa nguvu zinazokinzana na kujenga msuko. Katika kazi zingine za kifasihi, msuko huwa changamani. Matukio ya mwanzo yanaweza kupelekwa mwisho na ya mwisho yakaletwa mwanzo. Msanii huweza pia kutamba huku na huku akiachilia msuko mkuu na kuunda mingine midogo akijaribu kueleza visababishi mbalimbali vya tukio lililo katika msuko mkuu.
- iii) Uhusiano wa vitendo ni tokeo la mwingiliano wa nguvu na nguvu nyingine. Yaani pasipo mgogoro au ukinzani msuko hautakuwepo. Ukinzani huu ndio unaofungamanisha tukio moja kwa tukio lingine. Ndio unaoamrisha uhusiano wa kiusababishi unaojenga mapambano na mapambano ya nguvu kwa nguvu. Wakati mwingine hufikia kilele katika tukio moja na kuzua taharuki.

2.1.7 UMBO

Wamitila (2002) anasema kuwa dhana hii hutumiwa kuelezea sifa za nje zinazoipa kazi ya kifasihi sura za kutambulikana. Huhusisha sifa kama sura, matendo, maonyesho, vina

na mizani. Vipengele vinavyojenga umbo la shairi ndivyo hilitofautisha na tanzu zinginezo za fasihi.

Mohammed (1995) anasema kwamba umbo ni matokeo ya kuunganisha vitu vya namna moja na vitu vya aina mbalimbali. Hatua ya kutafuta mkamatano katika utaratibu au mfumo fulani unaoshikamanisha hiki na kile kwa ubingwa wa ufundi fulani ni hatua tuitayo muundo. Kwa maneno mengine kazi za sanaa zina miundo na maumbo mbalimbali. Zinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Sanaa zinatofautiana kwa mambo mengi kama tutakavyoona usoni, lakini miundo na maumbo yamekuwa vigezo muhimu vya kutenganisha sanaa. Kati ya vigezo vinavyotenganisha ushairi na sanaa ya nathari ni jinsi fani hizi zinavyoundwa na kujitokeza katika maumbo tofauti.

Kwa mujibu wa mawazo ya Wamtila (2002) na Mohammed (1995), kazi ya kifasihi hutambuliwa kwa umbo lake. Mawazo yao ni ya kweli kabisa ingawa, katika kazi zote za kifasihi, mashairi ndiyo yaliyo na muundo unaodhihirika wazi zaidi ya kazi zingine za kifasihi. Kuna tofauti ndogo kati ya novella, riwaya na hadithi fupi. Tukiangalia tamthilia, tunagundua kuwa, aina ya ushairi wa ngonjera pia umechuku muundo huo. Hatupingi kuwa kila utanzu wa fasihi una muundo wake, lakini tunalojaribu kusisitiza ni kuwa muundo wa kazi za ushairi ni wa kipekee.

Peck na Coyle (1984) wanasema kwamba muundo wa matini ni jumla ya umbo na mtindo. Wakati mwingine, umbo huitwa muundo, ingawa neno hili ni pana kwa sababu linajumlisha fani na maudhui ya kazi ya kisanii. Kimsingi, ushairi una mitindo miwili;

Kahigi, P. Kija, A. Mazrui, K. Mutiso, K. wa Mberia, H. Muhanika, T. Mvungi na S.A. Mohammed. Hawa ni waasisi wa mashairi huru ya Kiswahili ambayo hayajifungi kwenye arudhi. Matumizi ya neno 'huru' yanaweza kumpotosha msomaji kuamini kuwa mashairi ya aina hii hayana sifa maalum zinazoyatambulisha au hayana kanuni zake. Mashairi haya hutegemea mbinu nyingine kama: Mpangilio wa sentensi, unyambuaji maneno, mpangilio wake na muundo wa vifungu vya mistari kuzua hisia nzito ya utungo wa kishairi.

Swala la kuhifadhi umbo asilia la mashairi lilitetewa na wanamapokeo. Mashairi mapokeo hutungwa kwa kuzingatia mpangilio maalum wa beti, idadi fulani ya silabi au mizani, ukamilifu na upatanifu wa vina na mizani, vipande na mishororo. Baadhi ya wanamapokeo wa ushairi wa Kiswahili ni Kaluta Amri Abedi, Mathias Mnyampala, Chiraghdin Shihabuddin, Shaaban Robert, Abdilatif Abdalla na wengineo.

Kuanza kwa mashairi huru kulizua mjadala mkubwa ambao kwa kiasi kikubwa ulijengwa kwenye mvutano wa umbo la shairi la Kiswahili. Wanamapokeo walidai kuwa shairi haliwezi kuitwa la Kiswahili kama halikufuata vina na mizani. Nao wanamapinduzi walisisitiza kuwa kuna sifa nyingine zinazoutambulisha na kuufanikisha ushairi zaidi ya vina na mizani.

Abedi (1954:1) akitetea swala la umbo katika utungaji wa mashairi anasema:

**'.....mengi mno katika mashairi yanayotungwa, yametungwa
bila ujuzi wa kuṭoṣha, nayo yanaelekea kupunguza thamani
ya mashairi ya Kiswahili mbele ya mashairi ya lugha nyinginezo.'**

Hivyo nimeonelea ni jambo muhimu zielezwe kanuni juu ya kutunga mashairi, Ili tuwarejeshe watungaji katika mipaka inayotakiwa.....

Neno moja tukumbuke katika utungaji, nalo ni hili, ya kuwa mawazo ya mtungaji yazue vina, sio vina kuzua mawazo.....mtungaji hodari anao uwezo wa kuzua vina vizuri, vinavyochukuzana na habari anayoieleza kwa urahisi.....'

Wellek na Warren (1949) wana mawazo kuwa nadharia ya tanzu ni utaratibu wa kuainisha tanzu, si kiwakati au kimahali bali kutilia maanani maumbo na miundo ya fasihi. Wanasema kuwa nadharia ya tanzu inahusu uainishaji wa miundo, maumbo na sifa za kifani za tungo za fasihi ambazo zinatofautisha utanzu mmoja na mwingine. Katika enzi ya kiurasimi, kaida za utunzi ziliwekewa viwango vya juu sana. Mielekeo kuhusu nadharia ya tanzu katika enzi za urasimi ilikuwa ya kutoa sheria. Tunaporejelea ushairi wa Kiswahili wa karne ya 18 na 19, mtindo wa kiurasimi wa utunzi wa mashairi ya Kiswahili ulizingatiwa na Muyaka na Kaluta Amri Abedi.

Fasihi ni pana na imegawika katika tanzu ambazo kila moja ina sifa zake za kifani na kimuundo. Sifa hizi ndizo huupa kila utanzu wa fasihi sura inayotambulishwa nao. Kisanaa, washairi wengi wa Kiswahili pamoja na wahakiki waliokanganyika wanafikiri kuwa umbo la ushairi wa Kiswahili ni la pekee duniani. Kwao, vina, mizani na muwala ni sifa za ushairi wa Kiswahili tu. Hawajui kuwa hizi ni sifa za jumla za ushairi. Kimsingi, umbo la shairi liliwekewa mipaka na wanamapokeo. Juhudi ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangia katika kuhifadhi umbo la mashairi katika enzi ambazo mawazo ya kigeni

yameathiri utunzi. Hata hivyo fasihi ni hai, kwa hivyo mitindo mipya haina budi kujaribiwa na falsafa mpya kuibuka kufuatana na mikondo mipya ya kihistoria, fikra na mahitaji ya binadamu.

Vipengele vinavyoungana pamoja kujenga umbo la shairi ni ubeti ambao ni kifungu cha maneno yanayojitosheleza kimaana au kukamilishwa kimaana na kifungu kinachofuatia. Mizani ni silabi au mapigo katika neno, vina ni silabi za mwisho katika kila kipande cha mshororo. Mishororo ni mistari ya maneno inayojumlika pamoja kuunda ubeti. Vipande ni migao katika mshororo ilhali kibwagizo ni mistari wa mwisho katika kila ubeti. Kibwagizo huwa kimalizio au kiini. Kinakuwa kimalizio kinapotumiwa kulifunga na kulikamilisha wazo moja katika kila ubeti. Kinakuwa ni kiini kinapotokea katika kila mwisho wa ubeti na kutaja kwa muhtasari jambo muhimu linalozungumziwa. Kwa mujibu wa wanamapokeo, hizo ndizo sheria za utunzi wa mashairi ambazo Abedi (1954) amezieleza katika diwani yake.

2.1.8.0 LUGHA

Dhana ya lugha ni pana mno na kwa kuwa ndicho chombo cha mawasiliano, kinatumika katika nyanja zote za maisha. Lugha si andishi na zungumzi tu, kuna lugha ya ishara pia. Lugha ni hai na kadri binadamu anavyozidi kupiga hatua kimaendeleo ndivyo inavyokua na kubadilika. Ukweli huu uliwapelekea wataalamu wengi wa lugha kuanza kutazama lugha kwa upana wake. Akatokea Ferdinand de Saussure ambaye ni mmoja kati ya wataalamu waliofanya mapinduzi katika mtalaa wa lugha. Alipendekeza kwamba lugha itazamwe kisinkronia na kidaikronia (tawi la isimu-kihistoria). Waasisi wa matawi mengine ya isimu walianza kuwa na mtazamo tofauti wa lugha. Kukaibuka matawi kadha

wa kadha ya kiisimu yaliyoanza kuchunguza lugha kisayansi yakiwemo: Saikolojia kiisimu, isimu-jamii, demografia ya kiisimu, jiografia ya kiisimu, falsafa ya lugha, anthropolojia ya kiisimu na mengineyo.

Uchunguzi wetu katika sehemu hii utatupelekea kuangalia kwa makini lugha ya kifasihi ilivyotumiwa na msanii katika tenzi tunazoshughulikia. Tutakuwa tunakumbuka kuwa, lugha ya kifasihi inaingiliana na matawi mbalimbali ya kiisimu kama vile: la kihistoria kwa sababu ya matumizi ya msamiati chakavu, isimu-jamii kwa sababu ya sajili anuai zinazojitokeza katika kazi yenyewe, anthropolojia ya kiisimu kwa sababu ya tamaduni tofauti za wahusika na wanajamii ambazo zinaakisiwa katika kazi za kifasihi na mengineyo. Hatutasahau kutaja kuwa lugha ya kifasihi na uhusiano wake na matawi mengine ya kiisimu ni swala linalohitaji utafiti zaidi. Muda hauturuhusu kuliingilia swala hili kwa kina, isitoshe liko nje ya mipaka na upeo wa uchunguzi wetu.

Ni muhimu kuangalia maana ya dhana ya lugha kwa mujibu wa fasiri zinazotolewa na wataalamu mbalimbali. Habwe na Karanja (2007) wamezinukuu fasiri tofauti za dhana ya lugha kama zilivyoielezwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo Todd na Cook.

**Todd (1987:5) ameeleza kuwa lugha ni mfumo wa
ishara ambazo kwazo watu wanawasiliana.**

Maelezo ya Todd yana udhaifu kwa sababu yamepuuza swala la sauti; ambalo ndilo kiini cha lugha kwa hivyo si ufafanuzi toshelezi.

**Cook (1969:6) anasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti
nasibu na ishara za kisarufi ambazo kwazo watu wa jamii**

fulani ya lugha huwasiliana na kupokezana utamaduni wao.

Maelezo ya Cook yana upungufu kwa sababu hajasema lolote kuhusu lugha ya ishara. Ama kwa kweli hakuna mtaalamu anayeweza kujidai kuwa ameleza kikamilifu dhana hii, mawazo yote yanayotolewa ni ya kuchangizana kwa kuziba mapengo yaliyoachwa na waliotangulia.

Kamusi ya Isimu na Lugha (1990:35):

Lugha ni mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana.

Kuna mambo matatu yanayodhihirika katika kijejezi hiki: lugha ni mfumo, hutumia ishara, na tatu, kuwa lugha ni ya mawasiliano. Katika fasiri hii, swala la ishara halijatokea. Kwa maoni yetu, fasiri ya dhana lugha ingefaa zaidi iwapo ingejumlisha maneno kama sauti, ishara, chombo na mawasiliano. Yaani lugha ni chombo cha mawasiliano kilicho na mfumo wa sauti zenye maana na mfumo wa ishara zenye maana zinazofanikisha mawasiliano.

Uchunguzi wetu utajikita katika kufasiri na kuitalii lugha ya kifasihi ilivyotumiwa katika tenzi tunazoshughulikia. Kwa hivyo tutaeleza fasiri tofauti za lugha ya kifasihi kwa mujibu wa wanafasihi mbalimbali. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), lugha ina nafasi kubwa sana katika fasihi kwa kuwa fasihi yenyewe ni sanaa ya lugha. Lugha ndiyo nyenzo inayotofautisha fasihi na sanaa nyingine kama uchoraji, ufinyanzi, udarizi na nyinginezo. Lugha ni nguzo kuu ya kazi za kifasihi na uchunguzi wowote wa kazi hizo hauna budi kuangalia suala la lugha. Kazi ya kifasihi huyawasilisha maudhui yake,

dhamira na maana yake kwa kuitegemea lugha. Baadhi ya wahakiki wa fasihi wanasisitiza kuwa fasihi huitumia lugha kwa namna maalum inayozua lugha ya kifasihi. Sifa hizi ni kama uchimuzi wa lugha ya kazi za kifasihi pamoja na miundo isiyokuwa ya kawaida, matumizi ya tamathali za usemi na nyinginezo.

Mawazo ya Wamitila (khj) ni mazuri lakini ameangalia tu usanii wa lugha ya kifasihi kwa kuilinganisha na kazi zingine za kisanaa zisizotumia lugha. Usanii wa matumizi ya lugha umetamba katika uandishi wa magazeti, insha na hata katika uandishi wa nyaraka. Lugha ya kifasihi husikika pia katika mazungumzo ya kawaida baina ya watu kila siku.

Peck na Coyle (1984) wanasema kuwa tunapozungumza kuhusu fasihi tunazungumza kuhusu lugha na jinsi inavyotumiwa. Matini za kifasihi hujengwa kwa maneno na sharti tutofautishe baina ya lugha ya kawaida na ya kifasihi. Lugha hutumiwa kihisivu kwa ustadi kuibua mwitiko wa kihisivu wa msomaji katika fasihi. Peck na mwenziye wanasema kuwa njia zalishi na mwafaka ya kuzungumza kuhusu lugha ni kumakinikia mtindo. Jambo hili linahusu kueleza utendakazi wa kazi ya kifasihi, kujadili maneno yaliyotumiwa na kwa nini yalitumiwa. Kila msanii hata hivyo huwa na mtindo wake wa uandishi unaojikita katika uteuzi wake wa maneno ambao hutegemea maudhui ya kazi yake.

Tunapotazama kwa kina katika fasiri ya Peck na mwenziye (khj) tunaona dosari katika maelezo hayo. Kwanza, hakuna matini isiyojengwa na maneno. Ingekuwa bora iwapo wangedokeza kuwa fasihi hutumia lugha hisivu ya mvuto iliyo na athari kwa msomaji na

kwamba uteuzi wa maneno unaotumiwa hubeba maana tata. Katika hali kama hiyo, matini hubeba fasili nyingi za maana. Peck na mwenziye wanaona mtindo kama kigezo cha kuhakiki matumizi ya lugha. Kuna ukweli katika madai yao kwa sababu uteuzi wa maneno ya msanii unaweza kueleza mengi kumhusu, zikiwemo: Tajriba na panda shuka zake katika maisha, hali ya kisaikolojia, mtazamo wake wa maisha na eneo analotoka. Ni muhimu kuzingatia mtindo katika kiwango cha msanii binafsi na kwa mtazamo wa kijumla pia.

Uchunguzi katika lugha ya kishairi hautaenda mbali hadi msomaji awe na ufahamu wa uhusiano uliopo baina ya lugha inayotumiwa katika ushairi na aina nyinginezo za lugha. Lugha ya ushairi ina vipengele vikuu kama anavyosema Leech (1969:5-6)

Lugha ya kishairi yaweza kukiuka au kuvunja kaida za lugha kwa njia nyingi zilizo wazi au fiche. Njia na kusudi la ukiushi huu ni jambo la kutazamwa. Msanii mbunifu na hususan mshairi ana uhuru maalum miongoni mwa watumiaji lugha wa kutumia malighafi yote ya mawasiliano ya lugha pasipo kuheshimu wala kuzingatia miktadha ya kihistoria au ya kijamii anamoishi. Hili lamaanisha kuwa mshairi aweza kutumia lugha chakavu au akakopa vipengele vya lugha visivyo vya kifasihi na kuvitumia. Lugha yote inayochukuliwa kuwa ni ya kifasihi kama vile sitiari, jazanda, chukũ na nyinginezo ina mizizi yake katika matumizi ya lugha ya kila siku na kuangaliwa kwa kurejelea matumizi hayo. (tafsiri yetu)

Leech ametofautiana na Peck na mwenziye katika fasiri yake. Anasema kuwa matumizi ya lugha ya kifasihi yanapatikana katika matumizi ya lugha ya kila siku, jambo ambalo ni la kweli kwa sababu kabla ya fashi andishi, fasihi simulizi ilikuwepo. Kwa hivyo ni katika lugha zungumzi ambamo lugha andishi hutoa msamiati hususan wa kifasihi. Tuchukue mfano wa misimu kama vile *shukisha kwa mataa, piga ngeta, acha kwa mataa, piga kambi* na mingineyo. Misimu hii ilianza kama utanzu wa fasihi simulizi na kukubalika pia katika kazi za fasihi andishi. Kwa hivyo Leech hajakosea kusema kuwa lugha ya kifasihi imo katika matumizi ya kila siku ya lugha.

Suala jingine nyeti alilolizungumzia Leech ni la ukiushi. Jambo ambalo hutofautisha pakubwa lugha ya kifasihi na lugha katika matini zisizo za kifasihi. Lugha kiushi katika ushairi hutokea katika viwango vya kifonetiki, kimofolojia na kisintaksia. Hali hii humpa msanii nafasi ya kueleza ujumbe kwa njia ya mkato iliyo na uzito wa kimawazo.

Tutakapokuwa tunayatathmini matumizi ya lugha katika hizi tenzi mbili tutaangalia jinsi msanii alivyotumia msamiati wa Kiarabu, lahaja tofauti na tamathali za usemi. Tutavijumlisha vipengele hivyo kama uhuru wa msanii kwa sababu, ni katika vipengele hivi ambamo ukiushi hutokea. Tumegundua kuwa Zaynab Himid ametumia msamiati sahili kuliko uliotumiwa kutunga *Tenzi za Hamziyya na Mwanamnga* na baadhi ya tenzi nyinginezo zilizotungwa kati ya karne ya kumi na nne na kumi na saba. Hali hii inaeleweka kwa sababu alitunga tenzi hizi miaka mingi baada ya usanifishaji wa Kiswahili. Msanii huyu alisomea pia katika mfumo wa elimu ya kimagharibi.

Mambo haya yote yaliathiri matumizi yake ya lugha katika tenzi. Kimsingi, amezitunga tenzi katika lahaja ya kiunguja ambayo iliteuliwa na wanakamati wa usanifishaji wa Kiswahili kama *Ki-standard* yaani Kiswahili sanifu. Tutaeleza maeneo yanayozungumzwa kila lahaja aliyotumia na katika sura za tatu na nne tutanukuu msamiati wa kilahaja kama ulivyotumiwa na msanii.

2.1.8.1.0 UHURU WA KISHAIRI

Washairi wana uhuru wa kutumia lugha kinyume na matarajio ya kawaida. Wana uhuru wa kukiuka kaida fulani zinazohusiana na msamiati, na hata matarajio ya lugha ya kimaandishi na kiusemaji. Matumizi ya msamiati wa Kiarabu na lahaja katika utunzi yanaonyesha uhuru alio nao mshairi katika kutumia lugha.

2.1.8.1.1 MSAMIATI WA KILAHAJA

Baada ya usanifishaji wa Kiswahili, msamiati kutoka lahaja mbalimbali ulisalia tu katika utunzi wa kazi za kifasihi, hususan ushairi na mazungumzo ya kawaida.

2.1.8.1.2 KINGOZI

Wataalamu wa kuchunguza shajara za makabila ya kale wanasema kuwa asili ya lugha ya Kingozi inatokana na watu walioishi katika mji wa zamani sana uliokuwa ukiitwa ‘Ngozi’. Kabila la watu hao liliitwa ‘Wangozi.’ Kingozi kinaaminika kuwa lugha ya kikale ambayo ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili na inasemekana kuwa ni lugha nzee kuliko Kikae. Ilikuwa lugha ya kibantu halisi ambayo haikuwa na mchanganyiko wa maneno mengi ya lugha za kigeni. Hivi leo, lugha hii haitumiki tena katika maandishi ya kawaida. Imesalia tu katika utungaji wa mashairi kama zilivyo lahaja zingine. Kingozi kinaweza kuchukuliwa kama lugha rasimi ya Kiswahili.

2.1.8.1.3 MSAMIATI WA KIARABU

Kiarabu ndicho chenye maneno mengi katika Kiswahili kuliko lugha ya taifa lolote jingine la kigeni. Sababu kuu ni mbili: Kwanza, kwa kuwa Uarabu ndiyo nchi ya kigeni iliyokuwa jirani zaidi na upwa wa Afrika Mashariki. Watu wake waliingiliana zaidi na watu wa Pwani kuliko watu wengine wowote. Maingiliano yao yalikuwa ya kibiashara na kidini na msamiati mwingi wa Kiarabu ukapenya katika lugha za wenyeji. Baadhi ya maneno katika tenzi ni ya msamiati wa Kiarabu uliotoholewa na maneno ya Kiswahili yaliyo na athari za lugha ya Kiarabu. Harusi za Waswahili zilifungamana na utamaduni wa kiislamu na Kiarabu. Kwa hivyo mshairi hakuwa na budi kuutumia na kuathirika na msamiati huo katika matumizi yake ya lugha.

2.1.8.1.4 MSAMIATI WA KIINGEREZA

Mtunzi ametohoa msamiati wa Kiingereza katika kazi ambayo kimsingi imetungwa katika lugha ya Kiswahili. Hali hii inaeleweka kwa sababu mtunzi alisomea katika mfumo wa masomo ya kimagharibi na hata kuishi wakati Wazungu walitawala mataifa ya nchi za Afrika Mashariki.

Uhuru wa mtunzi humwezesha kuchota msamiati kutoka lugha chakavu na lahaja anuai ili aweze kuwasilisha ujumbe wake kwa mkato na uzito unaovuta nathari. Ushairi unasaidia kuhifadhi msamiati ambao ungekuwa umepotea na kusahaulika. Lahaja na kikale zina msamiati unaobeba maana pana ya kina. Yumkini hili laeleza sababu za kupendwa msamiati huo katika utunzi wa mashairi hususan ikikumbukwa kuwa matumizi ya msamiati huu pamoja na mbinu zingine za utunzi zinasaidia kuhifadhi umbo la mashairi ya kimapokeo.

2.1.8.2 MBINU ZA UTUNZI

Kama tulivyotaja awali mtunzi ametumia uhuru wa kishairi katika viwango mbalimbali (rejelea 2.1.8.1). Licha ya kiwango ambacho tumeeleza, kuna mbinu zinazotokea katika viwango vya sintaksi, mofolojia na fonetiki.

2.1.8.2.1 MPINDUO SARUFI

Katika kiwango cha sintaksi, msanii ametumia mbinu ya mpinduo au kugeuza sarufi. Katika sehemu nyingi anageuza mpangilio wa maneno katika mishororo yumkini kwa nia ya kutimiza urari wa mizani. Huu ni ukiushi wa kisintaksia ambao mshairi tu ndiye aliye na uhuru wa kuutumia.

2.1.8.2.2 TABDILA

Huu ni ukiushi wa kifonetiki ambapo mshairi hubadilisha sauti ya kina kwa madhumuni ya kupata urari.

2.1.8.2.3 MAZIDA

Mazida ni mbinu ya kurefusha maneno kwa nia ya kuongeza silabi ili kutosheleza mizani au kufikia kina fulani kinachohitajika. Kiisimu, huu ni ukiushi wa kimofolojia.

2.1.8.2.4 INKISARI

Ukiushi mwingine unaotokea katika kiwango cha kimofolojia ni wa kiinkisari. Hii ni aina ya ukiushi ambapo maneno hufupishwa kwa kudondosha silabi ili kutosheleza mizani au kupata kina maalum.

2.1.8.3 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi zina maana kiushi katika viwango vya kisemantiki na hata kisintaksia ambazo huziwezesha kupanua maana ya ujumbe unaowasilishwa. Mbinu hii huleta maana mpya ya neno au msisitizo na humwezesha mtunzi kutunga atungayo kwa njia inayoacha athari kwenye sikio la msomaji au hadhira. Mtunzi ametumia tamathali zinazotofautiana na kuingiliana pia. Tungependa kutaja hapa kuwa baadhi ya tamathali za usemi zina tofauti ndogo sana. Aghalabu sitiari, jazanda na jazanda hukaribiana sana kisemantiki. Zingine ni msisitizo bayana na takriri. Wataalamu wengi wamevuruga ufafanuzi wa tamathali za usemi na kila mmoja kuzuka na tafsiri inayofaa mahitaji yake. Ipo haja ya kuyaweka wazi mambo haya. Baadhi ya tamathali za usemi alizotumia mtunzi ni:

2.1.8.3.1 TASHBIHI

Tashbihi ni mbinu ya uhusisho na ulinganishi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa kutumia viunganishi vilinganishi kama: Ja, mithili ya, mfano wa, sawa na, kama na vinginevyo. Kufanana huku ni kwa ushabihiano wa hali ya utendaji au maumbile kama vile, sura. Wasanii hutumia mbinu hii kuchora taswira ya kitu au mtu kwa njia ya ulinganisho ambao unaeleweka, upesi na hadhira lengwa.

2.1.8.3.2 SITIARI

Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo kwayo kitu, matendo ya kitu au vitu vyenye tabia inayofanana hulinganishwa. Katika mbinu ya sitiari, mtunzi hulinganisha kitu kimoja na kingine kwa njia ya moja kwa moja pasipo kutumia vilinganishi vya tashbihi. Tamathali

hii hueleza sifa ya kitu fulani kwa kusema kwamba kitu hicho ni kitu kingine. Aghalabu kitenzi **NI** hutumiwa sana katika sitiari:

2.1.8.3.3 JAZANDA

Jazanda ni mbinu ya uwasilishaji wa maneno kwa mafumbo. Ujumbe anaouwasilisha msanii hauji kwa njia ya moja kwa moja. Kwa hivyo wahakiki huwa na uhuru wa kutoa fasiri zao mbalimbali mradi wana ushahidi wa kutosha kutoka katika matini yote kwa jumla. Wasanii hutumia mbinu hii aghalabu kwa minajili ya kuficha ukweli unaomiza katika ujumbe unaowasilishwa au wakati mwingine huchukua nafasi ya tasfida.

2.1.8.3.4 METHALI

Methali ni vifungu vya maneno yenye mafumbo ya hekima yanayopigiwa mtu kwa kusudi la kuonya, kubeza, kushauri na kufunza. Methali huakisi itikadi na imani za jamii zinazozitumia. Kila jamii huwa na methali zinazofungamana na mazingira yake. Methali nyingi za jamii zinzoishi katika mazingira ya bahari huwa na msamiati unaorejelea viumbe, mimea na vyombo vya baharini na maji. Methali za jamii zinazoishi makondeni huwa na msamiati unaorejelea mimea, mchanga na vifaa vya ukulima.

2.1.8.3.5 CHUKU

Chuku ni aina ya tamathali ya usemi inayotumia maneno yanayotia chumvi katika kauli fulani aghalabu kwa madhumuni ya kuchekesha au kuisisitiza. Mbinu hii inapotumiwa, huikuza sifa ya kitu au mtu kuliko hali yake ya kawaida kwa lengo la kuisisitiza sifa hiyo. Mbinu hii katika kazi ya kifasihi huwa na athari za kimguso kwa msomaji na huzuia uchovu wa akili inaposababisha kicheko.

2.1.8.3.6 MASWALI YA BALAGHA

Maswali ya balāgha ni maswali ambayo mtunzi au mhusika wake anayatumia kwa lengo la kumtanabahisha msomaji lakini hayahitaji majibu kwa sababu majibu hayo yanafahamika. Maswali ya balagha hutumiwa na watunzi kuwabeza baadhi ya wahusika, kutilia mkazo ujumbe na kuamsha nathari ya msomaji ili kumfanya atafakari zaidi juu ya kinachozungumziwa.

2.1.8.3.7 TASFIDA

Tasfida ni sifa inayotumiwa katika kazi ya kifasihi ili kufichia hali fulani ambayo inahisika kuwa itakuwa na athari fulani isiyokuwa nzuri kwa wasomaji au hadhira. Mbinu hii hutumiwa na wasanii wengi katika jaribio la kutaja mambo yasiyokubalika kwa njia inayokubalika. ‘Husafisha’ lugha ili kuepuka taathira yenye kuhujumu uso kwa upande wa hadhira.

2.1.8.3.8 KEJELI

Kejeli ni hali ambapo kuna kinyume fulani katika usemi, hali au tukio. Istilahi hii pia inaweza kuelezwa kama matamshi yanayolengwa mtu ili kumtweza bila yeye kujua. Katika kazi ya fasihi kejeli inayofanyiwa mhusika mmoja na mwingine hujulikana tu na mhusika anayekejeli pamojana msomaji au mtazamaji. Katika ushairi mtunzi husema jambo akilenga maana ya ndani na hivyo kumtarajia msomaji mpekuzi kuelewa maana fiche anayokusudia kuwasilisha.

2.1.8.3.9 TABAINI

Tabaini ni mbinu ya kulisisitiza jambo kwa kutumia maneno yanayoelekea kutoonyesha msisitizo huo waziwazi. Aghalabu mbinu hii ya kiusemi hutambulishwa na kuwepo kwa

kiungo **SI**. Wasanii hutumia mbinu hii kueleza kwa msisitizo sifa za mhusika au kitu fulani katika kazi zao.

2.1.8.3.10 SADFA

Sadfa ni dhana inayotumiwa katika fasihi kueleza utukiaji wa matukio kwa wakati mmoja na aghalabu kwa namna inayoshangaza au inayoashiria bahati.

2.1.8.3.11 MISEMO

Misemo ni mafumbo yaliyojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida yaliyositiri maana ya ndani. Kila utamaduni hutunga semi zinazofungamana na itikadi, utamaduni na mazingira yake. Kwa hivyo wanajamii husika huzielewa kwa uzito unaostahiki kwani hubeba mafunzo kwa jamii.

2.1.8.3.12 VISAWA

Visawe ni mbinu ambayo hufanya kazi ya kutilia mkazo wazo, dhana au maana fulani ya ujumla kwa kuibainishia maneno yenye maana ndogondogo za karibu. Kisemantiki tutasema kuwa maneno hayo yako katika kikoja kimoja cha maana. Hii ni mbinu muhimu katika uandishi wowote ule haswa kazi ya kifasihi kwa sababu urudiajirudiaji wa neno moja huchosha akili. Kule kutumia maneno tofauti kwa kurejelea maana ileile ndiko ujumi wa kazi za kifashi haswa.

2.1.8.3.13 TANAKALI SAUTI

Tanakali sauti hutumiwa kurejelea sauti ambayo inaigiza jinsi kitu fulani kiangukavyo, kiliavyo, kiliavyo na hata kitembeavyo. Kunga hii hutumiwa sana na washairi ili kutoa picha ya kile kinachowakilishwa na sauti hiyo.

2.1.8.3.14 NIDAA

Nidaa ni mbinu ya matumizi ya alama ya mshangao ambayo huonyesha mshangao au msisitizo wa jambo linalosemwa. Wasanii hutumia mbinu hii kuonyesha hisia za wahusika; zinaweza kuwa za furaha, uchungu, mshangao au masikitiko.

2.1.8.3.15 USAMBAMBA

Usambamba ni mbinu pana ya sanaa. Msanii huyarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti. Kimsingi hii ni mbinu ya kurudia. Urudiaji huu unaweza kujitokeza katika viwango tofauti kama vya vipashio vya kisintaksia, virai, vishazi au sentensi. Kuna aina mbalimbali za usambamba. Aina aliyotumia sana mtunzi (Bi. Zaynab) katika kazi zake ni usambamba wa aina ya ukinzani au uwili ambapo mambo mawili yaliyo kinyume hulinganishwa kwa kutumia maneno yanayokinzana kimaana. Mbinu hii inapotumiwa hususan katika ushairi, huiweka wazi toni ya mtunzi. Hii ndiyo mbinu anayoitumia kuyapa uzito na unyeti unaostahiki anayoyazungumzia.

2.1.8.3.16 TAKRIRI

Kama istilahi yenyewe inavyodokeza, takriri ni mbinu ya kukariri herufi fulani, neno au maneno fulani. Kwa hivyo kuna takriri sauti na takriri neno. Konsonanti, irabu na hata kina chaweza kurudiwarudiwa. Vilevile neno au kifungu cha maneno. Panapotokea takriri neno, inaweza kuwa kwa sababu ya kusiondika jambo na wakati mwingine kuchezea maneno tu.

2.1.8.3.17 TAASHIRA / ISHARA

Taashira ni neno, kitu au tukio linaloficha maana au hisia mahsusi katika kazi ya kifasihi. Mbinu hii inatumia kuelezea kitu katika kazi ya kifasihi ambacho huwakilisha kingine.

Kuwakilisha huku kunaweza kutokana na uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kuibua fikira fulani katika akili ya msomaji.

2.1.8.3.18 UTOHOZI

Utohozi una maana ya kuchukua neno fulani kutoka lugha moja na kulipa matamshi na mwendelezo wa lugha pokezi. Wasanii huitumia mbinu hii ili wasipoteze maana ya ujumbe uliodhamiriwa au kwa kukosa neno katika lugha wanayoitumia kutunga kazi yao.

2.1.8.3.19 MBINU REJESHI

Hii ni mbinu anayoitumia mtunzi kuyaeleza matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi. Mtunzi humtumia mmojawapo wa wahusika kukumbuka na kuyasimulia yaliyopita au yeye mwenyewe akasimulia yaliyopita. Mbinu hii hutumiwa kuziba pengo la habari za mhusika au matukio yasiyo dhahiri au kueleza sababu za hali walizomo wahusika katika kazi.

2.1.8.3.20 KINAYA

Kinaya ni tamathali ya usemi ambayo kwayo maana halisi husemwa kwa maneno yanayobeba maana kinyume. Maana ya juu katika usemi siyo huwa imekusudiwa. Huwa kuna maana nyingine fiche ambayo huwa na makali. Kwa hivyo huwa haiwezi kuwasilishwa kwa njia ya moja kwa moja.

2.1.8.3.21 TAABINI

Tabaini ni utungo wenye kumsifu mtu aliyekufa.

2.1.8.3.22 UBASHIRI / UTABIRI

Ubashiri ni mbinu anayotumia mtunzi kutaja au hata⁴kuwaza jambo litakalotokea kupitia kwa mhusika na hatimaye likatokea. Wasanii hutumia mbinu hii katika kazi zao kuonyesha hali za kisaikolojia za wahusika ambazo huakisiwa sana katika ndoto na matarajio waliyo juu ya hali zinazowakabili.

2.1.8.3.23 TASWIRA

Dhana ya taswira hutumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo (yaani maelezo fulani yakaunda picha) au za kiishara (zinazounda picha ambayo inaashiria jambo fulani au imeficha ujumbe mwingine). Taswira huweza kuundwa kwa matumizi ya tamathali za usemi hasa tashbihi na sitiari. Ingawa kimsingi, taswira nyingi ni taswira za uoni (yaani zinamchochea msomaji kuona picha fulani).

2.1.8.3.24 NYIMBO / NGOMEZI

Nyimbo ni kiperi cha fasihi simulizi cha utanzu wa ushairi. Ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kimuziki. Nyimbo hufungamanishwa na shughuli nyingi sana haswa za kitamaduni kwa madhumuni ya kufunza na kuhifadhi matukio katika shughuli hizo kupitia kwa nyimbo. Wanajamii hupewa nafasi ya kuhusika katika tajriba zisizosahaulika upesi kwa sababu ya athari zinazowachwa na nyimbo zinazoimbwa wakati wa shughuli hizo. Ngoma/ngomezi ni mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ambazo zilikuwa zikitumiwa wakati wa sherehe mbalimbali kwa makusudi tofautitofauti. Ngomezi ilitumiwa kama njia moja ya kuwasilisha ujumbe: Kama vile wa kifo, kuzaliwa kwa mtoto, kutangaza vita, ushindi fulani na ujumbe mwingineo. Kila mpigo wa ngoma

ulibeba ujumbe maalum uliojulikana tu na jamii husika. Katika tenzi tunazohakiki, kila ngoma katika arusi za Kiswahili ilikuwa na sababu maalum ya kucheza.

2.1.8.3.25 TASHIHISI / UHUIHAJI

Neno tashihisi lina asili yake katika lugha ya Kiarabu na maana yake ni kunafsisha au kufanya kitu kiwe na maumbile au tabia ya nafsi ya mwanadamu. Mbinu hii hutumiwa kuvipa vitu visivyo na uhai sifa na hisia za kibinadamu.

2.1.8.3.26 TAHARUKI

Taharuki ni hali ya matarajio anayokuwa nayo msomaji kutaka kujua yatakayotokea katika hadithi fulani. Taharuki hutokea sana pale ambapo msomaji ana hamu kubwa au anajua yanayoweza kutokea lakini hajui jinsi yatakavyotokea. Msanii hutumia mbinu hii ili kukitilia maanani kipengele anachotaka msomaji azingatie katika kazi yake. Athari yake kwa msomaji ni kumtia mshawasha wa kutaka kusoma zaidi.

2.1.8.3.27 VISAASILI

Visaasili ni mojawapo ya vitanzu vya fasihi simulizi kama zilivyo nyimbo. Ni hadithi ambazo hazihusishwi na mwandishi maalum bali hupatikana katika imani zilizopo katika jamii fulani. Aghalabu visaasili huhusisha matukio ya kiajabu au yasiyotarajiwa katika maisha ya kawaida au hata ya miungu. Huweza kuhusisha pia wahusika wa kishujaa wa kihistoria au wa kuaminika ambao wanatenda matendo yanayokiuka uhalisi wa kawaida. Visaasili huakisi muundo wa kitamaduni wa jamii inayohusika. Visaasili hutumiwa na wasanii ili kuupa nguvu ujumbe wao kwa kuufungamanisha na imani za jamii ambayo ujumbe umekusudiwa. Matumizi ya visaasili pia yanaonyesha umahiri wa msanii katika utunzi kwa kuweza kujenga daraja kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

2.1.8.4 HITIMISHO

Katika sura hii tumeshughulikia masuala muhimu ya kifasihi. Tumefafanua kwa kina baadhi ya vijenzi vya fani katika kazi ya kifasihi na haswa tenzi, ambavyo vinazitofautisha na kazi zingine za kifasihi. Tumewanukuu baadhi ya wasomi na maoni yao kuhusu vijenzi hivyo vya fani na kutoa maoni yetu pia kuvihusu. Ni matumaini yetu kwamba maoni yao na yetu yametoa msingi mwafaka katika uelewa wa tenzi ambazo tumeshughulikia katika sura zinazofuata.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

SURA YA TATU

UHAKIKI WA FANI KATIKA UTENZI WA HOWANI MWANA HOWANI

3.0 UTANGULIZI

Katika sura hii, tutahakiki utenzi wa Howani Mwana Howani. Tutachunguza jinsi mtunzi alivyojenga kazi yake kwa kutumia vijenzi vyote vya fani tulivyovieleza kwa kina katika sura ya pili. Hatutapoteza wakati kwa kuvieleza tena vijenzi hivyo vya fani, tutaenda moja kwa moja katika tenzi na kuonyesha fani hizi zinavyodhihirika katika utenzi.

3.1 UMBO

- 1) Tofauti na tenzi nyingi za Kiswahili, mtunzi ameuanza utenzi huu kwa kumhutubia mwanawe moja kwa moja bila kutumia fomula ya kawaida ya utangulizi katika utenzi wa tenzi ambapo watunzi huanza kwa shukurani kwa Maulana na kisha kuomba wino, kalamu na karatasi ya kuandikia. Baadaye, huwa wanamsifia Mwenyezi Mungu kwa maajabu ya viumbe vyake, kutoa dua na heshima zao kwa Mtume Mohammed na jamii yake, wafuasi wake na jamii ya waislamu kwa jumla. Kwa sababu za kudhihirisha jambo hili, tutatoa mifano katika beti za kwanza za *Tenzi za Fatuma, Siri Li Asirali* na *Howani Mwana Howani* kwa sababu za kiulinganishi tu na kuonyesha kuwa mtunzi wa *Utenzi wa Howani Mwana Howani* alikiuka hayo mazoea katika utenzi wa tenzi.

Utenzi wa Siri Li Asirali:

Akhi phani kwa upesi, ilo ali karatasi

Na wino mwema mweusi, utulizao maozi (ub.1).

Na kalamu mahabubu, ilo njema ya Arabu
Nowe ina la Wahabu, Mola wethu Muawazi (ub.2).

Nowe ina la Wadudi, Bismillahi, nibutadi!
Ndiye pweke wa Abadi, Mfalume Mwenye Ezi (ub.3).

Utenzi wa Fatuma:

Akhi nipha karatasi, njema isiyo kiasi
Na kalamu ya unyasi, na wino wa kuandikia (ub.1)

Wino lete wa hiburi, wenye nuru akhiyari
Pamoya na zenjefuri, kundufu iso misaa! (ub.2).

Nimsifu Maulaya, mwenye kuumbwa Nabia
Saidi l-Arabia! Akampa na shufaa (ub.7).

Utenzi wa Howani Mwana Howani:

Mwanangu nakueleza
Maneno haya sikiza
Kwa utuo pulikiza
Uyatie akilini (ub. 1).

Sasa mama umekua
Msichana watambua
Mazuri kupambanua
Mabaya kuyabaini (ub.2).

Jiepushe sana sana
Na mambo yaso maana
Yachunguwe ewe mwana
Maovu usiyabuni (ub.3).

Hata hivyo ametumia fomula inayotumiwa na watunzi wa tenzi katika kufunga utenzi. Watunzi huwa wanatangaza kuwa wametimia mwisho wa utenzi wao. Wengi huomba radhi kwa kutotunga kazi nzuri na kukubali kuwa, wako walio mahiri katika utenzi kuwashinda wao.. Kwa hivyo huomba kurekebisha iwapo kazi yao itapatikana na makosa. Wengine hujitambulisha kwa majina yao kama watunzi wa tenzi husika na mwishowe kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha kutunga kazi hiyo. Katika beti kumi za mwisho (ub.388-398), mtunzi anasema kuwa, utenzi umewalenga wazazi. Anawakumbusha kuwa yaliyomo ni ya zamani waliokuwa wakitendewa majumbani. Anamshukuru Mungu kwa kumpa nuru ya macho na kumjalua mikono ya kuandikia. Anawaomba Waislamu wote na kuwatakia mema. Mwishowe, anajitambulisha kwa kutaja jina lake na alikozaliwa. Mtindo huu wa kuhitimisha tenzi unapatikana katika tenzi zingine za Kiswahili kama tutakavyoona katika beti za mwisho za *Tenzi za Fatuma, Siri Li Asirali na Howani Mwana Howani*. Katika *Utenzi wa Howani Mwana Howani*, mtunzi anasema:

L-hakira jina langu
Amenipa baba yangu
Hapo kuzaliwa kwangu
Malindi ya Mkocheni (ub.396).

Naishi hapo Unguja
Na Pemba yake ni moja
Yeyote anayekuja
Jamhuri Tanzania (ub.397).

Zaynabu ndilo jina
Na Himidi hafatana

Muhamedi hapo tena
Lamalizia mwishoni (ub.398).

Utenzi wa Fatuma:

Nami ni mwane Amini, nimezoandika yuwani
Ni mwakwe shingoni, atatuhifazi Jalia (ub.438).

Tama basi, nimekwisa, sihitaji kupa sasa
Na mkiona makosa, sicheni kunitolea! (ub.439).

Utenzi wa Siri Li Asirali:

Kutoweza kuyawanga, mimi siyuwi kutunga
Si shairi si malenga, wala sina utambuzi (ub.553).

Na mkitaka nasabu, isimu yangu na abu
Ni mimi Mwana Mwarabu, na baba ina li wazi (ub.556).

Baba wangu watapamba, itwa Shekhe Bwana Lemba
Ya Rabi alimuumba na majaza kamjazi (ub.557).

Ilimu na Kuru' ani, alimjazi Manani
Nalishandwa Kivundoni, kwa nduze na kwa wazazi (ub.558).

- 2) Shairi lina jumla ya beti mia tatu tisaini na nane.
- 3) Kila ubeti una mishororo minne, imechukua mkondo wa kitarbia
- 4) Kila ubeti una kina kimoja ambacho kinahitilafiana na cha kila ubeti unaofuatia,
kwa mfano:

(ub. 1-3):

ub.1	za	ub. 2	a	ub.3	na
	za		a		na
	za		a		na
	ni		ni		ni

Kama ilivyo dhahiri katika mifano iliyo hapo juu, kila ubeti una urari wake wa vina unaohitilafiana na wa beti zinazofuatia.

- 5) Kina cha mshororo wa nne wa kila ubeti ni cha aina ya bahari, kimerudiwarudiwa.
- 6) Kila mshororo una mizani nane.

3.2 LUGHA

3.2.1 UHURU WA KISHAIRI

3.2.1.1 LAHAJA YA KIAMU

Mtunzi ametumia baadhi ya msamiati ufuatao wa Kiamu katika utenzi kwa sababu ndiyo lahaja sanifu ya utunzi wa mashairi: **Pulikiza** (kusikiliza-ub.1), **muwele** (mgonjwa-ub.49), **kalili** (kidogo-ub.83), **mboni** (macho-ub.130), **hapanapo** (hapana-ub.233), **pakambwa** (pakasemwa-ub.236), **wakamba** (wakasema-ub.251), **moya moya** (moja moja-ub.281), **akali** (kidogo-ub.290), **muwala** (magonjwa-ub.360), **tuli** (tulikuwa-ub.85), **sende** (usiende-182) **matungu** (ub.323), **aliteka** (alicheka-ub.170), **va** (vya-ub.264).

3.2.1.2 MSAMIATI WA KIARABU

Maneno aliyotumia mtunzi yametoholewa na mengine yana matamshi ya lugha ya Kiarabu. Ameathiriwa na lugha ya Kiarabu kwa kuwa alilelewa Unguja wakati ambao Waarabu walikuwa washapenya huko kwa sababu za kibiashara: **Ithneni** (mbili-ub.284),

inshalla (panapo majaaliwa-ub.368), **bibarakati** (baraka za-ub.117) **kunfayakuni** (hapo hapo bila ya kukawia-ub.117), **akraba** (jamaa waliohusiana-ub.124), **ikhwani ihwani** (ndugu-ub.125), **ihsani** (hisani-ub.150), **lamu, kafu** (L, K-ub.181), **quwa** (mwenye nguvu-ub.190), **ihaji** (haji-ub.204), **thinaashara** (kumi na mbili-ub.235), **sinini** (miaka-ub.235), **wahidi** (mmoja-ub.282) **abadani** (kabisa-ub.299), **nisai na niswani** (mwanamke na mwanamume-ub.309), **khamisa ishirini** (ishirini na tano-ub.305), **khamra** (ulevi-ub.359), la haula (jamani-ub.369), **Ya ilahi ya Ghafuru** (Mungu mwenye kufuta dhambi-ub.390), **burhani** (zawadi nzuri-ub.365), **fi-lawhi mahfudha** (kitabu kiandikwacho habari na vitendo vya kila mja-ub.279), **mahluki** (kiumbe-ub.370) **beiti** (nyumba-ub.295), **banu** (ukoo-ub.290), **sitara** (stara-ub.112), **khadharani** (kijani-ub.275), **alifu** (herufi ya kwanza ya alfabeti za Kiarabu-ub.158).

Licha ya mtunzi kutohoa msamiati huu, baadhi ya maneno ya Kiswahili aliyoyatumia pia yana matamshi ya lugha ya Kiarabu. Mtunzi ametumia herufi **kh** badala ya **h**: **khasa** (hasa-ub.116), **amekhitimu** (amehitimu-183), **makhluku** (vilivyoumbwa-350), **akhera** (ahera-ub.307), **anokhalifu** (anayehalifu-299), **khaini** (haini-ub.364), **maskhara** (masihara-ub.104).

3.2.1.3 MSAMIATI WA KIINGEREZA

Mtunzi ametohoa msamiati wa Kiingereza. Ameutumia msamiati huu japo kwa kiasi kidogo kwa kuwa alisoma kupitia kwa mfumo wa elimu wa kimagharibi: **vitamini** (vitamins-ub.155), **nambari wani** (number one-ub.262), **chaki** (chalk-ub.275), **saini** (sign-ub.387).

3.2.2 MBINU ZA UTUNZI

3.2.2.1 MPINDUO WA SARUFI

Mpinduo wa sarufi umetokea katika mishororo mingi kwa sababu ya kutimiza urari wa vina: **Hii ndio mama hali** (hii ndio hali mama-ub.31), **wako wema majirani** (wako majirani wema-ub.47), **na kusomwa nyingi sura** (na kusomwa sura nyingi-ub.97), **kwenye lesa mefungiwa** (mefungiwa kwenye lesa-ub.101), **mwanamke tapokuwa** (tapokuwa mwanamke-ub.130), **wenye njema nyingi kazi** (wenye kazi nyingi njema-ub.146), **wa hapo kale zamani** (hapo zamani wa kale-ub.175), **vyote hivyo shika mama** (shika hivyo vyote mama-ub.320), **mwenye nayo mama mche** (mche mwenye nayo mama-ub.327), **amenipa baba yangu** (baba yangu amenipa-ub.396), **ni nyembamba yako njia** (njia yako ni nyembamba-ub.10).

3.2.2.2 TABDILA

Mtunzi ametumia mbinu hii kwingi katika utenzi kwa sababu ya kutimiza urari wa vina: **jama** (jamani-ub.26), **tejeteje** (teletele-ub.141), **nabiyuna** (nabii-ub.227), **nakuoneza** (nakuonyesha-ub.280), **zisikiya** (zisikie-ub.281), **hino** (hii-ub.306), **sitachosha** (sitachoka-ub.368), **pahala** (pahali-ub.139).

3.2.2.3 MAZIDA

Baadhi ya maneno yalimerefushwa kwa sababu ya kutimiza urari wa mizani na vina: **kakupakaa** (kakupaka-ub.62) **ukifikiliya** (ukifika-ub.171), **hapanapo** (hapana-ub.233), **humuno** (humu-ub.30).

3.2.2.4 *INKISARI*

Mtunzi amefupisha maneno kwa kuwa alitaka kutimiza urari wa vina na mizani: **kele** (kelele-ub.13), **mwanetu** (mwanawetu-ub.13), **jama** (jamani-ub.26), **hachonekani** (hakionekani-ub.62), **kogeshwa** (kuogeshwa ub.91), **tamtowa** (watamtoa-ub.92) **jama** (jamani-ub.97), **mefungiwa** (amefungiwa-ub.101), **yalo** (yalio-ub.316), **wili** (wawili-ub.336), **mjawe** (mja wake-ub.330), **tapokuwa** (utakapokuwa-ub.130), **alonacho** (alicho nacho-ub.131), **wenetu** (wana wetu-ub.133), **kitoka** (yakitoka-ub.136) **jinale** (jina lake-ub.170), **rangiye** (rangi yake-ub.257) **mekujuza** (nimekujuza-ub.278), **kitabuche** (kitabu chake-ub.299), **jazaye** (jaza yake-ub.310).

3.2.3 *TAMATHALI ZA USEMI*

3.2.3.1 *TASHBIHI*

Mtunzi ametumia tashbihi ili kufafanua zaidi anachokizungumzia: **Ulikuwa kwenye tumbo mefunga kama mtambo** (umenyamaza kama kitu kisicho na uhai-ub.8), **ukuwe kama mgomba** (ukuwe haraka-ub.145), **nikahesabu miezi mithili yake mkwezi** (akahesabu miezi kama mtu anayengojea kuangua nazi-ub.19), **alikuwa yeye tende mfano wa peremende** (alikuwa mzuri-ub.34), **ikatandikwa na nguo mfano godoro...**(nguo ikafanywa godoro-ub.61), **ukuwe kama mnazi** (awe wa manufaa kwa jamii-ub.146), **huimba kama chiriku** (huimba kwa sauti nzuri anavyoimba chiriku-ub.140), **akayajuwa sihaba maneno kama katiba** (akayajuwa maneno yanayohusu unyumba kama ijulikanavyo sheria-ub.253), **fatani ni kama nyoka, mwenye sumu isotoka** (fatani.haachi fitina, kila anakokwenda anasababisha watu kukosana-ub.333), **watu ni kama siafu** (watu ni wengi-ub.213).

3.2.3.2 *SITIARI*

Msanii ametumia sitiari kwa lengo la kuchora taswira ya kiulinganishi kati ya vitu viwili vilivyo na sifa sawia: **Mgongoni ulitoka ni tone lisilo shaka** (ulitoka kwenye maji yenye mbegu ya uzazi-ub.9), **ni wewe ini langu** (mimi na wewe ni kitu kimoja-ub.358), **maziwa yako ni dawa** (maziwa yako yana chembechembe za afya ya mwili-ub.149).

3.2.3.3 *JAZANDA*

Jina Sihadaike, alilopewa mtoto alipozaliwa ni jazanda au fumbo lililo na ujumbe kwa mtoto. Anaambiwa asihadaiwe na dunia. Mtunzi anasema:

Mwanangu **sihadaike**

Maneno yangu yashike

Dini ndio peke yake

Itokutia peponi (ub.234).

Dunia **sikuhadaye**

Waovu uwaambaye

Usiwe karibu naye

Muovu kimbaini (ub.324)

3.2.3.4 *METHALI*

Mtunzi ametumia methali kuonya na kuliwaza. Amebadilisha kidogo muundo wa methali, anasema, 'Mola' badala ya 'Mungu' na 'kiwa' badala ya 'ndio': ... **polepole kiwa mwendo** (usifanye mambo kwa pupa-ub.267), ... **majuto ni mjukuu** (fanya mambo

wakati huu, usije ukajuta baadaye-ub.314), ... **Mola hamwachi mjawe** (Mola hamsahau anayemcha-ub.330).

3.2.3.5 MASWALI YA BALAGHA

Maswali yote ya balagha katika utenzi huu yametokea katika kibwagizo. Maswali ya balagha katika mishororo tuliyotaja yanaonyesha wasiwasi waliokuwa nao wazazi wa mamake Sihadaike: Hii ni balaa gani? (ub.12), hii ni miezi gani? (ub.14), mama anifanye nini? (ub.26), ...jina lake jama nani? (ub.97).

3.2.3.6 TASFIDA

Msanii amerejelea maji ya mbegu ya uzazi kama tone. Hakutaka kutaja neno 'manii' kwa sababu alitaka kuzingatia adabu katika kazi yake. Katika tasfida ya pili, njia nyembamba anayozungumzia ni sehemu ya siri ya wanawake, anapopitia mtoto anapozaliwa. ... mgongoni ulitoka, ni tone lisilo shaka (ub.9), ni nyembamba yako njia (ub.10).

3.2.3.7 MISEMO

Mtunzi ametumia semi katika utenzi kwa sababu ya kuitilia lugha nakshi kwani kazi ni ya kifasihi. Baadhi ya semi alizotumia ni: ...**mama roho juujuu** (mama alikuwa na wasiwasi-ub.44), **huvutwa nyingi fikira** (watu hufikiri sana pamoja-ub.97), **kupigwa kura** (kuchagua kwa kuinua mikono-ub.97), **iwe kunfayakuni** (hapohapo bila ya kukawia-ub.117), **kukawa na heka heka** (kukawa na shughuli-ub.89) **hakuwa na macho juu** (hakuwa na haya-ub.166), **roho kumtapatapa** (roho kuhangaika-ub.209), **kupiga mbio** (kukimbia-ub.218), **kuvunja ungo** (kubaleghe-ub.236), **akapiga marufuku** (akakomesha-ub.350), **usikunje uso** (usikasirike-ub.376), **salama u-salmini** (utulivu na amani-ub.295)

3.2.3.8 *VISAWE*

Mtunzi ametumia visawe vikifuatana katika baadhi ya mishororo katika beti. Usanii huu ni wa hali ya juu katika fasihi kwa sababu unasaidia kuitilia kazi nakshi na kusisitiza ujumbe licha ya kutochosha akili za wasomaji. Baadhi ya visawe hivyo katika utenzi ni: Bila taabu na udhiya (ub.10), bila tabu na matata (ub.58), haraka na mbiyombiyo (ub.99) kwa shangwe vigelegele (ub.251), tegemeo tegemani (ub.329), sawa sawa sawiyani (ub.346). Visawe vya jina mtume (ub.210): Nabiya (ub.132), Mmaka (ub.205), Rasuli (ub.198), Nabii (ub.37).

3.2.3.9 *TANAKALI SAUTI*

Msanii ametumia tanakali sauti kwa lengo la kutoa picha halisi ya milio anayorejelea: Baadhi ya tanakali sauti alizotumia katika utenzi ni:... wa tatu ndio ke-ke-ke (ub.20), ...ndani kuku,... mchana pekupeku (ub.67), nimekaa dukuduku (ub.88), ... vijongoo ti-ti-ti (ub.264), kwenye vita ka-ka-ka (ub.356), muepuke pe-pe-pe (ub.363), ukafanywa zu-zu-zu (ub.59).

3.2.3.10 *NIDAA*

Nidaa alizotumia msanii kuonyesha hali ya mshangao, masikitiko au furaha ni: Utadhani kuna nini! (ub.47), ukaona mbona mambo! (ub.160), Ee! Mwana wa imani (ub.360), la haramu la nini! (ub.381), yenye joto jingi ati! (ub.137).

3.2.3.11 *USAMBAMBA*

Mtunzi ametumia usambamba katika utenzi kwa lengo la kusisitiza: ... mazuri kupambanua, mabaya kuyabaini (ub.2), asubuhi na jioni (ub.32, 44, 76), wale ngia wale toka (ub.89), kuumeni kuukeni (ub.375, 121), usiku pia mchana (ub.138), kuipua

kuteleka (ub.192), za nje hadi za ndani (ub.286), nisai na niswani (ub.309), mwanamume mwanamke (ub.346), jepesi lisiwe zito (ub.66), tajiri na masikini (ub.70) kwa mama au babaye (ub.103).

3.2.3.12 TAKRIRI

Takriri zinatokea katika viwango vya neno, vionyeshi na vielezi. Msanii anazitumia kwa kuwa ana uhuru wa kufanya hivyo kama msanii wa kazi ya kifasihi. Baadhi ya takriri hizo ni: ... sanasana (ub.3, 138), sawasawa (ub.149, 14), huyo huyo (ub.18), mwanangu mwanangu howa (ub.56), hivyo hivyo (ub.85), ile ile (ub.139), tejeteje (ub.141), motomoto (ub.163), mbiombio (ub.173), ndogondogo, mojamoya (ub.353), fimbo hizo fimbo miya (ub.353), kua mama kua (ub.144), humu humu (ub.214), hapa hapa (ub.316), howani mwana howani (ub.65), halla halla (ub.70).

Takriri za irabu zimetokea mwanzoni mwa mishororo katika baadhi ya beti kwa sababu ya mahadhi katika uimbaji shairi:

Usidhani hiyo fimbo
Ukaona mbona mambo!
Ufito hilo ni jambo
La kutowa hadharani (ub.160).

Uzijue kazi zote
Utapokwenda popote
Utakupata chochote ..
Cha kutia mdomoni (ub. 276).

3.2.3.13 MBINU REJESHI

Utenzi wote wa Howani Mwana Howani umejengeka kwa mbinu rejeshi. Mtunzi ametumia mbinu hii kufafanua mambo ambayo mtoto hayafahamu. Mama anamweleza mwanawe, ambaye sasa amekua (ub.2) taabu alizopitia na mimba yake hata wazazi wakafikia kutambua kuwa alikuwa ameshika mimba. Anamweleza kuhangaika walikohangaika wazee na bibi yake hadi alipojifungua (ub.7-59). Mtoto anaelezwa kwa kina alivyolelewa na kuelezwa kilamila inayofungamana na malezi iliyofanywa (ub.59-157). Mama alipoanza kumfundisha mtoto dini alipotoka unyagoni, alirejea nyuma kumweleza mwanzo wa dini ya kiislamu na jinsi Mtume Muhammadi alivyopigana na Makureshi (ub.208-227). Mama aliwarejelea watu katika Kur'ani tukufu kama vile akina Hajara, Daudi, Musa, Mama Hawa, Bi Khadija, Bi. Maryamu na Nabii Issa. Alimweleza mtoto mambo ya kishujaa waliyoyafanya na hivyo kuwa vielelezo vya waislamu wote. Bibi alipoitwa na mama kumfanyia mizungu mamake Sihadaike, bibi aliwarejelea Mama Hawa, Bi. Maryamu na Amina binti Wahabu, akamwambia mjukuwe kuwa hata nao pia walipitia aliyokuwa akiyapitia yeye (ub.32-39).

3.2.3.14 TASWIRA

Utenzi wa Howani Mwana Howani ni taswira ya kuzaliwa na kulelewa kwa mtoto wa Kiswahili. Taswira imekusudiwa kuonyesha picha halisi ya malezi ya mtoto wa Kiswahili. Mtunzi ameeleza kwa kina jinsi mtoto anavyofanyiwa mila baada ya kuzaliwa ili kumzuia na mahasidi pamoja na shetani, lolote baya lisimpate. Kushirikishwa kwa jamii katika kutekeleza mila hizi kunatupatia taswira ya mtoto kuwa mali ya jamii. Tunapewa taswira ya kulelewa kwa mtoto kutoka kuzaliwa hadi anapotimu miaka sita;

jinsi anavyopitishiwa katika mafundisho ya kidini na ya kimaadili chuoni, unyagoni na nyumbani.

3.2.3.15 TAABINI

Mtunzi anamtungia mamake aliyefariki na kuzikwa nchi ya mbali alipokwenda ziara *Utenzi wa Howani Mwana Howani* ni taabini kwa sababu unasimulia kumhusu mamake Zaynab. Zaynab ni mtunzi wa utenzi wa mamake aliyeitwa Mwanakukuwa (Sihadaike). tukufu ya Hajj.

3.2.3.16 NYIMBO / NGOMA

Mtunzi anasema kwamba mtoto alipozaliwa bibi aliimba nyimbo (ub.57). Alikuwa akimwimbia nyimbo za kumbembeleza alipokuwa akimlea kabla siku arobaini baada ya kuzaliwa kwake kutimia (ub. 64,143). Mtoto alipokuwa akilia usiku, waliokuwa chumbani, bila shaka kina mama, waliimba kama chiriku ili ile sauti ya mtoto ibaki ndani (ub.140). Sihadaike alipoenda unyagoni, ngoma ya mrima ilichezwa makusudi kuona mambo yalivyokuwa zamani (ub.246-247).

3.2.3.17 VISAASILI

Utenzi una visaasili vinavyorejelea mashujaa wa kidini. Msanii ametumia mbinu hii kueleza usuli wa mambo yasiyofahamika. Mama anamweleza mtoto kuhusu kuzaliwa kwa Mtume na jinsi nuru ilivyozagaa katika chumba alichozaliwa (ub.39). Isitoshe alipotimu miaka arobaini, aliteremshiwa Kur'ani Tukufu na Mungu (ub.300). Alipokuwa akipigana dhidi ya wapinzani wake alijificha katika pango la Ghari Thawri ambapo njiwa walikuwa wakija kuimba nyimbo na buibui akatia utando wake mlangoni kuzuia hatari yoyote ambayo ingetokea (ub.221, 224).

Mama anaangazia kwa ufupi kisa cha Hajara na mwanawe Sumaili alipokuwa na kiu wakiwanywa maji ya milima Safaa na Marwa (ub.217-219). Kisa cha Musa na Firauni pia kimeangaziwa (ub.289-290), mama amekirejelea katika wasia wake kwa mtoto anapomwambia kwamba ‘Usijifanye jabari mtazame Firauni’ (ub.317). Ama kwa kweli usimulizi wa visa hivi umeupa ujumbe wa msanii uzito kwa sababu vina misingi yake katika dini. Baadhi ya utamaduni, imani na itikadi za jamii ya Kiswahili zina misingi yake katika dini ya kiislamu.

3.3 WAHUSIKA

3.3.1 WAZAZI WA MAMAKE SIHADAIKE

Wazazi hawajatajwa kwa majina. Ni wazazi wenye huruma na tunaambiwa kuwa, kabla ya ugonjwa wa mtoto wao kujulikana walikuwa wakipiga kelele kuwa mwana wao yu taabani (ub.13). Hali ilipozidi kuwa mbaya, mama alimwita bibi amwangelilie mwanawe (ub.27). Mama ni mhafidhina. Alimwambia bibi amuanzie mwanawe mizungu; mila isiyo na utani (ub.27).

Baba ni mwajibikaji. Alimnunulia mamake Sihadaike ng’ombe wa maziwa ili akiwanywa chuchu ziwe zikitoa maziwa mengi ya kumnyonyesha mtoto (ub.153-156). Baba alitoa ujira wa kumlipa mwalimu chuoni Sihadaike alipohitimu (ub.185-186).

3.3.2 MAMAKE SIHADAIKE

Huyu ndiye mhusika mkuu katika utenzi. Msanii amentumia sana katika kuwasilisha ujumbe wake. Alikuwa mbichi katika mambo ya uzazi, hakujua alichokuwa anaugua (ub.7). Mamake Sihadaike ni mhafidhina. Anapomsimulia mwanawe kuhusu ulezi wa

mimba yake, kuzaliwa kwake na kulelewa kwake, anasisitiza kumkumbusha kuwa mambo mengi aliyofanyiwa akiwa mchanga yalifanywa kulingana na mila yao wala hayakuwa ila (ub.70, 74, 130, 175, 139, 138, 271, 369). Mama anatumai kwamba Sihadaike atazishika mila zao kwa haraka ili apate baraka (ub.371). Mtunzi mwenyewe anayamulika yaliyosemwa na mama kwa kuisitiza kuwa zama zile za wazee zatakiwa zirejee, zienee visiwani hadi barani kwa sababu heshima yao ndiyo hiyo (ub.388-389).

Mama ni mwalimu na mlezi wa mwanawe. Alimnyonyesha Sihadaike mpaka alipokua, akapelekwa chuoni akiwa na miaka sita. Alipotoka chuoni baada ya mwaka mmoja, mama alimfundisha kupika (ub.192). Alimfunza nguzo tano za kiislamu (ub.193-204) na akamkumbusha kuwa ayashike maneno yake kwa sababu dini peke yake ndiyo itamtia peponi (ub.234).

Sihadaike alipotimia miaka kumi na miwili (ub.235), alivunja ungo na akapelekwa unyagoni. Alipotoka huko, mama alimfundisha mambo ya wazee wake yaliyo ya kitamaduni (ub.256). Alimfunza kusuka ukili, kupika rangi ya mikeka, kushona makawa, mikeka na misala, kushona kwa charahani, kusuka nywele na kufuma karatasi za masikio. Mama alimweleza mwanawe kuwa atakapolewa na pengine atakachopewa kisimtoshe jikoni, akiwa na darahima zake, ataendeleza nyumba (ub.256-277). Mama alimuusia mwanawe na kumtahadharisha dhidi ya maovu kama husuda, fitina, wizi, ulevi na kutowatii wazee (ub.325-384). Mama aliujenga msingi wa kimaadili wa mtoto.

Mama ni mcha Mungu kwa hivyo anamsisitizia mwanawe kushika dini. Yeye mwenyewe anayajua mengi kuhusu dini kama vile nguzo tano za kiislamu, vitabu vinne vya Mungu, usuli wa dini ya kiislamu, siku ya kiyama na kisa cha Adamu na Hawa.

3.3.3 BIBI

Bibi kama vile baba na mama hajatajwa kwa jina. Ni mhafidhina, na mjuzi wa mambo ya kitamaduni yanayofungamana na ulezi wa mimba na mtoto pamoja na wakati wa kujifungua. Mama alimwita kumshughulikia mwanawe akiwa taabani (ub.27). Bibi ndiye alikuwa mkunga (ub.15). Alimpokea mtoto alipozaliwa na akatekeleza mila zote za kuzaliwa kwake.

Bibi ni mcha Mungu. Alikuwa paziani na msahafu mkononi akimwombea dua mjukuu wake ajifungue salama (ub.46). Alipojifungua, alimwangualia mtoto na dua za Rahmani (ub.55).

3.3.4 WANAJAMII

Hii ni jamii iliyo na ushirika. Mamake Sihadaike anapokaribia kujifungua, majirani wanajaa ukumbini mwao ili mamake mtoto anapopiga siyahi, waige ili kelele zile zisije penya na kuenea mitaani (ub.52). Mtoto anapotolewa chumbani baada ya siku arobaini kila mtu hufurahi. Wazee huja pamoja kupiga kura na kusoma sura nyingi huku wakivuta fikira pamoja kutafuta jina litakalopewa mtoto (ub.97-107).

Ni jamii ya kihafidhina. Wanajamii wanazingatia mila zinazofungamana na ulezi wa mtoto. Anapozaliwa, anafanyiwa mila zitakazomwepushia uhasidi na shetani (ub.74,

131). Wanaokuja kumwona mtoto pia hawaruhusiwi wote kumwona (ub.86) labda kwa kuogopa jicho la mahasidi. Mtoto alitiwa wanja machoni ili apunguze jicho mahasidi wasimwone (ub.131).

Licha ya kuhifadhi mila zao, jamii hii inamcha Mungu. Inawakuza watoto kwa misingi ya dini ya kiislamu. Sihadaike alipelekwa chuoni alipotimu miaka sita, licha ya kufundishwa alifu, alifunzwa Kur'ani Tukufu pia, aliporudi nyumbani mama alimsisitizia maadili aliyopasa kuwa nayo mtoto mwislamu. Maadili na tabia zinazofunzwa watoto pia zina misingi yake katika dini (ub.159-169).

3.4 TONI

Utenzi unianza kwa toni ya wasia. Mama anamuusia mwanawe ambaye amemlea kwa taabu tokea ashike mimba yake, kujifungua na kumlea hadi alipofika. Anamwambia kwamba atambue mazuri na kuyabaini mabaya (ub.2). Anarudi nyuma na kumhadithia alivyoilea mimba yake. Anawaeleza wasioujua uzazi kuwa kulea mimba na kuzaa ni kazi (ub.50). Mtoto anaporudi nyumbani kutoka chuoni, mama alimuusia kushika dini, kwani ndiyo pekee ingemtia peponi (ub.234). Mama alimtajia mwanawe maovu ya husuda, fitina, wizi, uzinifu na ulevi, akamwambia ajiepushe nayo (ub.326-364). Licha ya hayo, alimwambia awaambae waovu pia (ub.324).

Katika beti za mwisho za utenzi, mtunzi anaeleza msimamo wake kuhusu aliyoyasema katika utungo wake. Toni ya kuwasihi wanajamii kuuhiifadhi utamaduni inadhihirika:

Zama zile za wazee
Zatakiwa zirejee
Visiwani zienee
Na pia hadi barani (ub.389).

Kwa yote yaliyohumu
Ya zamani mfahamu
Ndiyo yetu hitiramu
Kitendewa majumbani (ub.388).

Utenzi umetungiwa wote walio wazazi (ub.387) kwani kuzaa ni kazi kubwa. Mtunzi ameonyesha ulezi wa mtoto tangu awe tumboni hadi kufikia uwari. Anawafunza na kuwakumbusha wazazi wajibu wao katika malezi ya mtoto tukizingatia kuwa mambo ya kiutamaduni yalikuwa yameanza kusahuliwa alipotunga kazi hii (ithibati katika ub.389). Mtunzi alionyesha vile mtoto alivyolelewa tokea alipoingia tumboni hadi alipozaliwa. Alionyesha kila mila iliyozingatiwa katika malezi ya mtoto.

Toni ya dini na mafunzo ya maadili kama msingi wa maisha ya mtoto imetokea katika utenzi. Wahusika ni sauti ya mtunzi kwa hivyo mtunzi amemtumia mama na mwalimu kuonyesha thamani na uzito alioipa dini katika malezi ya mtoto. Mtoto ndiye amelengwa katika mafunzo hayo lakini pia mtunzi anataka mzazi awajibike na kuyatekeleza.

Mtoto alianza mafunzo mapema akiwa na umri wa miaka sita. Alipelekwa chuoni alikofunzwa Kur'ani Tukufu, unyagoni alifundishwa unyumba na tohara na jinsi anavyoweza kuzingatia usafi akiwa katika haidhi (ub.241-244). Baadaye mama alikuwa na jukumu la kumfunza nyumbani pia. Mama alimfunza nguzo tano za kiislamu, vitabu

vinne vya Mungu na akamweleza usuli wa dini ya kiislamu. Alimweleza kuhusu akhera na peponi na jinsi anavyoweza kukwepa kwenda akhera siku ya kiama kwa kutenda yaliyo mema. Alimtajia kwa kifupi maovu anayofaa kuepukana nayo. Licha ya kumfundisha na kumwambia mengi kuhusu dini ya kiislamu, mama alimfunza mtoto kazi na maadili.

Toni ya furaha inadhihirika mtoto anapozaliwa. Kina mama wanashangilia kwa vigelegele (ub.54). Bibi anaomba dua na kuimba (ub.55-57). Siku ya kumtoa mtoto chumbani inakuwa pia ya furaha, watu wanajaa nyumbani (ub.120). Kunakuwa na heka heka. Ndiyo siku ya kumpa mtoto jina pia: Wazee, vijana na akina mama wanajaa ukumbini (ub.94, 95) wakimpa mamake mtoto mkono wa kujaaliwa kuvuka salama. Majirani nao pia hujaa na watu wakasherehekea. Mtoto anapelekwa kwa nyumba za akraba na majirani wa karibu. Hiyo ni mila inayofanyiwa mtoto ili kuwafurahisha ikhwani (ub.124,125).

3.5 MSUKO

Msuko wa utenzi huu ni sahili. Matukio yanafululiza kwa utaratibu unaofaa. Mtunzi anakuza kila tukio kulingana na kutokea kwake kiwakati. Utenzi unapoanza, msanii anaeleza ulezi wa mimba ya Sihadaike kimantiki kuanzia mwezi wa kwanza mamake aliposhika mimba hadi wa tisa alipojifungua (ub.19-51). Amewasilisha matukio ya utenzi huu jinsi yanavyotokea kiwakati. Utenzi unasimulia matukio matatu makuu: Ulezi wa mimba, kuzaliwa kwa mtoto, malezi ya mtoto (chuoni, unyagoni na nyumbani). Ndani ya matukio haya mna masimulizi ya visa vidogo vya kidini ambavyo ni msingi wa kimaadili na wa kidini wa maisha ya mtoto mwislamu.

Msanii ametumia kaida za kuboresha msuko katika kazi ya kifasihi. Tutatathmini kaida zote alizotumia msanii katika utunzi wa utenzi huu na kuzieleza kadri ya uwezo wetu. Msuko wa utenzi umejengeka kwenye mbinu rejeshi. Utenzi unaanza kwa hotuba ya mama kwa mwanawe (ub.1-6). Mtoto tayari amekua, anaweza kuyabaini mabaya na kuyapambanua mazuri (ub.2). Mama anarudi nyuma kumweleza mtoto jinsi alivyoichukua mimba yake na kuilea hadi alipojifungua (ub.7-52). Katika usimulizi wake, alirejelea visa vya kuzaliwa kwa Nabii Issa na Mtume Muhammad (S.A.W) ambavyo bibiye alikuwa akimsimulia alipokuwa mja mzito (ub.31-40).

Mama alimweleza mwanawe alivyolelewa chuoni, unyagoni na hata alivyomfunza kazi nyumbani. Alipokuwa akimfunza dini, alimweleza jinsi mtume alivyopigana na wapinzani wake, jinsi Mungu alivyomteremshia Kur'ani Tukufu (ub.208-220). Alimsimulia kisa cha Adamu na Mama Hawa na jinsi walivyozainiwa na ibilisi (ub.231, 334, 339), kisa cha Hajara na mwanawe Sumaili (ub.217-219), na akamweleza kuhusu haji, mji mtakatifu wa Maka, kaaba tukufu (ub.213-216), pango la Ghari Thawri alimojificha Mtume na Abubakari wakiwakimbia maluuni (ub.221-226), Jabali Arafa (ub.229-230) na milima ya Safaa na Marwa walikokunywa maji Hajara na mwanawe.

Msuko wa utenzi umejengeka kwenye mbinu elekezi au kionambali. Kama hali ilivyo katika *Utendi wa Qiyama*, msanii amezungumzia kuhusu maisha wakati wa siku ya mwisho kwa misingi ya dini ya kiislamu. Mama alimuusia mwanawe kuhusu maadili na akhera. Alimwambia kuwa ni siku ya mwisho, siku ya kitisho ambapo maiti hufufuliwa

na kusomewa makosa yake (ub. 306-317). Anamwambia kuwa awe akisali ili asiingie mashakani na kujuta siku hiyo.

Mpangilio wa matukio unahusisha matumizi ya visaasili. Msuko wa utenzi huu unafuata mpangilio huu kwa sababu umetegemezwa kwenye visaasili vinavyopatikana katika Kur'ani Tukufu. Msanii ametumia matatizo kama kihamasishaji cha msuko wa hadithi yake kama tunavyoona katika visa vya Bi. Maryamu, Mama Hawa na Bi. Amina walivyochukua mimba na kuzilea katika Kur'ani Tukufu. Mama anamweleza mtoto kisa cha kuzaliwa kwa mtume kama alivyotambiwa na bibi, alivyopokea Kur'ani Tukufu kutoka kwa Mwenyezi Mungu alipokuwa na umri wa maka arobaini na alivyopigana na wapinzani wake.

Ameangazia pia kisa cha Adamu na Hawa, walivyohadaiwa na ibilisi, Mungu akawaondoa peponi na jinsi ibilisi anavyojigeuza joka au moshi, kuingia tumboni mwa mtu na kumwongoza kutenda maovu. Aliwaangazia mashujaa wa kidini kama vile Daudi, Musa, Issa na Hajara.

Msanii ametumia kaida ya udondoshi katika kazi yake. Kaida hii huhusu kuachwa au kudondoshwa kwa sehemu za hadithi. Hili ni jambo la kawaida katika usanii kwa sababu hakuna hadithi ambayo husimuliwa kwa ukamilifu. Isitoshe, uandishi unahusu uteuzi na uteuzi unahusu kuacha sehemu fulani ambazo si muhimu kwa mujibu wa msanii. Msanii ameeleza kuhusu matukio makuu peke yake katika maisha na malezi ya mtoto na kudondosha yasiyo muhimu. Ameelezea miezi ya kubeba mimba, siku ya kuzaliwa kwa

mtoto, kutolewa kwa mtoto chumbani, siku zake za chuoni na siku ya kubaleghe na kupelekwa unyagoni na siku alizokuwa akipewa wasia na mamake. Matukio yanayotokea kati ya hatua moja na nyingine yamedondoshwa.

Visa vyote vilivyoelezwa kuhusu mashujaa wa kidini vimeangaziwa tu. Misururu ya visa hivyo imedondoshwa na yale ya muhimu ambayo yanampasa msomaji kujua yameelezwa.

3.6 WAKATI

Mtunzi alitunga kazi hii katika karne ya ishirini baada ya wageni kuingia kisiwani na elimu ya kimagharibi kupenya katika mfumo wa elimu. Kimsingi, tukiangalia wakati kwa upana katika utenzi huu kwa kurejelea kipindi cha kihistoria ambacho kazi hii ilitungwa, tunagundua kuwa, utamaduni ulikuwa umeanza kusahauliwa. Beti nyingi katika utenzi zinadokeza kuwa ada, mila na mafunzo ya dini na dunia yanayoambatana na vipindi mbalimbali vya maisha ya mtoto wa Kizanzibari yalikuwa yanakabiliwa na hatari ya kumezwa na kugubikwa na utamaduni wa kisasa wa kigeni. Mtunzi akautunga utenzi wakati huo ili ayaweke katika kumbukumbu mambo haya ili yasisahauliwe.

Kipengele cha wakati katika kazi kimefumbatwa kwa sababu ya matumizi ya udondoshi wa sehemu za utenzi. Matukio ya miezi tisa ambayo mama anabeba mimba hadi anapojifungua yameelezwa. Mtunzi anasimulia kuhusu maisha ya mtoto baada ya kuzaliwa hadi siku ya arobaini ambapo anatolewa chumbani na kupewa jina. Baadaye, tunasimuliwa kuhusu mtoto akiwa na umri wa miaka sita anapopelekwa chuoni. Anarudishwa nyumbani akiwa ametimia miaka saba na mama anamuanzisha mafunzo ya

nyumbani (ub.157, 183, 184). Anabaleghe akiwa na umri wa miaka kumi na miwili (ub.235) na kupelekwa unyagoni. Mtunzi anatuonyesha mama akimpa wasia wa kimaadili akiwa na umri wa miaka kumi na minne (ub.372).

Visaasili katika utenzi vimeelezwa katika wakati uliopita ilhali hotuba iliyokusudiwa Sihadaike imetolewa katika wakati uliopo. Mtunzi ametumia pia wakati uliopo usiodhihirika katika beti ambazo ujumbe unailenga jamii moja kwa moja haswa anapoikumbusha kuwa mambo anayoyazungumzia ni mila zao (ub.384, 388, 389, 373). Wakati katika utenzi umeelezwa na mwandishi na wahusika kupitia mbinu rejeshi. Iwapo tutakadiria wakati ambao matukio katika utenzi yamechukua kutendeka, tutachukulia kwamba yametendeka kwa miaka kumi na mine kwa sababu alipewa wasia akiwa na miaka kumi na nne (ub.372).

3.7 USIMULIZI

Usimulizi ulio katika utenzi ni rahisi kuuelewa. Usimulizi uliotawala utenzi ni wa nafsi ya kwanza. Mtunzi amewapa nafasi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja. Usimulizi wa mama unatawala utenzi lakini katika beti zingine anachukua nafasi ya msimulizi wa nafsi ya tatu. Anaeleza kuhusu wahusika wengine pia.

Katika beti zingine, wahusika kama vile baba na mamake Sihadaike wanazungumza moja kwa moja. Wanafanya hivyo kwa kupewa nafasi hiyo na msimulizi wa nafsi ya kwanza (mama) ambaye anawaachilia kuwasilisha kwa nafsi ya kwanza (ub.27, 105-108, 110, 111).

Katika beti zingine, msimulizi anakuwa nje na anauchukua mtazamo wa mbali na hata kuyatathmini mambo yaliyofanyika. Hii ni nafasi iliyochukuliwa na mtunzi mwenyewe katika kazi. Msanii amejitokeza kwa njia wazi kuyasema mambo yanayohusu mila na itikadi na kutoa maoni yake. Kuhusu mambo ya kitamaduni yalioangaziwa katika utenzi tunahisi kuwa yanaakisi sauti ya msanii anayetoa maoni yake kuhusu mila na itikadi (ub.389, 175, 247, 369, 384, 138, 125).

Wahusika ni sauti ya mwandishi na huwatumia kuwasilisha ujumbe wake. Mtunzi wa utenzi huu amechukua nafasi ya mhusika mama katika kazi yake na kuwa kama msimulizi mwandishi. Anahisika katika beti za utenzi wake, yeye ndiye mwasilishaji aliyejificha haonekani waziwazi. Anajitambulisha mwishoni mwa utenzi kama mtunzi na anayoyasema yanamtambulisha kama msimulizi pia (ub.384-391).

3.8 MANDHARI

Mandhari ya usimulizi yanabainika wazi katika utenzi. Anasimulia mazingira ya kitamaduni yanayohusu malezi ya mimba na mtoto tangu anapozaliwa hadi anapovunja ungu. Mazingira ya kimalezi ya mtoto wa Kiswahili yamesimuliwa katika utenzi wote. Malezi hayo hufungamana na utamaduni wa dini ya Kiislamu.

Mtunzi ameeleza mila zinazofungamana na kila hatua ya malezi. Anasema kwamba mama anapochukua mimba, mkunga huwa jirani au bibi kwa sababu siku hizo hakukuwa na madaktari (ub.14, 15). Bibi kama mkunga alimfanyia mizungu na mila zote hadi alipojifungua. Alimpokea mtoto duniani alipozaliwa na kumkata kitovu. Bibi aliendelea kumfanyia mtoto mila zingine akiwa ndani kwa muda wa siku arobaini kama vile:

Kumtona wanja kila mara ili apunguze jicho na atakapokuwa mwanamke awe na haya za mboni (ub.130), kupakwa madawa asubuhi na jioni ili litakalokuja kumdhuru lipae huko mbinguni (ub.127-128), kutimiza mila za kumpeleka kwa nyumba za akraba (ub.124, 125), kurembwa usiku na mchana ili awazibe mashetani (ub.139) na kufungwa mivuje na kufukizwa mafusho ili afuje lolote liletwalo na majini (ub.141).

Mama alikuwa akifanyiwa mila hizo sambamba na mwanawe kwa muda wa siku arobaini. Alifukizwa kwa madawa, kukandwa na kusingwa mwili kwa madawa ili mwili ulainike na apate nafuu haraka. Siku arobaini zilipokwisha, watu walitoka mashambani na katika mitaa jirani kuja kushuhudia mtoto akitolewa chumbani (ub.120, 121). Mtoto alitolewa chumbani kwa furaha na vigelegele akapewa jina kwa utaratibu wa kitamaduni (ub.97-108). Katika wasia wa mama kwa Sihadaike, alikuwa akimweleza kuwa aliyokuwa akimwambia ni mila zao, akamwambia kuwa angeendelea kuunga wasia wake na utamaduni mwingi (ub.373). Mwishowe, alimweleza kuwa alitumai angezishika mila zao kwa haraka ili apate baraka (ub.371).

Malezi hayo hufungamana na mafundisho ya dini ya kiislamu kwa hivyo kuna mandhari ya dini pia. Wahusika ni wacha Mungu. Bibi alikuwa na msahafu mkononi chumbani akimwombea mjukuu wake dua ili ajifungue salama (ub.46). Alikuwa akimwombea mtoto dua (ub.144). Baba alimsomea mtoto sura katika Kur'ani Tukufu siku aliyotolewa chumbani na akamwombea dua (ub.109-111). Mama alimwambia mtoto kuwa Mungu ndiye alimuweka asifiye tumboni (ub.6) anamwambia pia kuwa akimjua Mungu ataupata murua na kupoa duniani, hatakuwa mtu duni (ub.383).

Mtoto huanza mafundisho ya dini akiwa na umri wa miaka sita anapopelekwa chuoni. Akiwa huko anafunzwa kusoma Kur'ani Tukufu na kurudishwa nyumbani baada ya mwaka mmoja. Mama anakuwa mwalimu wake wa dini nyumbani. Mtoto anafundishwa maadili kwa misingi ya mafundisho ya dini ya kiislamu. Utenzi umejaa mafundisho ya dini. Mama anamweleza mtoto usuli wa dini ya kiislamu, Nabii Muhammad na manabii waliomtangulia. Anamzungumzia kuhusu nguzo tano za dini ya kiislamu kwa kina. Anamsimulia kuhusu kisa cha Adamu na Hawa na kumweleza kuhusu akhera na jinsi anavyoweza kuiepuka. Mama anamweleza maovu anayotakiwa kujiepusha nayo pia.

Mbali na kufungamanishwa na tabia, imani na utamaduni wa wahusika, mandhari yanaweza kuwa ya kimazingira (mahali panapowasilishwa wahusika). Katika utenzi, kuna mazingira mapana ya kisiwa cha Unguja ambapo ndipo makao ya mtunzi (ub.389). Mtunzi anatupa taswira ya maisha na malezi ya mtoto wa Kiswahili kisiwani na hali ya mambo katika kipindi hicho cha kihistoria alipotunga utenzi huo. Inabainika wazi katika mishororo ya utenzi na toni ya mtunzi kuwa, mila zinazohusu malezi na maisha ya mtoto zilikuwa zimeanza kusahaulika ndipo mtunzi akaona haja ya kuzitia katika kumbukumbu kwa kuziandika.

Taswira ya mandhari finyu inadhihirika chumbani alimozaliwa mtoto, ukumbini kwa akina mamake Sihadaike, chuoni, unyagoni na mandhari ya mahali ambapo visa vya kidini vilikuwa vikitokea (pangoni, milimani, peponi, jabalini na mijini). Mtunzi ameyaelezea japo kwa kuyaangazia tu. ..

3.9 HITIMISHO

Katika sura hii tumehakiki fani katika *Utenzi wa Howani Mwana Howani*. Tumetoa mifano mingi kwa kila kijenzi cha fani na tukaifafanua baadhi ya mifano hiyo. Mifano tuliyotoa inadhihirisha kuwa utenzi una muundo wa ndani na wa nje. Kimsingi, tumegundua kuwa fani ndizo hujenga sehemu kubwa ya kazi ya kifasihi.

SURA YA NNE

UHAKIKI WA FANI KATIKA UTENZI WA MWANAKUKUWA

4.0 UTANGULIZI

Tutahakiki *Utenzi wa Mwanakukuwa* katika sura hii. Tutachunguza jinsi mtunzi alivyojenga kazi yake kwa kutumia vijenzi vyote vya fani tulivyovieleza kwa kina katika sura ya pili. Hatutapoteza wakati kwa kuvieleza tena vijenzi hivyo vya fani, tutaenda moja kwa moja katika tenzi na kuonyesha fani hizi zilivyojitokeza.

4.1 UMBO

- 1) Fomula ya ufunguzi na kufunga katika tenzi ni jambo la kawaida lililoanza na tenzi zilizojikita katika maudhui ya maisha ya Mtume na dini ya kiislamu. Bi. Zaynab ameanza utenzi wa Mwanakukuwa kwa fomula hiyo. Katika beti mbili za kwanza anamsifia Mwenyezi Mungu, muumbaji ulimwengu na kumtaka amjaalie nuru na furaha nyingi moyoni. Baadaye anaeleza kiini cha utunzi wake na kuendeleza kazi yake. Anasema:

Bismillahi ghafuru
Nijaaliye sururu
Nifunguliye na nuru
Furaha nyingi moyoni (ub.1).

Muumbaji ulimwengu
Ardhi na pia mbingu
Bahari pia mawingu
Majini na insani (ub.2).

Anapotamatisa utenzi, anakiri kuwa wapo walio mahiri kumliko katika utunzi kwa hivyo anaomba asitiwe makosani, atajitahidi:

Utenzi nimemaliza
Pengine nimeyasaza
Mpate kuniuliza
Tayari takujibuni (ub.1224).

Wako walionizidi
Nakubali sina budi
Lakini najitahidi
Sinitie makosani (ub.1225).

- 2) Shairi lina jumla ya beti elfu moja, mia mbili ishirini na nane.
- 3) Kila ubeti una mishororo minne, zimechukua mkondo wa kitarbia.
- 4) Kila ubeti una kina kimoja ambacho kinahitilafiana na cha kila ubeti unaofuatia,

kwa mfano:

(ub. 1-3):

ub.1	ru	ub. 2	ngu	ub.3	za
	ru		ngu		za
	ru		ngu		za
	ni		ni		ni

Kama ilivyo dhahiri katika mifano iliyo hapo juu, kila ubeti una urari wake wa vina unaohitilafiana na wa beti zinazofuatia.

- 6) Kina cha mshororo wa nne wa kila ubeti ni cha aina ya bahari, kimerudiwarudiwa.
- 7) Kila mshororo una mizani nane.

4.2 LUGHA

4.2.1 UHURU WA KISHAIRI

4.2.1.1 LAHAJA YA KINGOZI

Lahaja hii ni ya kale. Mtunzi ametumia msamiati huu katika utenzi kwa kuwa ni jambo la kawaida wasanii kutumia msamiati chakavu: **uromboni** (mahali panapofundishiwa ngoma za wanawari-ub.10), **msungu** (mwanamke aliye mjinga katika mambo ya unyumba-ub.9), **utanga** (mkeka wa wanawari-ub.12), **manyakanga** (wanawake wanaosimamia wanawari unyagoni-ub.23), **vihendo** (vitendo vinavyotendwa unyagoni-ub.25), **chuwa** (chembe za mchele ambazo zina magamba-ub.34), kizingo, **mziwanda** (mtoto wa kiume wa kwanza kwa wazazi wake-ub.145), **matemwe** (kijiji kilichosifika kwa kuyatazama mambo ya ndoa-ub.190), **sapatu** (viatu vya kike vya zamani), **visero** (pesa zinazopewa watu wanaocheza unyagoni-ub.387), **mserego** (ngoma ya watu wa Mombasa-ub.766), **kanono** (kitoto kidogo, kichanga kinachopendeza-ub.773), **vitango** (vitu vya mwari-ub.567), **kuno** (huku-ub.1054).

4.2.1.2 LAHAJA YA KIAMU

Mtunzi ametumia baadhi ya msamiati wa Kiamu katika utenzi kwa sababu ndiyo lahaja sanifu ya utenzi wa mashairi: **Kupulikiza** (kusikiliza-ub.219), **katiti** (kidogo-ub.405), **kalili** (madogo-ub.654), **wali** (walikuwa-ub.907), **mwenge** (mtunze-ub.1015), **magegoni** (menoni-ub.1090), **kuno** (huku-1054) **huno** (huyu-1054), **akayatongoa** (akayajibu maneno kwa heshima zote-ub.242), **akambwa** (akasemwa-ub.553), **ninene** (niseme-ub.555), **wali kimwambia** (walikuwa wakimwambia-ub.907), **ntasaza** (nitasaza-ub.1057), **venye** (vyenye-ub.522), **hatamuwata** (hatamwacha ub.1089), **yankwisha**,

yansoza (yamemalizika-ub.1151), **kunnua** (kununua-ub.458), **yakenda** (yakaenda-ub.955), **kuguria** (kuhamia-ub.998).

4.2.1.3 MSAMIATI WA KIARABU

Maneno aliyotumia mtunzi yametoholewa na mengine yana athari za lugha ya Kiarabu kwa sababu ya mwingiliano wake na Waarabu walipokuja Kisiwani Unguja kwa sababu za kibiashara. Baadhi ya msamiati wa Kiarabu aliyotumia ni:

Ithneni (saa mbili-ub.957), **inshaalla** (panapo majaaliwa-ub.1074), **halbadiiri** (kisomo kinachoaminiwa na baadhi ya watu kwamba kinaweza kumdhuru anayesomewa baada ya kuwa amefanya jambo baya-ub.968), **ilahu** (Mungu wako-ub. 1014), **insani** (wanadamu-ub.2), **akraba** (jamaa-ub.229), **khushui** (adabu na heshima kubwa-ub.418), **khenshe** (treya-ub.403), **ikhbari** (habari-ub.224), **huru-l-ayni** (wasichana warembo wanaopatikana peponi-ub.1106), **alifu** (elfu-ub.467), **fakhari** (fahari-ub.231), **naumu** (usingizi-ub.647), **ikhwani** (ndugu-ub.451), **Bismillahi Ghafuru** (kwa jina la Mungu mwenye kufuta dhambi-ub.1), **libasi** (nguo-ub.568), **akhdhari** (rangi ya kijani-ub.887), **faradhi** (kitu kilicho lazima ub.1141), **salama u-salmini** (salama-ub.436), **sunu** (kitu cha hiari-ub.701), **insi** (watu ub.616), **ikrahi** (makuruhu-ub.921), **kalimati** (maneno-ub.1174).

Licha ya mtunzi kutohoa msamiati huu, baadhi ya maneno ya Kiswahili aliyoyatumia pia yana matamshi ya lugha ya Kiarabu. Mtunzi ametumia herufi **kh** badala ya **h**: **khatuwa** (hatua-ub.1036), **fakhari** (fahari-ub.393), **khamsini** (hamsini-ub.405), **shekhe** (shehe-ub.478), **kheri** (heri-ub.1138), **akhera** (ahera-ub.1170), **usijikhini** (usijihini-ub.1163),

makhsusi (mahsusi-ub.1050) **anatafakhari** (anatafakari-ub.838), **khitima** (ub.1193), **mas-khara** (masihara-ub.1160).

4.2.1.4 MSAMIATI WA KIINGEREZA

Mtunzi ametohoa maneno ya Kiingereza ingawa hajayatumia kwa wingi. Ameathiriwa na matumizi ya maneno hayo kwa sababu ya kupitia katika mfumo wa elimu ya kimagharibi. Baadhi ya msamiati aliyotumia ni: **Peya** (pair-ub.12), **nambari wani** (number one-ub.129), **namba** (number-939), **saini** (sign-ub.975), **pawa** (power-ub.427), **buluu** (blue-ub.491), **soksi** (socks ub.496), **anchifu** (handkerchief- ub.497), **makochi** (coaches-ub.549), **kampeni** (campaign-ub.1088), **aupasi mtihani** (to pass exams-ub.629), **picha** (picture-ub.842).

4.2.2 MBINU ZA UTUNZI

4.2.2.1 MPINDUO WA SARUFI

Mpinduo wa sarufi umetokea katika wingi wa beti: **anamwita wake mama** (anamwita mama wake-ub.678), **kuhubiri alianza** (alianza kuhubiri-ub.319), **watatu watu kufika** (watu watatu kufika-ub.310), **kwa mema yote yaliyo** (kwa yote yaliyo mema-ub.909), **mbona mbio unatoka** (mbona unatoka mbio-ub.942) **macho chini kutazama** (macho kutazama chini-ub.943), **kwako uwe makini** (uwe makini kwako-ub.17), **tumia yako kalima** (tumia kalima yako-ub.1121), **umpe nyingi hishima** (umpe hishima nyingi-ub.1121) **pia sisi wake watu** (pia sisi watu wake-ub.969), **sare yetu kanga hizi** (sare yetu hizi kanga-ub.521), **wambie wote wazazi** (wambie wazazi wote-ub.452), **zikapangwa hizo fedha** (zikapangwa fedha hizo-ub.353), **na mikononi mchele** (na mchele mikononi-ub.501), **Kukuwa wetu mwandani** (Kukuwa mwandani wetu-ub.550)

njema zote burhani (burhani zote njema- ub.866), ...**kwa nyingi zao uluwa** (kwa uluwa zao nyingi-ub.769).

4.2.2.2 *TABDILA*

Mtunzi ametumia mbinu hii kwingi katika utenzi: **jituliza** (jitulize-ub.38), **hini** (hii-ub.54), **somalini** (Somalia-ub.93), **fununi** (fununu-ub.119), **fedhani** (fedha-365), **hino** (hii-ub.403), **nakasha** (nakshi-ub.464), **hinyahinya** (himahima-ub.451), **wanzani** (wenzao-ub.501), **tayarini** (tayari-ub.707), **kito** (kitu-ub.774), **kafungasha** (kafunganya-ub.931), **mahala** (mahali-ub.998), **muonyesha** (ub.muonyeshe-1122), **sitakanya** (sitakana-ub.451) **hadisi** (hadithi-ub.455) **jalikoni** (jaliko-ub.483), **kuibiya** (kuibiwa-ub.597), **Ungujani** (Unguja-ub.689), **nalipochukuza** (nalipochukua-ub.3) **kumhusudi** (kumhusudu-ub.1111), **kuzingiya** (kuzingira- ub.758), **jama** (jamaa-ub.960).

4.2.2.3 *MAZIDA*

Msanii ametumia mbinu hii kwa lengo la kutimiza urari wa vina na mizani. Baadhi ya maneno yaliyorefushwa ni: **kukusanyikiya** (kukusanyika-ub.488), **zikachachawaa** (zikachachawa-ub.507), **hongerani** (hongera-ub.526), **tayarini** (tayari-ub.707), **mapiya** (mapya-ub.1122), **kumlahaki** (kumlaki-ub.912), **unanawirika** (unanawiri-ub.695), **hualikiwa** (hualikwa-ub.691), **pembezeni** (pembeni-ub.692), **jalikoni** (jaliko-ub.483), **kalimati** (kalima-ub.1174), **tamkutiya** (tamkuta-ub.79).

4.2.2.4 *INKISARI*

Mtunzi amefupisha maneno kwa lengo la kutimiza urari wa vina na mizani. Baadhi ya inkisari alizotumia ni: **walokivaa** (walizokuwa wakivaa-ub.603), **miminika** (walimiminika-ub.7), **wanokuwa** (wanaokuwa-ub.14), **yanobidi** (yanayobidi-ub.17),

yalokuwa (yaliyokuwa-ub.22), **mekuja** (umekuja-ub.53), **ndu** (ndugu-ub.55), **waloozwa** (walioozwa-ub.64), **kiangaza** (yakiangaza-ub.60), **atapongi** (atakapoingia-ub.79), **mana** (maana-ub.84), **metiya** (umetia-94), **ngia** (ingia-ub.274), **utalosema** (utakalosema-ub.160) **sifaze** (sifa zake-ub.147), **shidaze** (shida zake-ub.159), **uulani** (uulaani-ub.159), **ba** (baba-ub.139), **anayeoneka** (anayeonekana-ub.408), **shukura** (shukurani-ub.253), **muorodhe** (muorodheshe-ub.453). Iliyo katika kurasa zilizotangulia ni baadhi tu ya mifano michache ya mbinu za utunzi katika *Utenzi wa Mwanakukuwa* ambao una wingi wa matumizi ya mbinu hizi.

4.2.3 TAMATHALI ZA USEMI

4.2.3.1 TASHBIHI

Mtunzi ametumia tashbihi ili kufafanua zaidi anachokizungumzia. Ametumia baadhi ya tashbihi zifuatazo katika ubeti: ...**kama paka kiangaza** ...(kuangaliaangalia huku na huku-ub.76), ...**sauti menipendeza kama njiwa**...(sauti tamu-ub.164), ...**nyakanga huwa mkali kama vile pilipili** (mkali sana mfano wa pilipili-ub.427), ...**maneno kama haluwa yatokayo mdomoni** (maneno matamu-ub.1127) ...**mwanamke hujikaza mithali kamba na kuni** (hujibidiisha kufanya mambo-ub.1127), ...**ni mashujaa kama ing'aravyo taa**...(ufanisi wao huangaza kote-ub.1012), ...**laini kama hariri** (isiyo ngumu-ub.1053), ...**umevaa yako chanda kama pete kidoleni** (umeolewa na mume kufu yako-ub.1115), **upowe kama barafu** (utulie-ub.1177), **maneno kama haluwa** (maneno matamu-ub.1105).

4.2.3.2 SITIARI

Msanii ametumia sitiari kwa lengo la kuchora taswira ya kiulinganishi kati ya vitu viwili vilivyo na sifa sawia. Baadhi ya sitiari ambazo mtunzi ametumia katika tenzi ni: ...**mwanamume ni mtoto**...(mwanamume hulelewa kama mtoto-ub.1124), ...**ni chini ya taa yenu**...(naweza kuitika wito wenu wakati wowote-ub.1142), ...**mapenzi ni yako taa**...(mapenzi ndiyo yatakayomulika njia yenu-ub.1214), ...**mzigo huu ni wenu**... (jukumu la kutunza liko mikononi mwao-ub.278), ...**habari hizi nyeupe**... (habari dhahiri, zilizo wazi-ub.321), ...**mguu huu ni wenu**...(tumekuja kwa sababu yenu-ub.510), ...**lakini huwa ni bubu, pale atafanya nini**... (hana ruhusa ya kuzungumza-ub.750), ...**ulimi ni maaluni**...(umejaa laana-ub.1103), ...**umevaa yako chanda**...(umepata kufu yako-ub.1115), ...**hao ni jengo la Shamu lililojengwa zamani** (ni wazee walio na hekima-ub.1165), ...**wazazi ni makuhani** (wanafahamu mambo vizuri-ub.1013).

4.2.3.3 JAZANDA

Mtunzi ametumia jazanda kwa lengo la kufumba ujumbe kwa sababu ya kuonyesha adabu katika kazi. Ametumia baadhi ya jazanda zifuatazo: ...**mekuja taka kujenga**...(tunataka kujenga uhusiano wa ndoa-ub.142), ...**nimetumwa kuja funga** (kumzuia mwingine atakayekuwa na nia ya kuposa kutofanya hivyo-ub.142) ...**maji yafika shingoni**...(subira imeanza kututoka-ub.306), ...**nituwe wangu mzigo, nilo nawo kifuani**...(nisikize nikwambie niliyo nayo moyoni-ub.256), ...**maji karibu tajaa na kufika ufukweni** (subira zinatuisha-ub.547), **ikikawia kujibu**...(majibu ya ubikira wa msichana yakikawia kutolewa-ub.615, 632), ...**ainowe yake fimbo, aupasi**

mtihani...(ajiandae kwa tendo la kujamiiana na afaulu-ub.629), ... **kila wanapoonana...**(kila wanapojamiiana-ub.682).

Bwana leo kalimbuwa
Mtama kaufunuwa
Kinuni kautifuwa
Mwana yuko hali gani...(653)

Somo huwasa watoto
Nasaha zake nzito
Wasitowe chao kito
Kwa vijana mitaani (ub.774).

...**kiambiwa hiyo dawa ya mke kiingiliwa ili asije umiya...**(dawa anayojipaka mwanamke kabla ya tendo la kujamiiana ili asiumie-ub.682), ... **wafanye ari, wangoje mali halali, papara lote la nini** (wangoje watapata mali yao halali katika ndoa-ub.784), **watakuja kukuchuma** (kutafuta mambo kwako-ub.1117).

Anwani ya *Utenzi wa Mwanakukuwa* ni fumbo na jazanda pia. Mtunzi anamtaka msomaji ausome utenzi ajionee jinsi kazi ya kumkuza mwana ilivyo ngumu yaani kwa ufupi anaonekana kusema kwamba, 'mwana kukua ni kazi!'. Mamake Mwanakukuwa analia kwa furaha kumwona mtoto aliyemkosesha usingizi tangu kuchukua mimba yake hadi kumlea akafikia alipofikia (ub.1023, 1024, 1025). Tulioyasema yamemulikwa na mtunzi katika (ub.1024) anaposema:

Yote alomtendeya
Na namna alivyolea
Hata kufika Kukuwa
Leo kuwa mke ndani

4.2.3.4 METHALI

Mtunzi amebadilisha muundo wa methali kisintaksia na kutumia maneno yasiyo katika hali ya kawaida kimatumizi katika methali alizotumia. Amezitumia kwa lengo la kufunza, kubeza na kuyatilia mkazo anayoyasema: ...**maneno mema hamkosi kumtowa nyoka pangoni**...(maneno matamu humtoa nyoka pangoni-ub.731), ...**na hasira za mkizi anapojirusha pwani**...(hasira za mkizi furaha ya mvuvi-ub.1042), ...**mwenyewe kajitakiya sasa silie na nani**...(msiba wa kujitakia hauna kilio-ub. 879), ...**mla ni mla leo...mla jana kala nini** (ub.1052), ...**ukatokea mkasa wa Musa na Firauni** (ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni-ub.961), ...**yaliyopita si ndwele hatuyajuwi ya kale**...(yaliyopita si ndwele tugange yajayo-ub.930), **mpende akupendaye** (ub.1216),... **miadi ni kitu deni** (ahadi ni deni-ub.962).

4.2.3.5 MASWALI YA BALAGHA

Maswali yote ya balagha katika utenzi huu yametokea katika kibwagizo na msanii ameyatumia kuonyesha hali ya wasiwasi au kutofahamu aliyo nayo mhusika: ...**vioja hivi vya nini?** (ub.38), ...**unaumwa au nini?** (ub.122), **jamaa huyo ni nani?** (ub.136), ...**haraka hizi za nini?** (ub.239), ...**mtoto yu hali gani?** (ub.57), ...**hiki ni kizee gani?** (ub.72), ...**tena unataka nini?** (ub.1177) ...**wameona walotaka, sasa wangojeya nini?** (ub.685), ...**sijui nifanye nini?** (ub.33), ...**wewe nani wewe nani?** (ub.49), ...**Kukuwa analiani?**

(ub.610), ...papara lote la nini? (ub.784) ...makusudi yake nini? (ub.800), jama ninyi watu gani? (ub. 935), ...mwari atakuwa nani? (ub.837), ...Angojee hata lini? (ub.838).

4.2.3.6 *TASFIDA*

Mtunzi ametumia baadhi ya tasfida zifuatazo katika utenzi kwa lengo la kuonyesha adabu katika kazi: ...**pia na tumbo la kwenda, nikaendeya chooni...**(kuhara-ub.121), ...**kila wanapoonana** ...(kila wanapojamiiana-ub.683), ...**wasitowe chao kito kwa vijana mitaani** (wasilale na vijana kabla ya ndoa-ub.774), ...**wangoje mali halali...** (wangoje waolewe ndipo wajamiiane katika ndoa-ub.784), ... **ya mke kiingiliwa ili asije umiya...**(mke akijaamiana na mumewe asije umiya-ub.683).

4.2.3.7 *TABAINI*

Mtunzi ametumia tabaini kwa sababu ya kusisitiza anachosema. Baadhi ya tabaini alizotumia mtunzi ni: ...si yeye wala si mimi... (ub.217), ...makubwa si kalili...(ub.654), ...si nyingi si za mafumbo...(ub.1011), ... sicheki wala sioni...(ub. 295), ...si vizee si vijana...(ub.745).

4.2.3.8 *MISEMO*

Mtunzi ametumia baadhi ya misemo ifuatayo ili kuitilia kazi yake nakshi: ...**ala kuli hali...** (kwa vyovyote vile-ub. 40), ...**kwa udi na ambari...** (kwa bidii sana-ub. 63), ...**umetia fora...**(umefana-ub. 275), ...**kwa furaha na bashasha** (kwa starehe na uchangamfu-ub. 328), ...**pigwa butwaa** (shangaa-ub. 902), ...**ule mrututu...** (umezee machungu-ub.1136), ...**msitupake matope** (msituaibishe-ub. 336), ...**mtoto toka tokeni...** (mtoto wa kusifika-ub. 208), ...**kwa marefu na mapana...**(kwa yoyote yale-ub.500),...**tumejifunga mkaja...**(tumeleta ada atozwayo anayechumbia ili kupewa watu

wa upande wa kuukeni wa anayechumbiwa-ub.557), ...**miwani kainamisha**...(macho akainamisha-ub.124), **maneno...tuyamezee rohani** (maneno tuyanyamazie-ub.131^f), ...**wenda zake arijojo**...(kujirusha huku na huku-ub.675), ...**mwana jaha na jamali**.. (mtoto mzuri na mwenye heshima-ub.654), ...**tunu na tamasha**... (sherehe na zawadi kemkem-ub.1125), **najikaza kisabuni** (jitahidi hata kama unaumia-ub.130), **mguu huu ni wako** (nimekuja kwako kwa shida fulani-ub.143), **nimetumwa kuja funga** (nimetumwa kuja kumzuia atakayeleta posa asilete-ub.142), **naapa kula yamini** (kula kiapo-ub.1175), **kuwa na roho kunjufu** (kuwa na uchangamfu wa roho-ub. 1177), **binadamu wana inda** (binadamu wana hiana-ub.1184).

4.2.3.9 *VISAWE*

Mtunzi ametumia visawe vingi katika utenzi kama tutakavyoona katika mifano tutakayotoa kwa lengo la kuepuka kujirudiarudia: Neno pesa (ub.257) lina visawe vingi katika utenzi. Visawe hivyo vinaonyesha ukwasi wa lugha alionao mtunzi mbali na kuepuka urudijirudijaji wa neno moja. Neno pesa lina visawe vifuatavyo katika utenzi: fulusi (ub.238), sarafu (ub.1163), kifungua mlango (ub. 720), kata (ub. 432), rupia (ub.338), fedha (ub.448), visero (ub.387), mapeni (ub.776).

Visawe vya neno udaku (ub.906), umbeya (ub.842), sabasi (ub.1092). Visawe vya jina la Mtume Mohammed (ub.1072): Amini (ub. 700), Mmaka (ub. 377). Visawe vya neno somo (ub.383), kungwi (ub.663). Visawe vya neno bi. arusi (ub.516), mtoto (ub.741), kanono (ub.773), kitoto (ub.399), kipenzi (ub.975), mwana (ub.1018), nana (ub. 1018), huru-l-ayni (ub.1020) tiba (1096). Mtunzi ametumia visawe vikifuatana katika baadhi ya mishororo katika beti. Usanii huu ni wa hali ya juu katika fasihi kwasababu unasaidia

kutilia kazi nakshi na kusesitiza ujumbe licha ya kutochosha akili za wasomaji. Baadhi ya visawe hivyo katika utenzi ni: Bila taabu na matata (ub.1226), enyi **watoto wanangu** (1208), **mapenzi** mengi **mahaba** (1152), **upes**i na **himahima** (ub.970), mwende **mbio himahima** (ub.960), **wang'aa wametameta** (ub.383), **harufu vumba** (ub.98), kwa **furaha** na **bashasha** (ub.91), **mbiombio** kwa **haraka** (ub.161), **kitoto kanono** (ub.403), kwa **khushui** na **adabu** (ub.418), kwa **maringo** na **matao** (ub.153), **akatoka kaondoka** (ub. 287), hana **haya hana soni** (ub.76).

4.2.3.10 *TANAKALI SAUTI*

Mtunzi ametumia tanakali sauti kuchora picha halisi ya milio inayoigwa. Baadhi ya tanakali sauti zifuatazo zimetumiwa katika utenzi: Jikoni nahangaika kurukuru kakaka (mtunzi amebadilisha muundo wa neno kukuru-ub.68), hagongwa wangu mlango ...ngo, (ub.70), ... kaja nyatu nyatu (ub.87), akihema kikiki (ub.202), hufunikwa gubigubi (ub.826), kujaa watu pomoni (ub.1095), kakara na kukuruku, ipuwa weka mekoni (ub. 563), wakangiya tubwi ndani (ub.655), wanakwenda kurukuru (ub.532), mayai kem-kemu (ub.561), wanawake kutukutu (ub.687), akisikia kakara (ub.716), ..na mikufu paku paku (ub.751) ...ukashikwa kutukutu (ub.768), ..huwa kukuru kakaka (ub.873).

4.2.3.11 *NIDAA*

Mtunzi ametumia nidaa zifuatazo kuonyesha hali za furaha, mshangao na bezo : Wasemaje baba mke! (ub.169), .. mahari kiasi gani! (ub.326), maskini! Aolewa (ub.378), .. kitanda kiko tayari! (ub. 549), ..kitanda cha samadari! (ub.549), vya msaji na vizito! (ub.550), ..mḥukwa!! mbukwa!! jamani (ub.766), mimi mnaniona! (ub.934), Akaguna! Nambieni (ub.933), Hatumsomei mtu! (ub.969).

4.2.3.12 *TAHARUKI*

Utenzi unaanza kwa taharuki; mama ana wasiwasi hapati usingizi wala hali mpaka akakondeana. Wasiwasi wa baba haudhihiriki waziwazi ingawa anao. Hali zao zinatokana na kuwepo kwa Mwanakukuwa mle nyumbani baada ya kutoka unyagoni. Mioyo yao inataharuki hawajui litakalomfika mwanamwari wao, iwapo atampata mchumba au la (ub. 28-45). Wageni waliofika nyumbani kwa visingizio mbalimbali walimwacha mamake Kukuwa katika hali ya taharuki. Alibaini kuwa si bure, faraji ilikuwa inawakabili katika siku za usoni (ub.81-82).

Baada ya washenga kuleta habari za posa baba aliwaambia warudi watulie, wataandikiwa barua ndipo waje kuposa (ub.198) kwa sababu alihitaji kuwashirikisha wazee wake katika shughuli hizi. Wakati huo ulikuwa wa taharuki kwa upande wa mume hadi babake (babake mume) akaandika barua ya kupeleka posa baada ya miezi sita. Posa ilipokelewa lakini kukazuka kikwazo kingine. Walipewa muda wa miaka miwili kungoja ndipo walete mahari. Wakati huu wote uliwatupa katika taharuki lakini hawakuustahimili muda mrefu waliopewa kungoja; walirudi baada ya mwaka mmoja wakitaka kujua kiasi cha mahari na siku ya kuileta. Mgogoro unatokea kidogo lakini wanaafikiana.

Tukio lingine linaloibua taharuki ni la kuibiwa kwa msichana. Haijulikani iwapo arusi itajibu au la. Mama, bibi na shangazi wanaomba dua mfululizo. Watu wa kuukeni wako kimya huku wameinamisha vichwa kwa kutojua iwapo aibu itaingia kwao au watafumbuliwa nyuso (ub.612).

4.2.3.13 *USAMBAMBA*

Baadhi ya maneno yanayoleta dhana ya usambamba katika yamekusudiwa kusesitiza ujumbe kwa kinyume : ...watu wote **kuumeni, kuukeni...**(ub.199), baba **mke** baba **mume** (ub.416), mimi **bibi** wewe **babu** (ub.447), kina **mama**, kina **baba** (ub.474), **mkubwa** hadi **mdogo** (ub.1211), tuyatafute yenye **kheri**, tuyatupe yenye **shari** (ub.1227), kina **dada**, kina **kaka** (ub.343), **waume** na **wanawake** (ub.612), ...**nje, ndani**, upenuni (ub.65), **watoto** hadi **vizee** (ub.965), **usiku** pia **mchana** (ub.683).

4.2.3.14 *TAKRIRI*

Takriri zinatokea katika viwango vya maneno kwa sababu ya kusesitiza ujumbe na mizani kwa sababu ya mahadhi na mdundo wa kishairi. Takriri maneno: ...hewalla, bwana hewalla, hewalla (ub.262), sirisiri (ub. 82), purushani purushani (ub.177) ...hamkani hamkani (ub.56), njoo ndani, njoo ndani (ub.137), karibu bwana, karibu bwana (ub.141), akarudi himahima (ub.160), mote mote majumbani (ub.166), kaondoka huyohuyo (ub.176), karibuni karibuni (ub.230).

Takriri za sauti za irabu na konsonanti zimetokea mwanzoni mwa baadhi ya mishororo. Aina hizi za takriri zimetokea kwingi katika utenzi lakini tutanukuu mifano miwili peke yake:

Uyashike ya shariya

Usishike yaso njia

Uislamu tumi ya

Ushikamane na dini (ub.1120).

Watu kimaliza kula
Wapakwe halahala
Wasimulie chakula
Wakirudi majumbani (ub.830).

4.2.3.15 *ISHARA / TAASHIRA*

Mtunzi ametumia mbinu hii ili kuangazia mapema yatakayotokea na kupanua akili ya msomaji ili afikiri zaidi na kuweza kutathmini mambo. Watu wawili waliokuja kwa akina Mwanakukuwa kisirisiri walikuwa ni ishara kuwa faraji iliwakabili wazazi wake, hivi karibuni habari za posa zingelewa. Bw. arusi anapoenda kumwiba msichana usiku ili kujaribu ubikira wake, huonyeshwa kitambaa cheupe chenye kung'aa, ishara ya kwamba msichana ni mchanga asiyejua mwanamume. Mwanamume huyo mziwanda hupashwa mambo yote anayofaa kujua na kutarajiwa kuinowa fimbo yake ili aupasi mtihani (ub.629). Ishara kuwa arusi imejibu huwa vigelegele (ub.638). Watu huja mbio mbio kutazama kizinda, wote wakafurahia kwa vigelegele (ub.638-641), kulia kwa Mwanakukuwa pia ni ishara kwamba alikuwa bikira kwa sababu alikuwa anaumwa (ub.636).

4.2.3.16 *TAURIA / KITANZA NDIMI*

Katika utenzi, baadhi ya beti zina matumizi ya tauria kwa sababu za kuboresha matamshi:

...Maskini **huyo** somo

Somo huyo mwanamomo

Kwa kila **jambo** huwamo...(ub.877)

...Mwanangu **Mwanakukuwa**

Mkubwa umeshakuwa

Kwa mumeo utakuwa (ub.1106)

4.2.3.17 MBINU REJESHI

Mtunzi ametumia mbinu hii kwa lengo la kufafanua mambo yasiyofahamika na wahusika. Mjombake Mwanakukuwa anawaambia wajumbe waliotumwa kutoka kuumeni kuwa mahari ni kitu cha hiari na watu wanaweza kupatana katika mazungumzo hayo. Mjomba anawataja Mama Hawaa na Bi. Khadija, anasema kuwa Adamu hakuyatoa mahari ya Mama Hawaa wala Bi. Khadija hakuyataja mahari. Mjomba anahitimisha kwa kusema kwamba hao wawili ndio vigezo vya jamii, wamepewa kama funzo lao. Urejeshi huu ulikusudiwa kusuluhisha mzozo iwapo ungetokea kwa kurejelea misingi iliyowekwa na ndoa mbili za kwanza kuhusu mahari.

Mbinu rejeshi imetumiwa pia mamake Mwanakukuwa anapaturejesha nyuma kutukumbusha Kukuwa alipozaliwa, alivyomlea hadi sasa amepata mume, haikuwa kazi rahisi (ub.1023-1025). Mtunzi anatutajia kuwa bi. arusi hulia anapokumbuka mazoea tangu tumboni (ub.1041).

4.2.3.18 KINAYA

Kinaya kimekusudiwa kuficha ukweli yaani mambo yanazungumzwa au kufanywa kinyume cha matarajio. Mamake Mwanakukuwa anasema maneno yafuatayo kwa mmbeya aliyekuwa amefika nyumbani kwake kwa nia ya kumwona Mwanakukuwa lakini akasingizia kuwa alitamani kumjulia hali mamake Kukuwa. Mama hakukusudia kumwambia aliyomwambia wala si ati alimsikitikia kwa kujitia katika jua kali. Anamwambia:

Msalkheri kimwana
Mbona mekuja mchana
Jua kali naliona
Umejitia njiani (ub.53)

Majibu ya mmbeya yakawa vile vile ya kinaya, alimjibu:

Nakutamani ndu yangu
Mbona babu huji kwangu
Vibaya hivyo mwenzangu
Si haki ya ujirani (ub.55).

4.2.3.19 UBASHIRI

Mbinu hii hutumiwa na mtunzi kama kiona mbali. Mamake Mwanakukuwa aliwaza kuwa jambo la heri lilikuwa njiani baada ya watu wawili kuja kwake kisirisiri mfululizo. Aliona kuwa faraji iliwakabili huko siku za usoni (ub.81-84). Hawakukaa siku nyingi, wakatokea washenga kuja kumposa Mwanakukuwa.

4.2.3.20 TASWIRA

Utenzi wa Mwanakukuwa ni taswira ya arusi za Kiswahili. Mtunzi amezeleza kinagaubaga na amefanikiwa kuchora picha ya arusi hizo akilini mwa msomaji. Kila hatua za arusi hizo, kuanzia kwa vyakula vinavyoandaliwa, mapambo ya bi. arusi, mila na desturi zinazoambatana na arusi hizo na jinsi sherehe zenyewe zinavyoendeshwa yote yameelezwa kwa kina.

4.2.3.21 CHUKU

Mtunzi ametumia chuku ili kuchekesha au kutilia mkazo ujumbe. Baadhi ya chuku ambazo mtunzi ametumia katika utenzi ni: ...mwali **amejaa ndani** (yuko ndani, hatoki

wala kuonekana nje-ub.36), azma kumpukusa wake **huru-l-ayni** (kumtuza mpenzi wake-ub.1020), ...nyumba huku yafukuta **uzuri kushika kuta** (yawaka ndani na uzuri ukashika ukuta-ub.814), ...kwa masiniya ya shaba...**ukiziona washiba** (kushiba kwa kuona tu sahani iliyo na chakula-ub.825), ...sifaze zimezagaa, **zimejaa majumbani** (sifa kujaa majumbani-ub.147), ...kwa **sauti za urembo zatoka ndani ya tumbo...** (sauti kutoka ndani ya tumbo badala ya moyoni-ub.855).

4.2.3.22 TASHIHISI / UHUISHAJI

Mtunzi ametumia tashihisi zifuatazo katika utenzi kwa sababu ya kumfanya msomaji awe na mguso wa kihisia kuhusu analozungumzia: ...roho huona makubwa..(ub.30), ...nyumba huku yafukuta, uzuri kushika kuta (ub.814), Huko nako limeuma lelemama linasema...(ub.706), ...usingizi hutoka..(ub.33), ...moyo ukaona raha..(ub.50),... asumini na vikuba ..shingo yake ilibeba (ub.891), Dunia ina hadaa, mara moja hukuvaa (ub.946), ...nalo fundo lilowakaa rohoni (ub.315).

4.2.3.23 KEJELI

Mtunzi ametumia kejeli kwa lengo la kuwachekesha wasomaji wake kwa sababu ni yeye tu na wasomaji wake ambao hujua ukweli wa jambo linalosemwa. Bi. kizee alipokwenda kwa akina Kukuwa, mama anasema: ...dirishani hachungiya hiki ni kizee gani? Maneno anayotumia mama kueleza kuja kwa bi. kizee ni ya kejeli (ub72-80). Maneno aliyoyasema mamake Kukuwa kumhusu mwanamke aliyekuja kwake kwa kisingizio cha kumjulua hali huku akitaka kumwona Kukuwa yanaonyesha kejeli (ub.56) Katika beti (879-880), mtunzi anamkejeli somo. Anasema kwamba somo anaenda kwa kujisukuma huku kiuno kimeinama kwa kazi ambazo alijitakia mwenyewe. Anazifanya mwenyewe

kwa hiari yake japo mizigo hiyo si yake. Mtunzi anauliza, aingilia kwa nini? Mtunzi anawakejeli wambeya baada ya sherehe za arusi kujibu. Anauliza wanalongojea kwa sababu washaona walilolitaka (ub.685)

4.2.3.24 SADFA

Babake Kukuwa alipopokea habari za posa ya mwanawe, alienda kwa wakweze kuwajulisha habari hizo mara tu akaelezwa kuwa alikuwa ametajwa siku hiyo na ikasadifu kuwa ndiyo siku aliyotokea, (ub.272):

Leo hivi nakutaja
Kwa siku nyingi hukuja
Kutweleza zako haja
Tutende namna gani.

Ilisadifu kuwa wazazi wa Mwanakukuwa walifika wote kwa wazazi wao (wakweze babake) kupeleka ujumbe wa posa ya Kukuwa (ub.288). Ilisadifu kuwa mamake Kukuwa alikuwa na wasia mrefu alioupanga kwa safu na akautumia kumuusia mwanawe (ub.1155).

4.2.3.25 TAABINI

Utenzi wa Mwanakukuwa ni taabini kwa sababu unasimulia kumhusu mamake Zaynab. Zaynab ni mtunzi wa utenzi wa mamake ambaye aliitwa Mwanakukuwa. Mtunzi anamtungia mamake aliyempenda, kumsifia na kumtukuza mno. Mama yake alifariki na kuzikwa nchi ya mbali alipokwenda ziara tukufu ya Hajj.

4.2.3.26 NYIMBO / NGOMA

Mtunzi ametumia nyimbo kwa sababu ya kuburudisha. Ametumia nyimbo mbalimbali ambazo zinaambatana na kila hatua ya arusi. Kila mmoja una umuhimu wake licha ya kuburudisha waliohudhuria sherehe hizo.

4.2.3.26.1 WIMBO WA CHENDA NAYE

Ni wimbo wa kupelekea kitu chochote cha mwari siku za arusi. Wimbo huu huimbiwa bi. arusi mahari yake yanapopelekwa kwao (ub.420-424) na bi. arusi akiwa amebebwa wakati wowote wa kupelekwa chooni. Kwa muda wa siku saba, bi. arusi huwa haendi chooni kwa miguu yake mwenyewe ila hubebwa mgongoni na somo (ub.420).

4.2.3.26.2 WIMBO WA CHEREKO

Chereko hutolewa pale masomo au manyakanga wanapoleta vitu vya mwari. Hupewa aliyekichukua kitu kile au kumchukua mwari yule kucheza naye wakati wa ngoma au kuimbwa nyimbo za arusi. Manyakanga hutoa sauti zao kwa pamoja kumfurahikia mtu yule aliyefanya kitendo kile. Kwa pamoja husema 'chereko, chereko somo' (ub.431).

4.2.3.26.3 NYIMBO ZA BATAANI

Nyimbo za kufurahisha, pengine huwa nyimbo zenye matusi au upuuzi. Huimbwa katika arusi za Kiswahili pande zote za mume na mke zinapobezana na kutaniana. (ub.428).

4.2.3.26.4 WIMBO WA SASAMBURA

Ni wimbo wa kunadia au kutangazia vitu vya mwari uwanjani, na watu wakivitazama vitu hivyo. Hutolewa kila kimoja kukionyesha na watu huku wakiimba, 'vitoweni tuvione' (ub.573).

4.2.3.26.5 TUMBUIZO

Ni ifyimbo zinazoimbwa maalum siku za arusi, za kumuwasa bi. arusi na bw. arusi juu ya mambo fulani (ub.676).

4.2.3.26.6 NGOMA YA LELEMAMA

Ngoma ambayo huchezwa na wanawake watupu. Wapigaji huwa wanaume. Wanawake hao husimama juu ya mabao na mikononi huwa mbiu, ambazo ni pembe za mbuzi. Hukamatwa mikono yote miwili (ub.473).

4.2.3.26.7 NGOMA YA BOMU

Ni ngoma kama lelemama, ya wanawake watupu, na vile vile hukamata mbiu mikononi, ila bomu huchezwa chini na wachezao huwa wamevalia nguo za mataifa mbalimbali zenye kupendeza. Hata nguo za kiume huvaliwa (ub.473).

4.2.3.26.8 NGOMA ZA UROMBONI

Hizi ni ngonia zinazochezwa wanawari wanapokuwa uromboni wanapofundishwa mambo ya utamaduni na unyumba ili watakapoozwa wayafanye waliofundishwa katika ndoa zao. (ub.10, 13, 16).

4.3 WAHUSIKA

4.3.1 MAMAKE KUKUWA

Hajatajwa kwa jina. Katika utenzi anarejelewa kama mamake Kukuwa. Mamake Kukuwa ni mzazi stadi katika ulezi kwani alikabiliwa na kazi ngumu ya kumtunza mwanawe baada ya kurudi nyumbani kutoka unyagoni. Kazi hiyo ilikabiliwa na changamoto na wasiwasi mwingi, huku mama akiwa anatamani aje mtu amwoze Kukuwa (ub.27, 28).

Mama huyu ni mchache wa subira. Alikuwa na wasiwasi mwingi kumhusu Mwanakukuwa mwenyewe akikiri kuwa usingizi ulimpaa pindi alipofika kitandani kwa kuwaza na kuwazua kuhusu hatma ya mwanawe; iwapo angetokea wa kumposa au la (ub.33, 36).

Ni mcha Mungu kwa hivyo hakuacha kumwomba mwanawe dua za kumpata mume (ub.26). Siku ilipowadia ya Kukuwa kuibiwa, bibi na mama walilia Rabi Mola awauni (ub.597), huku wakiomboleza, madua hawakusaza (ub.598). Arusi ilipojibu, akamshukuru Manani kwa utuo na akasema kuwa angepata naumu siku hiyo (ub.646,647). Mama anampa Kukuwa wasia wa mwisho kabla mumewe hajamchukua. Anamwomba dua na kumuusia ashike dini yake, nguzo tano za dini ya kiislamu, amjuwe na kumwabudu Rahmani (ub.1157, 1170, 1171).

Bila shaka mama huyu alimfunza mwanawe kazi alipotoka unyagoni. Hakumdekeza licha ya kutueleza kwamba ndiye alikuwa mwanawe wa pekee (ub.35). Mama alimfunza ushoni na akamzoesha kazi za nyumba (ub.5). Kukuwa alifunzwa charhani, ususi wa mikeka na ususi wa vichwa; wanawake walimiminika kwao nyumbani kusukwa nywele (ub.6, 7). Kukuwa alimsaidia mamake jikoni pia (ub.69). Katika wasia wake kwa mwanawe, mama anamwomba kutosahau au kudharau aliyomfunza; ususi na cherhani (ub.1166).

Ni mnyenyekevu kwa mumewe. Hili ladhihirika kwa jinsi anavyompokea mumewe anaporudi nyumbani na kumshughulikia kwa kumpokea koti, kumvua kofia, kanzu na

shati (ub.88). Baadaye alimtandikia mkeka na kumwekea sinia (ub.89), akaanza kumlisha huku akimwondoshea miba isimwingie kooni. Baada ya kula wanapoingia chumbani anamkanda miguuni na kumpapasa kichwa huku akimweleza yaliyojiri alipokuwa ametoka (ub.90-106). Taswira hii inatukumbusha *Utenzi wa Mwanakupona* ambao umeacha kubwa athari katika fasihi. Watunzi waliokuja baada yake walitunga kuhusu maudhui yayo hayo. Jamii ya wanawake wa Uswahilini iliitikia vizuri wito huu na kuugeuza utungo huu kuwa badala ya asasi ya kale ya unyago ambayo ilikuwa inaanza kutoweka. Katika ubeti wa (95) Mwanakupona anasema:

Somani mite ya nganu
mutii waume zenu
musipatwe na zitunu
za akhera na dunia.

Mamake Kukuwa anamuusia mwanawe kumtunza mumewe (ub.1159-1164), anawausia watoto wa leo pia kuwatunza waume wao (ub.100-105).

Ni mwanamke aliye na hekima pamoja na heshima. Aliwatahadharisha wazee kutofanya mambo kwa pupa bila kumhusisha somo wa Kukuwa kwa sababu yeye ndiye aliyetakiwa kushika usukani wakati wa arusi (ub.369-372). Kabla hajawaambia wazee, haya aliomba kusikizwa hata ingawa lile angesema halingetiwa maanani (ub.366-368).

4.3.2 BABAKE MWANAKUKUWA

Baba huyu ni mtulivu na mwenye subira. Mamake Kukuwa anapoonekana kukosa tumaini la mwana wao kuposwa, mumewe anamwomba kutulia. Alimuusia aache

kutapatapa (ub.37-44) kwani yeye mwenyewe alijikaza asiwe na la kufanya huku akisubiri Mungu awape fungu lao. Isitoshe, alimkumbusha kuwa mwanawe hakuchina wala hakuwa na utukutu na hakutajwa na watu kwa ubaya kwa hivyo mamake Kukuwa hakuwa na sababu za kuwa na hofu (ub.115).

Babake Kukuwa anathamini mila na desturi za utamaduni wao. Mshenga anapofika kwake kuleta habari za posa, alitarajia kujibiwa papo hapo lakini baba akamjibu kuwa katika mila zao, hathubutu kujibu lolote hadi awaarifu wazee (ub.170-171). Baba anaiendesha arusi ya Kukuwa kwa misingi ya mila zao: Anamwachia babake na wazee kutoa uamuzi juu ya posa, mahari na shughuli za arusi ya mwanawe.

Ni mwenye kuwa na tahadhari. Mshenga anapokuja na habari za kutaka ndoa ya haraka, anasema kuwa hana haja ya papara maanake mwanawe hakuchina (ub.184). Anamwambia mkewe kwamba awaarifu kina mama walosabiki usoni wantazame mchumba kama hatoyumbayumba yaani bilisi hatomkumba akachafukia njiani (ub.187-190, 199). Baba anasema kuwa mambo sharti yatazamwe, wasiyavamie yakaleta shida.

Ni msiri kwa sababu, baada ya kukubali posa ile, alimtahadharisha mshenga kutoyasema kwa majirani kwani wangeanza kuyachambua na watu mahasidi wangetaka kuyafisidi. Anamwambia kuwa maneno hayo yasimdondoke, ayamezee moyoni (ub.172, 174, 175). Babake Kukuwa alipotoka kusali mwendo wa saa mbili hivi alimwita mkewe akamwambia kuna mnong'ono kuwa kuna watu watakaokuja kumposa mwana wao. Baada ya kumpasha habari hizi, alimwambia asizihubiri, wayamezee roho, wasiwajulishe hata wazazi wao kwa sababu wangeyafumbua (ub.131-133).

Ni mcha Mungu kwa sababu tunaelezwa kuwa alikuwa akienda kusali (ub.120). Kukuwa alipokuwa nyumbani kabla ya posa, mamake akiwa na wasiwasi, baba alimwambia atulie kwani mpaji ni Mungu. Alimtaka wasubiri kwani wangepewa fungu lao na akatumia maneno yaliyojifunga katika dini kumuusia (ub.38-43).

4.3.3 MWANAKUKUWA

Mwanakukuwa ni mhusika mkuu katika utenzi. Ni mtoto wa pekee kwa mama na babake (ub.35). Mwanakukuwa ni mhusika bubu, hasemi lolote katika utenzi isipokuwa anapoitikia wasia aliopewa na makungwi, somo na mamake (ub.1175). Mtunzi amemjenga kupitia wahusika wengine.

Mamake anasema kwamba si mshindani (ub.5), alimzoesha kazi za nyumba, akamfunza charhani, ushoni, upishi na ususi wa mikeka na vichwa. Kukuwa alimsaidia mamake kazi za jikoni baada ya kutoka unyagoni (ub.6, 7, 150). Kukuwa alikuwa mwenye haya nyingi kwani mgeni alipobisha kwao, alikimbia kwenda chumbani ili asimpate pale. Mtunzi anasema kuwa Bi. kizee alipobisha Kukuwa alikuwa akikuna nazi, mara tu aliposikia ile hodi, akatoka mbio hadi chumbani (ub.71). Wakati mwingine tena, mgeni mwingine alipofika pale nyumbani, Kukuwa aliingia chumbani (ub.ub.48).

Kukuwa ni mtulivu na mwenye hulka nzuri. Babake Kukuwa akizungumza na mkewe baada ya kutoka msikitini alimwambia kuwa mwana wao hakuchina, hakuwa na utukutu wala hakutajwa na watu kwa ubaya (ub.115). Kukuwa ni mtulivu. Hatoki nje, hushinda nyumbani kutwa kucha kama anavyosema babake (ub.116). Mshenga anayamulika haya pia anaposema kwamba watu wamezipekua sifa zake na hazina ila zozote, sifa zake

zimejaa majumbani (ub.146-147). Tabia zake nzuri ambazo hata wanajamii wote walikuwa washazitambua ndizo zilipelekea kuposwa kwake na hatimaye kujibu kwa arusi yake.

Ni mcha Mungu. Bi. Mrashi alipokwenda kwao kisirisiri kwa nia ya kumwona, hakufanikiwa lakini aliisikia tu sauti yake. Mshenga anasema kuwa, Bi. Mrashi alimsikia Kukuwa akimweleza mamake kuwa anakwenda chooni kutawadha ili aje asali (ub.162,163).

4.3.4 BABU YAKE MWANAKUKUWA

Huyu ni baba mzaa babake Kukuwa. Ndiye mkuruba au aliye na jawabu la kila jambo nyumbani. Washenga walipokuja kutaka kujua thamani ya mahari, aliachiwa yeye kutoa uamuzi. Aliwaeleza kuwa wangoje miaka miwili ndipo waje kujua kiasi cha mahari (ub.245, 259). Babu ndiye alitoa uamuzi kuwa walipe rupia alfeni kama mahari (ub.338).

4.3.5 SOMO / MANYAKANGA / MAKUNGWI

Somo ni mwanamke anayewafunza wasichana mambo ya unyumba wakiwa unyagoni. Ni mtu muhimu sana katika arusi za Kiswahili. Wazee wanapokutana na kuanza kupanga arusi, mamake Kukuwa anawatahadharisha kuwa wasianze lolote bila kumhusisha somo kwa sababu yeye ndiye mshika usukani katika arusi kwa hivyo wampashe habari hizo kisha wamsubiri (ub.369-372).

Maneno ya mama yanatukumbusha maneno ya Cheusi mamake Bahati katika riwaya ya *Kiu* ya Mohammed S. Mohammed. Idi alipokuja kutangaza arusi kati yake na Bahati,

mamake aliomba apewe nafasi ya maandalizi. Alimweleza kwamba kuna somo wa Bahati, (Bi. Mvita) aliyekuwa mbali na ambaye alifaa kuhudhuria arusi hiyo kwa sababu alimtaabikia sana Bahati alipovunja ungo. Bi. Mvita ndiye alishika usukani katika arusi ya Bahati. Hivi visa viwili ni ithibati tosha kuwa arusi za Kiswahili huendeshwa na somo.

Ni mwelekezi wa arusi. Anapopokea habari za kuposwa kwa Kukuwa anaupanga unyago kuingia kazini (ub.379, 383). Somo ndiye msimamizi wa kila shughuli arusini. Anashughulikia na kusimamia upambaji wa bi. arusi kama vile kumwogesha, kumfukiza manukato, kumpeleka chooni, kumpaka wanja, hina na kumtia mapambo mbali mbali. Somo pia humbeba mgongoni akimtoa ndani na pia kumwingiza anapohitajika. Somo pia huendesha shughuli za kutekeleza mila za Waswahili katika arusi kama vile kumtayarisha bi. arusi kwa shughuli za 'kuibiwa', kuvunja mayai mlangoni ili bi. arusi ayaruke na nyinginezo. Ni mkali kwani mtunzi anatwambia kuwa ukali ni sifa yake (ub.933).

Somo ni mcha Mungu. Alipopata habari za posa ya Kukuwa alisema kuwa dua zake alizokuwa akiziomba na kusali zimepaa (ub.378). Mwanamwari alipokuwa anapitia hatua zote za arusi, alikuwa akisali. Somo alimuusia Kukuwa ashike nguzo za kiislamu na ashike dini (ub.1003). Anasema kwamba Kukuwa aeuliwe na kuzunguliwa na walimu wanaojua wamsomee Hal-badri, Yasini na Kul-huwa ili aepuke husuda (ub.967-971).

Manyakanga na makungwi ni wanawake wanaofanya kazi unyagoni. Manyakanga humsaidia somo katika shughuli za arusi, humpamba bi. arusi, husaidia kumbeba, kumuusia na kushiriki katika mila zinazotekelezwa arusini. Manyakanga na makungwi

hufanya kazi chini ya somo na kutekeleza amri zake anapozitoa. Huwa wasaidizi wa somo katika arusi kwa sababu yeye ndiye huwapangia na kuwapa kazi.

4.3.6 WAHUSIKA WA KIKE

Hawa ndio wahusika walioutawala utenzi mzima. Wamesawiriwa kama wambeya. Mwanakukuwa alipotoka unyagoni wanawake walipitapita kwao kwa visingizio mbalimbali huku wakiwa wameletwa pale kwa umbeya. Baadhi yao ni Bi. Mrashi na Bi.Kizee (ub.56, 79).

Babake Kukuwa anamtahadharisha mamake Kukuwa kutowahubiria watu kuhusu posa ya Mwanakukuwa. Mwanakukuwa anatahadharishwa dhidi ya marafiki mahasidi (ub.1111). Wanawake wamesawiriwa kama wasengenyaji. Mtunzi anatwambia ni ila ya mwanamke kutia domo wenzake (ub.881).

Wanawake katika utamaduni huu wanawaheshimu na kuwatumikia waume wao kwa misingi ya mila za Waswahili. Nafasi yao katika jamii ya Kiswahili ni muhimu sana kwa sababu wanaonekana kuwa wao ndio uti wa mgongo wa jamii. Wao ndio watekelezaji wa mambo yanayopangwa na wanaume kama tulivyoona jinsi walivyoendesha arusi ya Kukuwa. Ni watumishi wa waume wao pia.

Wanawake wana ushirika. Habari za posa zinapoletwa, baba anamwambia mama kuwaarifu kina mama waliosabiki kumtazama mchumba. Wanawake; wazee kwa wanawari wanashirikiana kuifanikisha arusi ya Mwanakukuwa. Hawana uhuru wa kujichagulia wachumba. Mila zao zinawadhulumu zinapotaribu ubikira wao ilhali ule wa

mwanamume haujaribiwi. Fedheha huingia katika ukoo wa msichana haswa kwa wazazi wake anapopatikana kuwa si bikira. Jambo ambalo kwa maoni yetu linaonyesha dhuluma ya mwanamke kwa sababu mwanamume anapopoteza ubikira hakuna anayepata kujua kwa hivyo hapewi nafasi sawa na mwanamke.

4.3.7 WANAJAMII

Hii ni jamii iliyo na ushirikiano wa pamoja. Walihudhuria arusi kwa wingi na kutoa huduma zao. Miongoni mwa wanajamii pia mna mahasidi, wachongezi na wambeya. Watoto katika jamii ni mali ya wanajamii. Wazazi hawawezi kufanya uamuzi wowote juu ya mtoto wao peke yao bila kuihusisha jamii. Wanajamii ni wakarimu na wanaweza kwenda kwa jirani wakitaka msaada na wakaupata. Wanaume hasa wazee ndio hutoa mwelekeo katika mambo yanayoihusu jamii na wanawake ndio watekelezaji. Ni jamii inayoshikilia na kuthamini mila na itikadi za zamani kuhusu ndoa.

Hawa ni wanajamii ambao wanathamini sana ndoa na hawazichukulii kimzaha. Mabinti na wavulana wao hawaachiliwi kuoa au kuolewa waliowachagua wao wenyewe. Kabla ya ndoa wazee wa pande zote wanachunguzana kwa kusudi la kutaka kujua anakooa au kuolewa mtoto wao. Babu na baba yake Mwanakukuwa hawakukubali posa tu haraka. Babu aliwapa washenga miaka miwili ya kungoja, labda wakiichunguza jamii ya mume. Baba naye akamwambia mamake Kukuwa awaariifu wanawake wenzake watazame mambo na wafike hata matemwe (kijiji kinachotazama mambo ya ndoa).

Hii ni jamii ya wahafidhina. Ni watu wanaoamini katika husuda za watu, nuksani na mashetani. Hali ambayo imesababisha kutoaminiana kati ya marafiki na majirani. Baba

hataki habari za posa zijulikane kwani huenda mahasidi wakayachambua na kuyatia nuksani. Mama na somo wanapomuusia Kukuwa wanamtahadharisha dhidi ya marafiki. Wanamwambia kuwa awaambae marafiki kwa sababu watamtia nuksani na kumtenga na mumewe. Nyumba wanayohamia maarusi pia inafukizwa mafusho, kutiwa ubani na dua kuombewa hapo kwa imani kuwa wanaondoa nuksani na kuzuia mahasidi.

Hii ni jamii ambayo inamkandamiza mwanamke. Hata hivyo hatuwezi kuchukua msimamo mkali na kuihukumu kwa sababu katika wakati ule wa kihistoria ukandamizaji huu ulisaidia sana katika kuhimili asasi ya ndoa na kuendeleza kitengo cha jamii. Mama anasema kwamba mwanamwali wa zamani hakutoka wala kuonekana, kila saa alikuwa ndani, hakisikiwa (ub.32). Awali katika utenzi babake alitueleza kuwa Kukuwa hatoki nje, jambo ambalo linatuonyesha kuwa mwanamwari wa Kiswahili hufungiwa sana.

Mila hizi zinafaa. Kumweka mtoto wa kike hivi ni jambo la busara na laweza kuzuia talaka ambazo zimekithiri katika kizazi hiki. Ndoa imekuwa asasi ambayo haiheshimiwi tena kwa sababu ya uozo wa jamii na kutohusisha wazazi katika uchaguzi wa wachumba. Kuolewa kwa msichana kwa mujibu wa utenzi kulitegemea sana tabia zake na hulka ya ukoo aliotoka. Ndoa hizo zilikuwa tofauti sana na za siku hizi ambazo misingi yake imejengeka kwenye kazi anayofanya mtu, sura, mali au pesa na hadhi aliyo nayo mtu katika jamii.

4.3.8 WAHUSIKA WADOGO

Hawa ni akina Shekhe aliyefungisha arusi, wazee, wachezaji ngoma, washenga, warombo, shihata aliyevunjia mayai mlangoni mwa Kukuwa, wanawari, majirani, baba

na mama mkwe, shangazi, vijana kutoka kuumeni waliohudhuria arusi na wengineo. Hawa wote walichangia katika shughuli za arusi na pia wanasaidia katika kuwajenga wahusika wakuu.

4.4 TONI

Utenzi wa Mwanakukuwa una toni inayotoa mausio kwa jamii haswa ya wanawake. Jamii inayozungumziwa ni jamii inayothamini mila, itikadi na dini yake. Toni ya dini imetawala utenzi mzima. Kila mhusika tunayekumbana naye ni mcha Mungu. Baba alimtuliza mama alipokuwa na wasiwasi wa kutoposwa kwa mwanawe akimkumbusha kuwa Mungu ndiye mtowaji (ub.42-43). Baba alikuwa ametoka kusali alipokuja nyumbani na fununu kuwa kuna watu watakaoleta habari za posa (ub.120).

Mama alianza kumwomba dua mwanawe pindi tu alipotoka unyagoni ili apate mume wa kumwoa (ub.26). Mama, shangazi na somo walikuwa na wasiwasi, roho juujuu wakimwomba Mwanakukuwa 'aupasi mtihani'. Arusi ilipojibu, mama alimshukuru Karimu, kwani Bi. Kukuwa alimfunua uso (ub.647-648). Mama anapompa Mwanakukuwa wosia wa mwisho ndipo amwache kwa mumewe, anamkumbusha kuishika yake dini, amwabudu na kumjua Rahmani (ub.1170) na kushika nguzo tano za dini ya kiislamu (ub.1171).

Mafunzo ya dini ni ya kimsingi sana katika hii jamii. Mama ndiye hutwikwa jukumu la kumfunza mwanawe pamoja na manyakanga, somo na makungwi anapoenda unyagoni. Somo aliumulika wosia uo huo wa mama alipomsisitizia Mwanakukuwa kuwa sala na

Kur-ani Tukufu ndiyo mihimili ya kuondosha husuda (ub.1001-1003). Alimtaka ashike nguzo tano na kuzihifadhi moyoni (ub.1003).

Siku sita baada ya mwanamwari 'kuibiwa' wanaume husoma maulidi na kuomba dua (ub.815-819). Nyumba wanayokwenda kuishi maarusi hufanyiwa dua maalum, Kulhuwa husomwa hapo na nyumba kutiwa ubani (ub.997-999). Mila zote katika arusi hutangulizwa kwa dua. Tumegundua kuwa dini, mila na itikadi za jamii za Kiswahili ni mambo yasiyoweza kutenganishwa. Imani yao katika dini na utamaduni wa kiislamu ni kubwa mno. Mtunzi mwenyewe anapouanza na kuutamatisha utenzi, anafanya hivyo kwa toni ya dini. Tamaa yake kubwa ni kuiona jamii ikintanguliza Rabi Mola katika mambo yao ya kila siku yakiwemo ndoa, ulezi wa watoto, ushirika na watu na mengineyo. Kumjua Mola humwepusha mtu na husuda, visirani na balaa nyingi. Yeye tu ndiye huwaauni wanadamu.

Toni ya wasia inadhihirika wazi katika utenzi. Kila mhusika katika utenzi ni mwingi wa mawaidha haswa yanayorejelea mila na itikadi za jamii. Wosia wao unamlenga mtoto wa kike. Mtunzi anakisihi kizazi cha sasa kuregea kwenye utamaduni, kuuthamini na kuuhiifadhi. Wanawari wanausiwa kuwatunza waume wao wanapoolewa.

Unyumba na ulezi wa mume hufunzwa unyagoni na wakati wa fungate kama anavyosema mtunzi katika beti za (874, 914). Wasia huwa mwingi wakati huo mpaka mwanamwari hulia (ub.901). Wakati wa arusi mwari hutakiwa kumfanyia mumewe aliyofunzwa hadharani palipo somo, makungwi na manyakanga (ub.911-923).

Mama alimuusia Kukuwa kumtunza mumewe, akamweleza kwa utuo jinsi atakavyoishi naye. (ub.1156-1172). Somo aidha alimuusia kumtunza mumewe na kumtahadharisha dhidi ya mashoga (ub.1105-1137).

Mamake Kukuwa aliwapa watoto wa leo wasia wa kuwatunza waume wao. Yeye mwenyewe alimtunza na kumdekeza mumewe (ub.100-105). Somo naye akawaasa watoto wasitowe vito vyao kwa vijana mitaani, wangoje mali halali wasiwe na papara (ub.774, 784).

Toni nyingine inayodhihirika kwa uzito ni ya nasaha ya kuhifadhi utamaduni. Katika mojawapo ya beti za kwanza utenzini, mtunzi anasema ameuandika utenzi makusudi usomwe na wajao watakaobahatika kujifunza ya zamani (ub.8). Msanii anawasihi watoto kuyashika aliyowausia. Wayatafute kwa sababu yanafaa kuigwa. Anasema kuwa mambo mengi huharibika kwa kutoshika yale mazuri ya zamani. Alidhamiria kuuandika na kuuwacha wasia huo ili watoto wasome na kuutamani (ub.1208-1212). Msanii anasema kwamba mila ni nyingi Unguja na zote zina msingi. Anamwambia msomaji aukumbuke utamaduni, katu asiusahau. Anadokeza kuwa wageni huutamani na kuwaendea majumbani wakitaka kuujuu (ub.1219-1223).

Mambo yanayohusu utamaduni yameangaziwa kwingi katika utenzi na msimamo wa mtunzi ni kuwa uhifadhiwe. Maneno ya mama kuwa wanawari wana kazi enzi hizo za zamani (ub.27) ni ithibati kuwa, mila na itikadi nyingi hazizingatiwi na ndipo mtunzi anawasihi wanajamii kuuzingatia na kuuhifadhi utamaduni huo unaoelekea kusahaulika.

Mamake Kukuwa anasema kwamba mwanamwali wa zamani alikuwa ndani kila saa, hakutoka wala kuonekana (ub.32). Babake anayamulika haya zaidi anaposema kwamba zamani mwanamke alokwisha zake (ub.65) alitafuta wanawari watakaoposwa majumbani (ub.62.63). Tunamshuhudia Bi. Mrashi akifanya kazi iyo hiyo utenzini. Baba na mamake Kukuwa walikuwa wakizungumza haya wanawake watatu walipofika mfululizo nyumbani kwao kwa sababu zisizobainika wakiwa na lengo la kumwona Kukuwa.

Wahusika ni sauti ya msanii, kupitia kwao hupitisha ujumbe wake kwa jamii. Wahusika katika utenzi wanatumia maneno kama zamani yalifanywa hivi, mila zetu zinasema hivi, utamaduni wetu.... na mengineyo. Ama kwa kweli hii ni sauti ya msanii, 'inaomboleza' kuanza kusahauliwa na kudharauliwa kwa mila na itikadi za zamani.

Mshenga anapoleta habari za posa, anasema kwamba sifa za Bi. Kukuwa zilipekuliwa na watu, zikapatikana hazina ila (ub.146). Tabia na mila zao za zamani zilichunguzwa na watu (ub.166). Baba anamwambia mshenga kuwa asiwe na haraka, mambo lazima yatazamwe kwa sababu ni mila zao kuwa wakati wa ndoa zao lazima hilo lifanyike (ub.191). Mshenga alipotaka jawabu la haraka baada ya kuleta habari za posa, babake Kukwa alimjibu kuwa katika mila zao hathubutu kusema lolote hadi wazee wa pande zote waitwe kuzungumza na kuitathamini posa (ub.170-171).

Kuanzia mwanzo hadi mwisho wa arusi, mila na itikadi zinazofungamana na arusi za Kiswahili zilizingatiwa katika arusi ya Mwanakukuwa. Mila na itikadi hizi hutekelezwa katika arusi kwa madhumuni ya kupunga mashetani na pepo wabaya na kuzuia mahasidi

na nuksani katika ndoa. Msanii anasema kwamba bw. arusi huenda kwa akina bi. arusi kutembelea kila jamaa wa mkewe akiwasalimia. Msanii anadokeza kuwa mila hiyo ilikuwapo wala hawakubagua, lao kubwa lilikuwa kujenga utamaduni (ub.870).

Toni nyingine inayotokea ni ya makaripio. Mtunzi anaonyesha kuchukizwa na umbeya. Anatumia maneno mazito ya kuwabeza na kuwakejeli anapowarejelea. Tutarejelea baadhi ya matukio katika utenzi yanayoonyesha udhia huu.

Maneno aliyosema mama kuhusu wanawake wawili waliokuja kwake yanaonyesha kuudhiwa na tabia ile. Alimkejeli mwanamke wa kwanza akamuuliza kwa nini alijitia njiani katika jua kali kuja kumwona (ub.53) Anatumia maneno ya dharau kuelezea juu yake: ‘...mbeya anaonyesha, mdomo unamwasha...’ (ub.56).

Mama anasema alikuja Bi. kizee baada ya mwanamke wa kwanza. Mama anasema hakujua la kusema, ... kama paka kiangaza’ (ub.76). Mama anasema kwamba Bi. kizee alidhania atakapoingia atamkuta mwanawe jikoni (ub.79). Alihizika, mabega yakaporomoka (ub.80). Baba anapopata habari za posa, anamweleza mshenga kuwa si vyema watu kuyajua waanze kuyachambua, kwa sababu halijawa, lisienee mtaani (ub.174). Anamtahadharisha mamake Kukuwa kutoyahubiri (ub.131) wala kuwaambia wazee wao kwani pengine watayafumbua (ub.133). Mshenga anapopata habari za posa, anasimulia kisa cha Bi. Mrashi aliyefika pale nyumbani kisirisiri kuja kumwona Kukuwa lakini hakumwona, alisikia tu sauti yake. Katika hizo heka heka alijigonga akaumia lakini hakulia, mtunzi anatwambia, ‘... anavojua umbea, Mrashi hawezekani... (ub.152).

Baba anapotoka kwa akina mama kuwapasha habari za posa ya Kukuwa, mama anataka kujua kwa nini amesawijika na kuonekana kuwa yuko taabani (ub.294). Baba anamwambia kuwa kila anayemwona anamwangalia. Anashuku kuwa huenda watu wamesikia walivyo wambeya (ub.296) wanayaacha yao, yao wayatakiyani? (ub.297).

Siku na wakati wa mama na somo kutoa zawadi kwa bi. arusi katika arusi za Kiswahili hutengwa. Wakati kama huo ulipofika katika arusi ya Kukuwa, mtunzi anasema kuwa umbeya huuma wakati huo, kila mmoja akitaka kujua ni vitu gani vilivyoletwa, wanavilinganisha na kukadiria aliyeenda hasara (ub.575, 578). Mtunzi anasema, unajua wanawake kila mtu ana lake, hapo amejia lake, umbeya na ushindani (ub.842).

Baada ya arusi kujibu, mtunzi anasema kuwa wambeya hutawanyika, wameona walotaka, sasa wangojea nini? (ub.685). hayo maneno ya mwisho yanaonyesha alivyochukizwa na umbeya. Maneno ya mtunzi kuwa ... huku wakisukumana wambeya wa mtaani... (ub.765) yanaonyesha udhia alio nao dhidi ya umbeya. Hufika wakati arusini ambapo wanawari hupewa wasia. Kila aliye na dukuduku moyoni mwake hulitoa pale anapompa Kukuwa wasia (ub.904). Mtunzi anasema hapana mtafaruku, kwenda huku na huku kwa kuufanya udaku, kunong'ona vipembeni (ub.906). Mtunzi asema kuwa ni ila ya mwanamke kutia domo wenzake. Tabia hii huwa kama kanuni kwao (ub.881).

Toni ya furaha imetawala utenzi mzima. Toni hii inafungamana na sherehe za arusi zinazosimuliwa. Bila shaka msomaji hatarajii wingu la huzuni kutanda katika arusi. Ingawa utenzi ulianza kwa toni ya huzuni na wasiwasi kidogo kwa lile ambalo mamake

Kukuwa aliliona kama kuchelewa kwa kuposwa kwa mwanawe. Polepole toni hii inabadilika haswa watu wanapoanza kuja pale nyumbani wakitaka kumwona Kukuwa. Mama anang'amua kwamba kuna jambo jema laja. Kuanzia hapo, fununu na baadaye habari za posa zinawafikia. Arusi inapangwa na kilele cha furaha kinafika inapojibu.

4.5 MSUKO

Matukio katika utenzi huu yamepangwa kimfululizo na katika muumano ulio wazi. Hali hiyo inaufanya msuko wa utenzi kuwa sahili. Kuna ushahidi wa uhusiano wa kiusababishi unaotokana na tukio moja kulijenga tukio linalofuata kwa njia ya mantiki. Msanii anapoeleza utaratibu wa arusi, anamulika kuukeni na kuumeni, kila upande na wakati wake, akieleza yanayofanyika huko. Kabla hajaanza kueleza juu ya upande wowote ule, anamdokezea msomaji kuwa anaeleza kuhusu mtu au upande fulani. Tumenukuu baadhi ya beti ambazo ametumia mbinu ya kudokeza anachoeleza. Maelezo haya yametokea katika mishororo ya kwanza ya beti: ...Ndani kwa bw. arusi (ub.850), Upande ule wa mke (ub.364), ...Haya twende kwa mchumba (ub.301), ...Kule kwa kina Kukuwa (ub.411), ...Narudi kwa bi. Kukuwa (ub.871), ...Huku kwa Mwanakukuwa (ub.229) ...Na mume upande wake...(ub.690). Mtindo huu wa uandishi unaufanya msuko ueleweke kwa urahisi kwa sababu msomaji hupata kufahamu haraka tukio linaloelezwa na linakofanyika.

Baada ya mtindo wa kawaida katika tenzi wa kumtukuza Mungu katika beti za mwanzo mwanzo, msanii anaeleza kuwa anataka kuuendeleza utenzi ule wa kwanza (*Howani Mwana Howani*). Anaeleza kusudi la kuutunga utenzi huu (ub.8) kisha anaanza kuelezea kumhusu Kukuwa tangu alipomzaa, alivyomlea hata akafika umri wa kupelekwa

unyagoni. Alipomaliza unyago, akaja akatiwa ndani hadi alipokuja mtu akamposa, wazee wakatoa mahari na akafanyiwa arusi.

Msanii ametumia kaida mbalimbali kuuboresha msuko wa utenzi huu. Tutaangalia baadhi ya kaida alizotumia katika kazi yake. Msuko wa utenzi huu kwa kiasi kidogo, umejengwa kwa mbinu ya taharuki. Taharuki ni ile hali ya matarajio ambapo tuna hamu ya kutaka kujua kitakachotokea baadaye. Kimsingi, hii ni hali ya kuisimua inayompata na kumshika msomaji kiasi cha kuwa na hamu kubwa ya kutaka kujua hali au mambo ya baadaye.

Utenzi unianza kwa taharuki ya posa ya Mwanakukuwa, mama ameshikwa na wasiwasi ambao pia anamfanya msomaji kuwa na hamu ya kutaka kujua iwapo ataposwa. Washenga walipoambiwa na babu warudi baada ya miaka miwili ni jambo linalowaacha wazazi wa mume katika taharuki. Hawajui mahari watakayoitishwa na iwapo watakubaliwa kumchukua msichana.

Watu wa kuukeni wanakuwa katika taharuki Kukuwa anapokuwa ndani na bw. arusi. Hawajui iwapo arusi itajibu awafunue uso au aibu itaingia upande wao. Roho zao zinatua arusi inapojibu. Kauli ya babu kuwa washenga warudi baada ya miaka miwili pia inasababisha ukinzani. Baba anapomkanya mshenga kuwa hatofanya mambo kwa pupa, ni jambo linalosababisha ukinzani na linaloibua mbinu ya mshtukizo. Tunakumbuka kuwa kabla aje mshenga kuleta ule ujumbe, wazazi wa Kukuwa walikuwa na wasiwasi kumwona mwana wao akiwa ndani bila kuposwa. Matarajio ya msomaji hapa ni kwamba

baba atakubali ile posa haraka bila kuweka vikwazo vyovyote lakini matarajio hayo yanavunjwa.

Kaida nyingine ambayo imejenga msuko wa utenzi huu ni mbinu ya usababishi na tokeo. Hii ni kaida ambapo matukio yanafuatana kwa mpangilio wa kimuundo unaonyesha uhusiano wao wa kimantiki na ambao unategemea kusababishwa na tokeo la kusababishwa huko. Tunataraji kuwa tokeo tunaloliona katika kazi ya kifasihi limesababishwa. Utenzi unapoanza, tunakutana na mama aliye na wasiwasi mwingi uliosababishwa na kuweko kwa mwanawe nyumbani baada ya kutoka unyagoni. Mara anatokea mtu wa kumposa na hili lawafanya wazee wake na ukoo wao kukimbia huku na kule kwa mipango ya mahari na maandalizi ya arusi. Umuhimu wa somo katika arusi hiyo unamleta somo katika picha.

Msanii anaeleza mengi kumhusu somo na jukumu lake katika arusi. Majukumu ya manyakanga, wanawari na makungwi pia yanamulikwa. Kujibu kwa arusi pia kunausukuma utenzi mbele. Ufanisi huo unafuatiwa na mila nyingine nyingi zinazoambatana na ushindi huo. Msanii amefaulu katika kuwasilisha ujumbe wake kwa mhusika wa kike na jamii kwa jumla. Msimamo wake ni mmoja, mila na desturi zinazohusu ndoa zihifadhiwe. Matukio katika utenzi yana mantiki. Kila tukio linaoana na lingine kwa njia inayojenga mantiki na kuonyesha upatanifu na muungano wa kuwa kitu kimoja.

Msuko wa utenzi umejengwa pia kwa mbinu ya mgogoro. Mgogoro ni mvutano unaotokea kati ya wahusika fulani, katika akili ya mhusika, kati ya itikadi na mtazamo wa mhusika mmoja na mwingine na mengineyo. Msanii anaweza kuwa na aina tofauti ya migogoro katika kazi yake. Kiini cha mgogoro huwa ni mhusika anayetaka kukifikia au kukipata kitu fulani kisha pakawepo na kizuizi.

Utenzi unianza kwa mgogoro wa kisaikolojia katika akili ya mamake Mwanakukuwa. Mama anajiwazia mengi, hali wala halali, amekondeana kwa wasiwasi wa kuwa na mwanamwari nyumbani. Wasiwasi wake unamfanya kumshuku kila anayemtembelea kuwa amekujia umbea. Shwari inapatikana Kukuwa anapoposwa.

Mgogoro mwingine unatokea watu wa kuumeni wanapotaka mambo ya mahari na arusi yafanywe haraka haraka. Babake Kukuwa alipomweleza mshenga kuwa hangeweza kumjibu lolote hadi atakapowaona wazee wake, hakutulia, aliendelea kwenda huko kuulizia ni lini wangeleta mahari. Babake mume aliandika barua baada ya miezi sita akawatuma washenga kupeleka posa huku akiwa na wasiwasi kuwa huenda isikubaliwe. Walipokewa kwa akina Kukuwa lakini babu akawaambia wangoje kwa muda wa miaka miwili.

Haikuisha ile miaka miwili, wakaja baada ya mwaka mmoja, wakitaka kujua lini wangeleta mahari. Ingawa pia walipokelewa vizuri, mgogoro mdogo ulizuka kuhusu kiasi cha mahari. Watu wa mke walianza kutoa maelezo mengi ya imani yao kuhusu mahari na ndoa kwa misingi ya dini ya kiislamu. Watu wa mume walionyesha kukereka na

baadaye babu akasema kiwango cha mahari waliyohitaji. Kauli ya babu ilirejesha shwari na palepale ikapangwa siku ya kuletwa mahari ile. Mipango ya arusi pande zote mbili ikanoga, watu wakaingia katika shamrashamra za maandalizi.

Mgogoro mwingine unaodhihirika, na ambao wahakiki wengi huupuza ni ule wa msanii. Tumetathmini kuwa, ili msanii afikie kuandika kazi huwa kuna jambo lililomkera siku nyingi ndipo akaamua kulizungumzia kupitia uandishi. Tuliposoma kazi ya Bi. Zaynab Himid Mohammed, tunagundua kuwa, anaisihi jamii kurejelea mila na desturi zake.

Nasaha hizi zinatokea waziwazi anaporejelea mambo yalivyofanywa zamani. Zaynab alikuzwa katika misingi ya ulezi wa wasichana wa Kiswahili. Katika kipindi alichishi, wageni wa kizungu walikuwa washaanza kuingia kisiwani Unguja na akawa na nafasi ya kupata elimu ya kimagharibi. Kuja kwa elimu ya kimagharibi kisiwani huenda kulisababisha kuanza kusahaulika kwa misingi ya utamaduni wa Kiswahili na dini ya kiislamu kuhusu kukua kwa mtoto wa kike na mambo yanayofungamana na ndoa. Jambo hili laeleza vyema ilhamu ya mtunzi ya kuutunga utungo huu. Utungo huu unasaidia kuleta shwari akilini mwake akijua kuwa ameuandika ili wajao wabahatike kujifunza utamaduni.

4.6 MANDHARI

Mandhari ya usimulizi yanabainika wazi katika utenzi. Anasimulia mazingira ya kitamaduni juu ya malezi ya mtoto wa kike tangu anapokuwa unyagoni, anapotoka, hadi anapoposwa na kuolewa. Mazingira ya kimalezi ya msichana wa Kiswahili

yamesimuliwa katika utenzi wote. Malezi hayo hufungamana na utamaduni wa Kiswahili.

Mwanakukuwa alikaa ndani, hakutoka wala kuonekana nje alipotoka unyagoni, hadi walipokuja kwao washenga kumposa na akaolewa. (ub.4-184). Malezi hayo hufungamana na utamaduni wa Kiswahili na misingi ya dini ya kiislamu, kwa hivyo kuna mandhari ya dini pia. Kila mhusika wakiwemo kina baba, mama na somo wanaomba dua katika kila hatua ya arusi. Mazingira yao ni ya kutoaminiana, watu wana husuda na uwezo wa kutia nuksani mambo yakimwendea vizuri mtu kama Kukuwa anavyoelezwa na somo pamoja na mamake. Wanazuia vijicho na nuksani hizo kwa dua nyingi, mafusho, kumzunguwa na kumweua bi. arusi.

Haya ni mandhari ambayo ndoa zimejengeka kwenye misingi na imani za kitamaduni na kidini. Kur'ani Tukufu inasisitiza kuheshimiwa kwa mwanamume na mwanamke. Ni kwa misingi hii, ambapo watunzi waislamu wa tenzi walisitiza na hata kutilia chumvi jambo hili na kumpa mwanamke usawiri hasi. Bi. Zaynab kama wenzake waliomtangulia anasisitiza kuwa mwanamke daima awe chini ya mume. Mwanamke anatarajiwa kumzungumzia mumewe polepole pasi kelele kwa sababu wanaume hawapendi kelele, kuwapokea kwa maneno matamu wanaporudi nyumbani hata ikiwa una ugomvi nao, kuwakanda, kuwapepea na kuwaonyesha mapenzi. Utenzi umejaa wasia wa aina hii kwa bi. arusi kutoka kwa mamake, somo na makungwi wake.

Mbali na kufungamanishwa na tabia, imani na utamaduni wa wahusika, mandhari yaweza kuwa ya kimazingira (mahali panapowasilishwa wahusika). Katika utenzi, kuna

mazingira mapana ya kisiwa cha Unguja ambapo ndipo makao ya mtunzi. Mtunzi anatupa taswira ya maisha ya mtoto wa kike kisiwani na hali ya mambo katika kipindi hicho cha kihistoria alipotunga utenzi huo. Inabainika wazi katika mishororo ya utenzi na toni ya mtunzi kuwa, itikadi zinazohusu malezi na ndoa za Kiswahili zilikuwa zimeanza kusahaulika ndipo mtunzi akaona haja ya kuzitia katika kumbukumbu kwa kuziandika.

Taswira ya mandhari finyu inadhihirika unyagoni ambapo mtunzi ameyaelezea japo kwa kifupi. Anaangazia yanayofanyika huko na wanayofunzwa wanawari (ub.9-25). Baadaye anatupeleka nyumbani kwa akina Kukuwa ambako haelezi taswira ya nyumba yao isipokuwa kutuonyesha Mwanakukuwa na mamake wakiwa jikoni kila wakati wakikuna nazi au wakizichagua chuwa. Mandhari mengine anayotupeleka na kuelezea kwa kina mtunzi ni ya arusi. Anaeleza mila zote zinazoambatana na arusi hiyo. Anaeleza kwa kina kila hatua ya arusi kimantiki huku akieleza na kutaja mapochopocho ya vyakula vilivyoliwa. Mapambo ya bi. arusi yanaelezwa pia na kuchora picha ya arusi za Kiswahili isiyosahaulika na msomaji.

4.7 WAKATI

Msanii amebana matukio kiwakati. Mbinu hii hutumiwa katika ushairi kwa sababu ya sifabia ya utunzi wa mashairi ya kueleza mambo kwa njia ya mkato. Tutaangalia wakati katika upana wake kwa kurejelea kipindi cha kihistoria ambacho kazi hii ilitungwa. Kipindi hiki ndicho msingi mkuu wa kazi hii. Kinatusaidia kubaini hali ya mambo ilivyokuwa wakati huo.

Msanii alitunga kazi hii katika karne ya ishirini, baada ya bara la Afrika kuathiriwa na utamaduni wa kimagharibi kupitia kwa mifumo yao kielimu, kitamaduni, kiuchumi na kifalsafa. Kutokana na toni yake katika utenzi, ni rahisi kubaini kuwa alikuwa akiwasihi wasomaji kurudia utamaduni. Katika beti ambazo yeye mwenyewe alitoa usimulizi na hata kupitia kwa wahusika wake, alikuwa akieleza matukio katika arusi na baadaye kumkumbusha msomaji kwamba ndivyo mambo yalivyokuwa yakifanywa zamani. Uteuzi wake wa maneno kama mila, utamaduni, zamani, siku za mababu zetu na mengineyo ni ithibati kuwa utamaduni ulikuwa umeanza kusahauliwa.

Msanii alitumia njeo zote katika utungo wake. Hali ya mazoea imetanda kote katika utenzi. Huenda nia yake ya kutumia hali hiyo ni kusesitiza kuwa mambo anayoyasimulia yalikuwa mazoea ya watu wa zamani wala hawakushinikizwa kuyafanya.

Kipengele kingine cha wakati kinahusu muda ambao matukio katika utenzi yamechukua kuwasilishwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa usimulizi. Matukio hayakuelezwa kikamilifu. Mengi yamedondoshwa na mengine kuangaziwa tu kwa ufupi. Wakati katika utenzi huu umeelezwa na mwandishi, wahusika na kupitia mbinu rejeshi. Matukio katika utenzi, tangu mwanamwari aondoke unyagoni hadi anapoolewa yalichukua karibu mwaka mmoja na nusu. Tumefikia takwimu hii baada ya kukadiria wakati yaliyochukua matukio haya katika beti zifuatazo: (21, 205, 207, 305, 348, 684, 736, 804, 809 na 1084). Wakati yaliyochukua matukio hayo yote umefumbatwa katika utenzi na kuonekana kama yaliyochukua masaa mawili au matatu.

Mbali na idadi ya miezi, miaka na siku zilizotajwa kama muda ambao matukio yalichukua kutendeka, tumegundua kuwa yalikuwa yanatendeka wakati wa usiku. Tumegundua pia kuwa siku saba ni muhimu katika kalenda ya arusi za Kiswahili. Aghalabu kila tukio huchukua siku saba kutimiza: Mwanamwari anaishi unyagoni siku saba (ub.21), tiba ya mwanamwari baada ya kuonana na mumewe huchukua siku saba (ub.684), fungate huchukua siku saba (ub.736), lima ya kuukeni na kuumeni huchukua siku saba kila mojawapo (ub.564, 804, 809).

Licha ya nyakati hizi mbili: Wakati mpana wa kihistoria na ule wa matukio katika kazi, kuna wakati matini. Huu ni wakati anaouchukua msomaji fulani kuisoma kazi. Wakati matini hutofautiana kwa sababu wasomaji wana kasi zinazotofautiana.

Usimulizi wa utenzi huu ni wa kufululiza. La kwanza limekuja mwanzo na la mwisho likaja mwisho; mtindo ambao umerahisisha uelewa wa utenzi. Mbinu rejeshi imetumiwa katika utenzi mzima. Arusi iliyoelezwa ni ya kitamaduni, mtunzi ameturejesha nyuma kutupa taswira ya malezi ya mtoto mswahili wa kike na haswa arusi yake.

Tukiuweka utenzi huu katika muktadha na mazingira ya nyakati alizoutunga mtunzi, tunatambua uzuri na umuhimu wake. Kwa jamii ya Waswahili, utungo huu ni hazina ya nyakati zote kwa sababu una mambo mengi yanayohusu mila na itikadi za malezi ya mtoto wa kike.

4.8 USIMULIZI

Usimulizi katika utenzi huu ni wa kufululiza. Umetiririka kwa njia iliyo rahisi kufuata. Usimulizi ulio katika utenzi ni wa kitamthilia. Wahusika wanazungumza moja kwa moja (usimulizi wa nafsi ya kwanza) na wanashiriki katika matukio utenzini huku mtunzi akiwa kama mwelekezi wa matukio. Anatoa maelezo kabla ya mhusika kutoa usimulizi. Baba, mama, somo, bibi, babake mume na wahusika wengineo wanazungumza moja kwa moja. Msanii anatumia nafasi yake ya usimulizi kuisisitiza ujumbe wake, kuwatania, kuwabeza na hata kuwafokea wahusika wake.

Mtunzi ni msimulizi-mwandishi. Usimulizi wa aina hii ni wa nafsi ya mtu wa tatu. Anaelewa jamii anayoizungumzia vizuri. Anaeleza kwa kina mtazamo alio nao kuhusu anayoyazungumzia. Amesimulia sana mambo yanayomhusu Mwanakukuwa kwa vile ni mhusika bubu na kueleza mila na itikadi za Kiswahili. Mbali na mtunzi kumsimulia msomaji kisa, wahusika pia wamefanya vivyo hivyo (ub.28-37). Utenzi una aina tatu ya usimulizi; wa nafsi ya kwanza, wa nafsi ya pili na wa nafsi ya tatu. Mtunzi amechanganya aina zote za usimulizi katika kazi yake na kuufanya utenzi umwathiri msomaji kwa njia ambayo anafikia kuzithamini itikadi na mila zinazorejelewa. Anavunja mazoea ya usimulizi wa mtu mmoja ambao pia waweza kumchosha msomaji. Mtunzi pamoja na wahusika wake wanazungumza kauli moja ambayo pia ni mbinu mojawapo ya kufanya kazi iaminike kwa sababu maelezo yake yanamulikwa na kuisisitizwa na wahusika wake. Usimulizi wa nafsi ya pili unadhihirika sana katika wasia ambao mama, somo na mtunzi wanawapa wasomaji na Mwanakukuwa katika utenzi.

Usimulizi aliotoa mtunzi si wa kiubunifu. Utamaduni ambao amerejelea kwa msistizo ni wa kihalisia na alikuwa akimulika hali ya kuzorota kwa utamaduni huo katika kipindi alichotunga kazi yake. Mwandishi amejitokeza kwa njia wazi kuyasema mambo na kutoa maoni yake. Anaelekea kumwelekeza msomaji kwenye mtazamo alioupendekeza yeye mwenyewe kuwa ndio ulio sahihi.

4.9 HITIMISHO

Katika sura hii tumehakiki fani katika *Utenzi wa Mwanakukuwa* kwa kurejelea mifano katika utenzi wenyewe. Kama tulivyoona kutokana na data yenyewe, kazi imejengeka kwa vijenzi vyote vya fani vinavyojenga muundo wa ndani na wa nje wa shairi. Tumbainisha kwamba kazi imetambuliwa kama utenzi wala si tamthilia au riwaya kwa sababu ina sifabia zinazoitambulisha na utunzi wa tenzi. Baadhi ya sifabia hizo ni: Uwasilishaji wa ujumbe kwa mkato, uzingatiaji wa vina, mizani na mishororo na matumizi ya lugha kisanii pamoja na msamiati wa kirasimi. Msanii ametumia ufundi wa kiwango cha juu kisanaa na pia kuhifadhi kaida za utunzi wa mashairi kwa mujibu wa wanamapokeo.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO

Katika tasnifu hii tumeshughulikia *Tenzi za Mwanakukuwa na Howani Mwana Howani*. Utenzi mmoja unaendeleza mwingine. Mtunzi wa tenzi Bi. Zaynab Himid Mohammed amechangia pakubwa katika fasihi ya Afrika Mashariki na Bara la Afrika kwa kutunga tungo ambazo ujumbe wake ni hazina yenye thamani kwa vizazi vya sasa na vijavyo vya jamii za Kiswahili.

Tumehakiki tenzi hizi kifani kwa kuchunguza jinsi Bi. Zaynab alivyotumia vipengele mbalimbali vya fani kuunda tenzi. Tumetaja na kufafanua vipengele vinavyojenga fani katika sura ya pili. Katika sura ya tatu tumeuhakiki *Utenzi wa Howani Mwana Howani* kifani. Tumegundua kuwa utenzi huu umejengeka kwa misingi ya fani. Tumehakiki fani katika *Utenzi wa Mwanakukuwa* katika sura ya nne. Tumetambua kuwa, mbali na hisia ya wahakiki wengi kuwa uhakiki wa kimuundo hauiakisi jamii, utafiti wetu unaelekea kukataa mawazo hayo. Vipengele vya fani vinaakisi jamii anayoilenga mtunzi, vipengele hivyo huchotwa katika jamii. Tukirejelea vipengele vya wahusika, mandhari na matumizi ya lugha tunapata kuwa msomaji anaweza kuitambua jamii inayozungumziwa ilivyo kwa kurejelea vipengele tulivyovitaja. Hata hivyo misingi ya nadharia tuliotumia kuihakiki kazi hii haituruhusu kufanya urejelezi wa nje ya kazi. Msanii ameitunga utungo huu kwa misingi ya vipengele mbalimbali vya fani. Matumizi ya vipengele vya fani katika tenzi zote mbili hayana tofauti. Kwa muhtasari, uchunguzi wetu umebainisha kuwa:

1) Tenzi zote mbili zina muundo wa ndani na wa nje. Muundo wa nje ni umbo la utenzi. Hiki ndicho kipengele kikuu ambacho huli tofautisha shairi na kazi nyingine za kifasihi. Ni kipengele ambacho hufanya utenzi uitwe utenzi wala si tamthilia wala riwaya. Umbo hujumlisha vijenzi vyake kama beti, mishororo, mizani, vipande, vina na kibwagizo. Vijenzi hivi huvipa utenzi sura na muundo wa kipekee.

Hatukutambua muundo wa ndani kwa kuzitazama tenzi tu. Tulizisoma na kuzitathmini kwa makini ndipo tukagundua kwamba zimebeba vipengele vingi vya fani vinavyojenga muundo wa nje. Vipengele hivyo ni wahusika, mandhari, usimulizi, wakati, toni, msuko na matumizi ya lugha. Msanii ametumia vipengele hivi kwa ustadi wa kiwango cha juu. Kupitia kwa vipengele hivi amefanikiwa kuwasilisha ujumbe wake, kuchora taswira ya jamii anayoizungumzia na kuvuta nadhari ya wasomaji.

2) Tumegundua kuwa usawiri wa wahusika ni wa kuaminika. Msanii amewaumba wahusika ambao matendo na tabia zao zinaakisi mienendo ya wanajamii katika ulimwengu wa kihalisia. Msanii hajawataja wahusika wake kwa majina isipokuwa Sihadaike, Mwanakukuwa na Bi. Mrashi. Wale wahusika wengine wanarejelewa kama baba, mama, shangazi, mshenga, bibi, babu, majirani, jamaa, somo na manyakanga. Msanii hakueleza sifa za wahusika kwa kina kama tuonavyo katika riwaya na tamthilia. Pengine amefanya hivyo kwa sababu ya sifa ya mashairi ya kueleza mambo kwa mkato. Wahusika waliosawiriwa kwa kina ni wahusika wakuu peke yao na wale anaowatumia kuwasilisha ujumbe muhimu. Wahusika katika *Utenzi wa Mwanakukuwa* ni wengi kuliko wale walio katika *Utenzi wa Howani Mwana Howani*. Mtunzi amewapa wahusika katika *Utenzi wa Mwanakukuwa*

nafasi ya kuzungumza moja kwa moja. Tumepata kujua sifa za wahusika kupitia maelezo ya msanii kuwahusu, matendo na mazungumzo yao wenyewe kwa wenyewe na wanayosema kujihusu na kuwahusu wenzao. Katika *Utenzi wa Howani Mwana Howani*, mhusika mmoja, mamake Sihadaike ndiye anayetawala usimulizi na wengine wanazungumza tu kwa kifupi.

3) Katika utafiti wetu, tumebaini kuwa tenzi zina mandhari mbalimbali yanayodhihirika. Mandhari yaliyotawala tenzi zote ni ya kitamaduni na dini. Mandhari tuliyoyaona katika tenzi yanavumbuliwa kwa hatua baada ya nyingine kupitia maelezo na matukio. Mandhari haya yanawasilishwa kwa njia tofauti na tamthilia au riwaya ambapo mandhari huwasilishwa kwa maelezo ya kina punde tu msuko unapochukua mkondo mpya. Katika tenzi, mtunzi ameyazungumzia maisha ya mtoto wa kike wa Kiswahili kuanzia anapozaliwa hadi anapolewa. Malezi na kukua kwa mtoto huyu kunafungamana na dini ya kiislamu pamoja na utamaduni wa Kiswahili. Mtunzi anahamishahamisha mandhari kutoka mahali pamoja hadi pengine. Kuna mandhari mapana ya kisiwa cha Unguja ambayo pia yanadhihirika katika tenzi. Msanii amechora taswira ya mandhari finyu ya chumba ambacho mamake Sihadaike alijifungulia na kukaa kwa siku arobaini hadi mtoto alipotolewa nje, sebuleni kwa akina mamake Sihadaike, chuoni, unyagoni na nyumbani kwa akina Mwanakukuwa. Msanii hakuelezea mandhari kwa kina, aliyaangazia tu. Kila tukio linatokea katika mandhari mwafaka yanayofungamana na matukio yanayoshuhudiwa.

4) Tumegundua kuwa misuko ya tenzi zote mbili ni sahili. Usahili huu umetokea kwa sababu ya mtiririko na mfuatano wa matukio unaoeleweka kwa urahisi. Licha ya kuwa kila utenzi ulitungwa wakati tofauti na mwingine, usahili wa misuko yake unazifanya

zionatekane kama kazi zilizotungwa wakati mmoja. Ingawa kuna misuko mingine midogo katika msuko mkuu wa tenzi zote mbili, hiyo midogo inaisukuma hadithi mbele. Misuko midogo katika *Utenzi wa Howani Mwana Howani* inatokea kwa sababu ya mighani inayosimuliwa na mamake Sihadaike. Misuko midogo katika *Utenzi wa Mwanakukuwa* inazuka kutokana na migogoro inayotokea. Hata hivyo misuko hii inasaidia katika kuujenga msuko mkuu ambao umewekwa dhahiri katika tenzi zote. Msomaji anaweza kuyafuata na kuyaelewa masimulizi ya malezi na arusi ya msichana wa Kiswahili kwa urahisi kwa kuwa, misuko ya tenzi ni sahili na inadhihirika wazi.

5) Tumbaini kuwa msanii alitumia lugha kwa ustadi mkubwa wa kisanii kutunga kazi inayovuta nathari na kugusa hisia za msomaji. Matumizi yake ya lugha yanasaidia kuitofautisha kazi yake na kazi nyingine zisizo za kifasihi. Bi. Zaynab ametumia lugha kitaswira kuchora picha ya yale anayoyasimulia katika akili ya msomaji na kuacha athari isiyosahaulika. Licha ya kufundisha, kazi yake inaburudisha pia kwa sababu ya usanii mkuu wa lugha alioutumia. Tamathali mbalimbali za usemi zimetumiwa na mtunzi katika tenzi zote na kuifanya kazi yake iwe ya mvuto isiyochosha akili ya msomaji na kumfanya awe na hamu ya kutaka kusoma zaidi. Ujumi wa kazi hii unadhihirika kupitia matumizi ya hizi tamathali za usemi. Matumizi ya lugha ya kishairi yamedhihirika katika tenzi. Lugha ya kishairi ni lugha maalum inayotofautisha mashairi na kazi nyingine za kifasihi. Msanii ameonyesha ustadi kwa kutumia lugha kwa misingi ya mbinu za uhuru wa kishairi kama vile mazida, inkisari, tabdila na mpinduo sarufi. Mbinu hizi zimemsaidia kufikia mahitaji ya utunzi kwa misingi ya kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo. Katika utafiti wetu, tumegundua kuwa msanii ametumia msamiati kutoka lahaja mbalimbali za Kiswahili zikiwemo Kimvita, Kingozi na Kiamu. Matumizi ya msamiati

wa lahaja yamesalia sana katika utunzi wa mashairi. Watunzi wengi wa mashairi ni wazawa wa pwani kwa hivyo ni wazungumzaji wenyeji wa lahaja hizi. Matumizi ya lahaja hizi katika utunzi wao ni jambo la kawaida. Huenda pia watunzi hutumia msamiati wa kilahaja kwa madhumuni ya kuuhifadhi ili usipotee katika kumbukumbu ya wasemaji wa lugha ya Kiswahili.

Nadharia ya umuundo ina uwezo wa kuhakiki fani na kwa hivyo tumefaulu katika kueleza na kuhakiki fani katika *Tenzi za Howani Mwana Howani* na *Mwanakukuwa* kwa misingi ya nadharia hii. Nadharia hii imejikita katika uhakiki wa kimuundo wa tenzi pasipo urejelezi wa nje. Utafiti wetu ulijikita katika uhakiki wa matini kimuundo. Tumegundua kuwa uhakiki wa kimuundo ni wa kimsingi sana katika kazi za kifasihi kwa sababu ndio hutofautisha kazi za kifasihi na kazi nyingine kama vile za uandishi wa magazeti, insha, ripoti na nyinginezo.

Nadharia zetu tete katika **1.3** zilikuwa tano, tumezajaribu na tukapata kuwa zote tano zina mashiko katika uhakiki wa tenzi hizi. Katika utafiti wetu tumegundua yafuatayo:

1. Tenzi zina muundo wa ndani kwa sababu ya kuwepo kwa vipengele vifuatavyo vya fani katika kazi: Wahusika, mandhari, toni, wakati, usimulizi, matumizi ya lugha na msuko. Kipengele cha umbo katika kazi ndicho kinachodhihirisha kuwepo kwa muundo wa nje.
2. Sifa za wahusika zinadhihirika katika maelezo ya msanii kuwahusu, matendo yao pamoja na mazungumzo yao wenyewe kwa wenyewe.

3. Msanii ametumia mandhari mapana na finyu kutegemea matukio na wahusika. Mandhari aliyoyatumia yanafungamana na mila na itikadi za jamii.
4. Msuko katika tenzi zote ni sahili. Msanii anaeleza kisa moja kwa moja kwa mfululizo unaoeleweka haraka.
5. Msanii ametumia lugha kisanaa na kishairi. Tumegundua kuwa matumizi yake ya lugha ni ya kiwango cha juu. Jambo ambalo limeifanya kazi yake iwe ya kuvutia.

5.1 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umejikita katika uhakiki wa fani katika *Tenzi za Howani Mwana Howani* na *Mwanakukinwa*. Kuna haja ya tenzi hizi kufanyiwa uhakiki linganishi wa kimaudhui na kimuundo. Hatungeweza kuzifanyia tenzi hizi uhakiki wa kimaudhui au kuhakiki nafasi ya mwanamke katika jamii kwa sababu ya wakati kwani kazi yetu ilihusu uhakiki wa kifani. Mambo haya ni muhimu lakini yako nje ya upeo na mipaka ya kazi yetu. Yanahitaji kufanyiwa utafiti.

Tumeona kuwa ipo haja ya wasomi watakaokuja baadaye kufanya uhakiki linganishi wa matumizi ya lugha katika tenzi na mashairi ya kisasa. Lugha inayotumiwa katika tenzi na uhusiano wake na matawi mengine ya kifasihi ni swala linalohitaji utafiti zaidi pia.

Katika utafiti wetu tumegundua kuwa baada ya mashairi kuondolewa misikitini, tenzi zilichukua muundo mpya kifani. Tunapendekeza kuwa fani katika tenzi za zamani ishughulikiwe kwa kuilinganisha na tenzi za hivi karibuni.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M.H. (1968) 'A note on the form of the language of the poem,' uk.81-83 katika Lienhardt, P (mhariri) *The Medicineman*.
- Abedi, K.A. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*.
- Allen, J.W.T. (1971) *Tendi*, London : Heinemann
Nairobi: KLB.
- Aristotle, (1987) *The Poetics of Aristotle*. Stephen Halliwell (trans)
London : Duckworth.
- Chiraghdin, S.
na Mnyampala, M. (1977) *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: OUP.
- Dammann, E. (1940) *Utenzi wa Fatuma*. Dichtungen in der Lamu-
Mundart des Suaheli. Hamburg : Friednchsen, de
Gruyter & Co.
- Dorsch T.S. (1965) *Aristotle/ Horace/Longinus: Classical Literary
Criticism*.
Harmondsworth: Penguin.
- Eco, U (1976) *A Theory of Semiotics*. Indiana University Press.
- Forster, E.M. (1927) *Aspects of the Novel*. London : Penguin Books.
- Gill , R. (1985) *Mastering English Literature*. London: The Macmillan
Press Ltd.
- Habwe, J. na
Karanja, P. (2007) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix
Publishers.
- Hawthorn, J. (1994) *A Concise Glossary of Contemporary Literary
Theory (2nd edition)*. London: Edward Arnold.
- Harries, L. (1962) *Swahili Poetry*. OUP : Oxford.
- Holman, C.H. (1960) *A Handbook to Literature*. NewYork: The Odyssey
Press Inc.

- Kazungu, E.K. (1982) *Deviation and Foregrounding in Chosen Swahili Literary Texts: Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi* (haijachapishwa).
- Khatib, M.S. (1985) 'Mwana Kupona', uk.46 -52 katika *MULIKA Na.16* Dar es Salaam: TUKI.
- Knappert, J. (1979) *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology*. London: Darf Publishers.
- _____.(mhariri) (1964) *Four Swahili Epics*. Leiden: DRUKKERIJ LUCTOR ET EMERGO.
- _____ (1972) *An Anthology of Swahili Love Poetry*. California: University of California Press.
- _____ (1967) *Traditional Swahili Poetry: An Investigation into the Concepts of E. African Islam as reflected in the Utenzi*. Leiden: E.J. Brill Publishers
- _____ (1983) *Epic Poetry in Swahili and other African Languages*. Leiden: E.J Brill Publishers.
- Leech, G.N. and Short, M.H. (1981) *Style in Fiction. A linguistic Introduction to English Fictional Prose*. New York: Longman Group.
- Lienhardt, P.(ed) (1968) *The Medicineman*. Oxford: Clarendon Press.
- Lyndon, H. (1962) *Swahili Poetry*. London: Oxford University Press.
- Maina, V. (2005) *Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi mbili za Shabaan Robert: Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili*. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa)
- Massamba, D.P.B. (1983) *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili, toleo la tatu*. Dar es Salaam: TUKI. Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).
- Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Fotoform Ltd.

- Mohammed, S.A. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: E.A.E.P.
- Mohammed, Z.H. (1983) *Howani mwana Howani*. Dar es Salaam: TUKI.
- _____ (2004) *Mwanakukuwa*. Dar es Salaam: TUKI.
- Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: E.A.E.P Ltd.
- Mungai, P. (2005) *Ulinganishi wa Kifani wa Tenzi za Swifa ya Nguvumali na Mikidadi na Mayasa*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (hajachapishwa).
- Murray, P. (1978) *Literary Criticism: A Glossary of Major Terms*. New York: Longman Group.
- New York: OUP, (2005) *Oxford Advanced Learners Dictionary, 7th ed.*
- Njogu, K.
na Chimerah R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: J.K.F.
- Noor, I. (1972) *Utenzi wa Qiyama*. Nairobi: Heinemann Books.
- Olali, T (2004) *The Veneration of The Prophet: The Role of Kasida ya Hamziyya During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago, Kenya*. Tasnifu ya PhD (hajachapishwa).
- Peck, J. na Coyle, M. (1984) *Literary Terms and Criticism*. London: Macmillan Education Limited.
- Richards, I.A. (1964) *Practical Criticism: A study of Literary Judgment* London: Routledge.
- Senkoro, F.E.M.K. (1982) *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity.
- TUKI, (2006) *English Swahili Dictionary 3rd Edition*, Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI, (1990) *Kamusi ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

- Wa Mberia, K. (1989) 'Fumo Liyongo', uk.25- 43 katika *MULIKA Na.21* Dar es Salaam: TUKI.
- Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- _____ (1996) *Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry, Kasida ya Burudai*. Tasnifu ya PHD: Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani (haijachapishwa).
- _____ (1999) *Sira ya Majagina: Buddha na Muhhamadi*: Mswada Uliowasilishwa katika Semina ya Swahili Colloquism. Universität Bayreuth, (Mei 14-15, 1999).
- _____ (2002) *The Epic of Princess Fatuma* (Mswada)
- _____ (2003) *The Epic of the Secret of all Secrets* (Mswada)
- _____ (2005) *Utenzi wa Hamziyyah*. Dar es Salaam: TUKI.
- _____ (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.
- Wa Mutiso, K. (1985) *Hurafa na Uyakiniifu katika Hamziyyah*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).
- Wellek, R. na
Warren, A. (1949) *Theory of Literature. A Seminal Study of the Nature and Function of Literature in all its Contexts*. Harmondsworth: Penguin Books Ltd.
- Werner, A. (1932) *The story of Miqdad and Mayasa*. Hampshire: The Azania Press.
- Wesah E. (2005) *Uhakiki wa Kifani katika Utenzi wa Siri Li Asirali na Mwana Fatuma*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).